JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**

# TAARIFA YA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI KUHUSU UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI, 2015




Posta House
7 Mtaa wa Ghana,
S.L.P. 10923,
**11300 Dar Es Salaam,**
**Tanzania**

**Simu:** +255 22 2114963-6
**Nukushi**: +255 22 211674
**Tovuti**: www.nec.go.tz
**Barua pepe:** uchaguzi@nec.go.tz

Tume ya Taifa ya Uchaguzi
Posta House
7 Mtaa wa Ghana,
S. L. P. 10923,
**11300 Dar Es Salaam**

© Tume ya Taifa ya Uchaguzi, 2016

**ISBN 978 – 9976 – 9957 – 0 – 1**

Imepigwa chapa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, Dar Es Salaam - Tanzania

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili au kutoa kitabu hiki kwa njia yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi

**YALIYOMO**

**ORODHA YA MAJEDWALI** .................................... **VII**
**ORODHA YA VIAMBATISHO** .................................... **VIII**
**ORODHA YA MICHORO** .................................... **IX**
**ORODHA YA RAMANI** .................................... **X**
**ORODHA YA CHATI** .................................... **XI**
**VIFUPISHO VYA MANENO** .................................... **XII**
**SHUKRANI** .................................... **XIV**
**BARUA YA UWASILISHAJI** .................................... **XV**
**DIBAJI XVIII** .................................... **XVIII**
**MUHTASARI WA TAARIFA** .................................... **XIX**
**SURA YA KWANZA** .................................... **1**
**UTANGULIZI** .................................... **1**

1.1 Jamhuri ya Muungano wa Tanzania .................................... 1

1.2 Mfumo wa Siasa Tanzania .................................... 3

1.3 Mfumo wa Uchaguzi Tanzania .................................... 3

1.4 Mzunguko wa Uchaguzi Tanzania .................................... 4

1.5 Tume ya Taifa ya Uchaguzi .................................... 6
1.5.1 Muundo wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi .................................... 7
1.5.2 Dira na Dhima ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi .................................... 10
1.5.2.1 Dira .................................... 10
1.5.2.2 Dhima .................................... 10
1.5.3 Majukumu ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi .................................... 10
**SURA YA PILI** .................................... **11**
**MAANDALIZI YA UCHAGUZI** .................................... **11**

2.1 Gharama za Uboreshaji wa Daftari la Wapiga Kura na Uchaguzi Mkuu .................................... 11
2.1.1 Gharama za Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura .................................... 11
2.1.1.1 Ununuzi wa Vifaa vya Uboreshaji wa Daftari la Wapiga Kura .................................... 11
2.1.2 Gharama za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015. .................................... 12
2.1.2.2 Uchapishaji wa Nyaraka za Uchaguzi .................................... 13
2.1.3 Mchango wa Washirika wa Maendeleo .................................... 13

2.2 Ratiba ya Uchaguzi Mkuu ..... 14
2.3 Marekebisho ya Sheria na Nyaraka nyingine za Uchaguzi ..... 15
2.3.1 Sheria za Uchaguzi ..... 15
2.3.2 Kanuni za Uchaguzi ..... 15
2.3.3 Maadili ya Uchaguzi ..... 16
2.3.4 Maelekezo kwa Watendaji na Wadau wa Uchaguzi ..... 17
2.4 Majimbo ya Uchaguzi ..... 17
2.4.1 Vigezo vya Ugawaji Majimbo ..... 19
2.4.2 Taratibu za Ugawaji wa Majimbo ..... 19
2.4.3 Majimbo Mapya ya Uchaguzi ..... 20
2.4.4 Majimbo yaliyobadilishwa Majina ..... 22
2.5 Kutangazwa kwa Kata za Uchaguzi ..... 23
2.6 Ugawaji na Usambazaji wa Vifaa ..... 23
2.7 Watendaji wa Uchaguzi ..... 24
2.7.1. Watumishi wa Tume ..... 24
2.7.2 Uteuzi wa Watendaji wa Uchaguzi ngazi ya Mkoa, Halmashauri, Jimbo, Kata na Vituo ..... 24
2.8 Mafunzo kwa Watendaji ..... 26
2.8.1 Mafunzo kwa Watumishi wa Tume Makao Makuu ..... 26
2.8.2 Mafunzo kwa Watendaji wa Ngazi ya Mkoa, Halmashauri, Kata na Vituo. ..... 27
2.9 Elimu ya Mpiga Kura ..... 27
2.9.1 Utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura katika Uchaguzi wa mwaka 2015 ..... 27
2.9.2 Uratibu wa Asasi za kutoa Elimu ya Mpiga Kura ..... 30
**SURA YA TATU ..... 31**
**UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA ..... 31**
3.1 Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ..... 31
3.1.1 Teknolojia iliyotumika Kuandikisha Wapiga Kura ..... 31
3.1.2 Upokeaji wa BVR *Kits* ..... 33
3.2 Uandikishaji wa Majaribio. ..... 34
3.2.1 Matokeo ya Uandikishaji wa Majaribio. ..... 34
3.2.2 Hatua zilizochukuliwa ..... 35

3.3 Uandikishaji wa Wapiga Kura ..... 35
3.4 Uwekaji Wazi Daftari la Awali la Wapiga Kura ..... 36
3.4.1 Matokeo ya Zoezi la Uwekaji Wazi Daftari la Awali la Wapiga Kura ..... 37
3.4.2 Uchapishaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na Orodha ya Wapiga Kura ..... 40
3.5 Mafanikio ya Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ..... 40
**SURA YA NNE ..... 41**
**UTEUZI WA WAGOMBEA NA KAMPENI ZA UCHAGUZI ..... 41**
4.1 Uteuzi wa Wagombea ..... 41
4.2 Uteuzi wa Wagombea wa Nafasi ya Kiti cha Rais na Makamu wa Rais ..... 41
4.2.1 Pingamizi kwa Wagombea wa Nafasi ya Kiti cha Rais ..... 44
4.3 Uteuzi wa Wagombea Ubunge ..... 44
4.3.1 Pingamizi dhidi ya Uteuzi wa Wagombea Ubunge ..... 46
4.3.2 Rufaa kwa Tume ..... 46
4.3.3 Mgombea Aliyepita Bila Kupingwa ..... 47
4.4 Uteuzi wa Wagombea Udiwani ..... 47
4.4.1 Pingamizi Dhidi ya Uteuzi wa Wagombea Udiwani ..... 49
4.4.2 Rufaa Dhidi ya Wagombea Udiwani ..... 49
4.4.3 Wagombea wa Nafasi ya Udiwani Waliopita Bila Kupingwa ..... 50
4.5 Mfumo wa Menejimenti ya Wagombea ..... 50
4.6 Kampeni za Uchaguzi ..... 51
4.6.1 Ratiba za Kampeni ..... 51
4.6.1.1 Uratibu wa Kampeni za Nafasi ya Kiti cha Rais ..... 51
4.6.1.2 Uratibu wa Kampeni za Ubunge na Udiwani ..... 52
4.7 Mambo Yaliyozingatiwa Wakati wa Kampeni ..... 52
4.7.1 Sheria ya Gharama za Uchaguzi Na. 6 ya Mwaka 2010 ..... 52
4.7.2 Maadili ya Uchaguzi ..... 52
4.7.2.1 Kamati za Maadili ya Uchaguzi ..... 53
4.7.2.2 Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Kamati za Maadili ya Uchaguzi ..... 53
**SURA YA TANO ..... 55**
**KUPIGA NA KUHESABU KURA ..... 55**
5.1 Siku ya Uchaguzi ..... 55

5.1.1 Vituo vya Kupigia Kura ........................................................................ 55
5.1.3 Wapiga Kura kutambua Vituo vya Kupigia Kura ........................................... 56
5.1.4 Maamuzi ya Kisera kuhusu Upigaji Kura ..................................................... 56
5.1.5 Mawakala wa Upigaji Kura ........................................................................ 57
5.1.6 Usalama wa Vituo vya Kupigia Kura ........................................................... 57
5.1.7 Risala ya Mwenyekiti wa Tume kwa Wapiga Kura ......................................... 57

5.2 Utaratibu wa Upigaji Kura ........................................................................... 57

5.3 Kuahirisha Uchaguzi katika baadhi ya Majimbo na Kata ................................ 58

NB: *Kasoro mbalimbali inajumuisha upungufu wa Karatasi za Kupigia Kura, kukosewa kwa jina la mgombea katika Karatasi za Kupigia Kura, kuharibiwa kwa vifaa vya Kupigia Kura na kuchelewa kufika kwa Karatasi za Kupigia Kura.* ............ 60

5.4 Ratiba ya Uteuzi na Uchaguzi kwa Majimbo ambayo Uchaguzi Uliahirishwa ... 60

5.5 Kuhesabu Kura........................................................................................... 60

**SURA YA SITA ........................................................................................ 63**

**KUJUMLISHA KURA NA KUTANGAZA MATOKEO YA UCHAGUZI ................ 63**

6.1 Kujumlisha Kura ......................................................................................... 63
6.1.1 Utaratibu wa Kujumlisha Kura .................................................................... 63
6.1.2 Mfumo wa Menejimenti ya Matokeo ( *Results Management System* – RMS) .. 64

6.2 Kutangaza Matokeo ya Uchaguzi. ................................................................ 64
6.2.1 Matokeo ya Uchaguzi wa Rais ..................................................................... 65
6.2.2 Matokeo ya Uchaguzi wa Ubunge ................................................................ 68
6.2.3 Matokeo ya Udiwani. .................................................................................. 69

6.3 Uteuzi wa Wabunge na Madiwani Wanawake wa Viti Maalum ....................... 70
6.3.1 Uteuzi wa Wabunge Wanawake wa Viti Maalum ........................................... 70
6.3.1.1 Mgawanyo wa Viti Maalum vya Ubunge kwa Chama ................................ 71
6.3.2 Uteuzi wa Madiwani Wanawake Viti Maalum ............................................... 72
6.3.2.1 Mgawanyo wa Madiwani Wanawake Viti Maalum kwa Vyama ................... 72

6.4 Kesi za Kupinga Matokeo ya Ubunge na Udiwani ............................................ 73

**SURA YA SABA ........................................................................................ 74**

**USHIRIKISHWAJI WA WADAU WA UCHAGUZI ........................................ 74**

7.1 Ushirikishwaji wa Wadau ............................................................................. 74
7.1.1 Wadau Walioshirikishwa ............................................................................ 74

7.1.1.1 Serikali ........ 74
7.1.1.2 Vyama vya Siasa ........ 75
7.1.1.3 Asasi za Kiraia ........ 75
7.1.1.4 Vyombo vya Habari ........ 75
7.1.1.5 Taasisi na Viongozi wa Dini ........ 76
7.1.1.6 Makundi Maalum katika Jamii. ........ 76
7.1.1.7 Taasisi za Ulinzi na Usalama. ........ 76
7.1.1.8 Washirika wa Maendeleo. ........ 76
7.1.1.9 Watazamaji wa Uchaguzi ........ 77
**SURA YA NANE ........ 78**
**WATAZAMAJI WA UCHAGUZI ........ 78**
8.1 Utazamaji wa Uchaguzi ........ 78
8.1.1 Kamati ya Watazamaji na Mashirika ya Kimataifa ........ 78
8.1.2 Mialiko kwa Watazamaji wa Uchaguzi ........ 78
8.1.3 Usajili wa Watazamaji wa Uchaguzi ........ 78
8.1.4 Kuongeza Muda wa Utazamaji wa Uchaguzi ........ 79
8.1.5 Mikutano ya Tume na Watazamaji wa Uchaguzi ........ 80
8.2 Maoni na Ushauri wa Watazamaji wa Uchaguzi ........ 80
**SURA YA TISA ........ 81**
**TATHMINI BAADA YA UCHAGUZI MKUU ........ 81**
9.1 Tathmini ya Uchaguzi. ........ 81
9.2 Maeneo ya Tathmini ........ 81
9.3 Njia Zilizotumika Kufanya Tathmini ........ 82
9.4 Vigezo Vilivyotumika Kuchagua Maeneo ya Kufanyia Tathmini. ........ 85
9.5 Matokeo ya Awali ya Tathmini ........ 85
**SURA YA KUMI ........ 87**
**MAFANIKIO NA CHANGAMOTO ........ 87**
10.1 Mafanikio ........ 87
10.2 Changamoto ........ 87
10.2.1 Changamoto Wakati wa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ........ 88
10.2.2 Changamoto Wakati wa Uchaguzi Mkuu ........ 88
**SURA YA KUMI NA MOJA ........ 90**

**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........................................................ 90**

11.1 Hitimisho ........................................................................................ 90

11.2 Mapendekezo.................................................................................... 90

## ORODHA YA MAJEDWALI


Jedwali Na. 1: Wajumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi........................................7

Jedwali Na. 2: Fedha zilizoombwa na zilizopokelewa kwa ajili ya Uboreshaji ......... 11

Jedwali Na. 3: Ratiba ya Uchaguzi Mkuu 2015 ................................................... 14

Jedwali Na. 4: Orodha ya Majimbo yaliyotokana na Ongezeko la Halmashauri ...... 21

Jedwali Na. 5: Orodha ya Majimbo yaliyotokana na kigezo cha idadi ya Watu ........ 21

Jedwali Na. 6: Majimbo yaliyounganishwa kwa Upande wa Tanzania Zanzibar ....... 22

Jedwali Na. 7: Orodha ya Majimbo yaliyobadilishwa Majina kwa Tanzania Bara...... 22

Jedwali Na. 8: Ugawaji wa Vifaa kwa Kanda ....................................................... 23

Jedwali Na. 9: Idadi ya Watendaji wa Uchaguzi Vituoni ...................................... 26

Jedwali Na. 10: Ratiba ya Upokeaji wa BVR *Kits*................................................ 33

Jedwali Na. 11: Idadi ya walioandikishwa kwenye zoezi la majaribio ..................... 34

Jedwali Na. 12: Ratiba ya Uwekaji Wazi Daftari la Awali la Wapiga Kura ................ 37

Jedwali Na. 13: Idadi ya Wapiga Kura waliokadiriwa na walioandikishwa ............... 38

Jedwali Na. 14: Majina ya Wagombea wa Nafasi ya Kiti cha Rais na Makamu wa Rais ........................................................................................................... 43

Jedwali Na. 15: Wagombea Ubunge kwa Jinsi na kwa Chama .............................. 44

Jedwali Na. 16: Mchanganuo wa Rufaa za Ubunge.............................................. 46

Jedwali Na. 17: Wagombea kwa nafasi ya Udiwani kwa Jinsi na kwa Chama.......... 47

Jedwali Na. 18: Mchanganuo wa Rufaa za Wagombea Nafasi ya Udiwani .............. 49

Jedwali Na. 19: Wagombea Waliorejeshwa na Walioondolewa Baada ya Uamuzi wa Tume ......................................................................................... 50

Jedwali Na. 20: Muhtasari wa Idadi ya Wagombea, Pingamizi na Rufaa katika Uchaguzi wa Mwaka 2015 ......................................................................... 50

Jedwali Na. 21: Kamati za Maadili Zilizoundwa katika Ngazi mbalimbali ................. 53

Jedwali Na. 22: Orodha ya Majimbo ambayo Uchaguzi wa Wabunge Uliahirishwa .. 58

Jedwali Na. 23: Orodha ya Kata ambazo Uchaguzi Uliahirishwa............................ 59

Jedwali Na. 24: Ratiba ya Uteuzi na Uchaguzi katika Majimbo Yaliyoahirishwa ....... 60

Jedwali Na. 25: Matokeo ya kura alizopata kila Mgombea wa Kiti cha Rais............. 66

Jedwali Na. 26: Matokeo ya Ubunge kwa kila Chama cha Siasa............................. 68

Jedwali Na. 27: Matokeo ya Udiwani kwa kila Chama .......................................... 69

Jedwali Na. 28: Idadi ya Wabunge Wanawake wa Viti Maalum kwa Chama ........... 71

Jedwali Na. 29: Mgawanyo wa Madiwani Wanawake Viti Maalum kwa Chama........ 72

Jedwali Na. 30: Aina na Idadi ya Waliohojiwa kwa Jinsi ........................................ 82

Jedwali Na. 31: Mgawanyo wa Waliohojiwa kwa Umri .......................................... 82

## ORODHA YA VIAMBATISHO

Kiambatisho Na. 1: Orodha ya Vyama vya Siasa vyenye Usajili wa Kudumu ........... 92

Kiambatisho Na. 2: Orodha ya Majimbo ya Uchaguzi ........................................... 93

Kiambatisho Na. 3: Orodha ya Madiwani Waliopita bila Kupingwa ....................... 102

Kiambatisho Na. 4: Risala ya Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa Wapiga Kura ........................................................................................ 105

Kiambatisho Na. 5: Orodha ya Wabunge walioshinda katika Majimbo .................. 109

## ORODHA YA MICHORO

Mchoro Na. 1: Mzunguko wa Uchaguzi ........................................................................ 6
Mchoro Na. 2: Muundo wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ............................................... 9
Mchoro Na. 3: Biometric Voters Registration Kit ...................................................... 32

## ORODHA YA RAMANI

Ramani Na. 1: Ramani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ................................ 2
Ramani Na. 2: Idadi ya Majimbo ya Uchaguzi Kimkoa. ......................................... 18
Ramani Na. 3: Asilimia ya Wapiga Kura Walioandikishwa Kimkoa .......................... 39
Ramani Na. 4: Halmashauri zilizofanyiwa Tathmini Baada ya Uchaguzi .................. 81

## ORODHA YA CHATI


Chati Na. 1: Wagombea Ubunge kwa kila Chama kulingana na Viti vya Ubunge ..... 45

Chati Na. 2: Wagombea Ubunge kwa jinsi ........................................................ 45

Chati Na. 3: Wagombea Udiwani kwa kila Chama Kulingana na Viti vya Udiwani .... 48

Chati Na. 4: Wagombea Udiwani kwa Jinsi ........................................................ 48

Chati Na. 5: Matokeo ya Kiti cha Rais kwa kila Chama ......................................... 67

Chati Na. 6: Matokeo ya Ubunge kwa kila Chama................................................ 68

Chati Na. 7: Matokeo ya Madiwani kwa Chama .................................................. 69

Chati Na. 8: Wabunge Wanawake wa Viti Maalum kwa Chama ............................ 71

Chati Na. 9: Madiwani Wanawake wa Viti Maalum kwa Chama............................. 73

Chati Na. 10: Uelewa kuhusu Elimu ya Mpiga Kura.............................................. 85

Chati Na. 11: Wastani wa muda waliotumia Wapiga Kura kufika katika Kituo cha Kupigia Kura ............................................................................................ 86

**VIFUPISHO VYA MANENO**

| | |
|---|---|
| ACT-Wazalendo | Alliance for Change and Transparency- Wazalendo |
| ADA – TADEA | African Democratic Alliance - Tanzania Democratic Alliance |
| ADC | Alliance for Democratic Change |
| AFP | Alliance for Tanzanian Farmers Party |
| ANC | African National Congress |
| APPT – Maendeleo | African Progressive Party of Tanzania- Maendeleo |
| ARO | Assistant Returning Officer |
| ASP | Afro Shirazi Party |
| BVR | Biometric Voters Registration |
| CCK | Chama Cha Kijamii |
| CCM | Chama Cha Mapinduzi |
| CHADEMA | Chama cha Demokrasia na Maendeleo |
| CHAUMMA | Chama cha Ukombozi wa Umma |
| CHAUSTA | Chama cha Haki na Ustawi Tanzania |
| CMS | Candidates Management System |
| CSO | Civil Society Organizations |
| CUF | Civic United Front |
| DEP | Democratic Empowerment Project |
| DP | Democratic Party |
| GIS | Geographical Information System |
| GN | Government Notice |
| GPS | Global Positioning System |
| IGP | Inspector General of Police |
| JNICC | Julius Nyerere International Convention Centre |
| JWTZ | Jeshi la Wananchi wa Tanzania |
| Mst. | Mstaafu |
| NLD | National League for Democracy |
| NRA | National Reconstruction Alliance |
| OMR | Optical Mark Recognition |
| OMS | Observers Management System |

| | |
|---|---|
| REC | Regional Election Coordinator |
| RMS | Results Management System |
| RO | Returning Officer |
| SADC | Southern African Development Community |
| SMS | Short Message Service |
| TANU | Tanganyika African National Union |
| TBC | Tanzania Broadcasting Corporation |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TCDA | Tanganyika Centre for Development and Advocacy |
| TLP | Tanzania Labour Party |
| TLS | Tanganyika Law Society |
| TOT | Training of Trainers |
| TPA | Tanzania Ports Authority |
| TV | Television |
| UDP | United Democratic Party |
| UNDP | United Nations Development Programme |
| UPDP | United People's Democratic Party |
| UTP | United Tanganyika Party |
| ZEC | Zanzibar Electoral Commission |
| ZNP | Zanzibar Nationalist Party |
| Znz | Zanzibar |
| ZPPP | Zanzibar and Pemba People's Party |

## SHUKRANI

Tume ya Taifa ya Uchaguzi licha ya kuwa ni chombo huru kwa mujibu wa Katiba, utendaji kazi wake huilazimu kwa namna moja au nyingine kushirikiana na Serikali na wadau mbalimbali wa Uchaguzi. Uchaguzi wa mwaka 2015, ulikuwa na ushindani mkubwa zaidi wa kisiasa kuliko chaguzi nyingine zote zilizowahi kusimamiwa na Tume tangu kurejeshwa kwa Mfumo wa Vyama vingi vya Siasa nchini mwaka 1992.

Tume kwa kutambua hilo, inatoa shukrani za dhati kwa viongozi wote wa ngazi za juu waliokuwa madarakani wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. Viongozi hao ni Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal, Makamu wa Rais Mstaafu, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Shukrani za pekee, ziende kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kuwezesha kupatikana kwa rasilimali watu na fedha katika kufanikisha zoezi la Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

Mafanikio makubwa ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, yalitokana na umakini na umahiri wa Watendaji wote wa Uchaguzi na wadau mbalimbali kuanzia ngazi ya Taifa hadi Kituo cha Kupigia Kura. Miongoni mwa wadau hao, ni pamoja na Vyama vya Siasa na Wagombea, Asasi za Kiraia, Washirika wa Maendeleo, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC), Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Jeshi la Polisi na Vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama. Tume inapenda kuwashukuru kwa dhati kwa ushirikiano wao ulioiwezesha Tume kutimiza majukumu yake.

Aidha, Tume inatoa shukrani kwa Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Vyombo vya Habari na Watazamaji wa Uchaguzi kwa ushirikiano waliouonesha.

Mwisho, shukrani za dhati ziwafikie Wapiga Kura na Watanzania wote kwa ujumla wao kwa **amani, utulivu** na **uvumilivu** walioonesha wakati wote wa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, Kampeni na Siku ya Uchaguzi hadi kutangazwa kwa Matokeo.

## BARUA YA UWASILISHAJI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**

*Anwani ya Simu "UCHAGUZI".*
Nambari ya Simu: +255 22 2114963-6,
*Nambari ya Faksi +255 22 2116740*
*Barua Pepe: uchaguzi@nec.go.tz*
Tovuti: www.nec.go.tz
***(Barua zote za kiofisi ziandikwe kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi)***

POSTA HOUSE,
7 MTAA WA GHANA/OHIO,
S. L. P. 10923,
**11300 DAR ES SALAAM.**

**Unapojibu tafadhali taja:**

Kumb. Na. **CEA.74/75/01/158** **23 Juni, 2016**

Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli,

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

Ikulu,

1 Barabara ya Barack Obama,

S. L. P. 9120,

**11400 DAR ES SALAAM.**

Mheshimiwa Rais,

Tume ya Taifa ya Uchaguzi ni chombo huru kilichoanzishwa chini ya Ibara ya 74 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977. Wajumbe wote saba wa Tume iliyosimamia Uchaguzi wa Rais, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wa Madiwani Tanzania Bara mwaka 2015, waliteuliwa na Mheshimiwa Rais kwa nyakati tofauti.

Wajumbe hao ni Waheshimiwa Jaji (Mst.) Damian Z. Lubuva (Mwenyekiti), Jaji Mkuu (Mst-Z) Hamid M. Hamid (Makamu Mwenyekiti), Prof. Amon E. Chaligha (Mjumbe), Mchanga H. Mjaka (Mjumbe), Jaji (Mst.) John J. Mkwawa (Mjumbe), Jaji (Mst.) Mary H. C. S. Longway (Mjumbe) na Asina A. Omari (Mjumbe). Kila Mjumbe wa Tume huteuliwa kwa kipindi cha miaka mitano.

Aidha, katika Utekelezaji wa majukumu yake, Tume husaidiwa na Sekretarieti ya Tume inayoongozwa na Mkurugenzi wa Uchaguzi. Kwa sasa Mkurugenzi wa Uchaguzi ni Ndugu Kailima Ramadhani Kombwey ambaye ndiye Katibu wa Tume. Mkurugenzi wa Uchaguzi huteuliwa kwa mujibu wa Ibara ya 74 (7) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977. Sekretarieti ya Tume huratibu na kusimamia shughuli zote za utendaji wa Tume za kila siku.

Chini ya Ibara za 74 (6) na 78 (1) ya Katiba, na Kifungu cha 4C Sheria ya Taifa ya Uchaguzi Sura ya 343 Majukumu ya Tume ni:-

Kusimamia na kuratibu Uandikishaji wa Wapiga Kura katika Uchaguzi wa Rais na Wabunge, katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Madiwani kwa Tanzania Bara;

Kusimamia na kuratibu uendeshaji wa Uchaguzi wa Rais na Wabunge katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Madiwani katika Tanzania Bara;

Kuchunguza Mipaka na Kuigawa Jamhuri ya Muungano katika Majimbo mbalimbali kwa ajili ya Uchaguzi wa Wabunge;

Kutekeleza majukumu mengine yoyote kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge.

Kuwatangaza wanawake waliotimiza masharti kwamba wamechaguliwa kuwa Wabunge au Madiwani wa Viti Maalum vya Wanawake;

Kutoa Elimu ya Mpiga Kura nchini kote; kuratibu na kusimamia Watu/Taasisi zote zinazoendesha Elimu hiyo; na

Mheshimiwa Rais, Tume imekuwa ikitekeleza majukumu yake wakati wote kwa kuzingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura 343.

Aidha, Tume huzingatia Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287, Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288, Sheria ya Gharama za Uchaguzi Na. 6 ya mwaka 2010, Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge, na wa Madiwani, Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ambazo hutungwa kila mwaka wa Uchaguzi.

Kabla ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2015, Tume ilifanikiwa kufanya Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa kutumia Teknolojia mpya ya "Biometric Voters Registration" (BVR). Katika uboreshaji huo Tume kwa kutumia BVR Kits 8,000 iliandikisha Wapiga Kura 23,161,440 sawa na asilimia 96.9 ya lengo lililokusudiwa la kuandikisha Wapiga Kura 23,901,471.

Mheshimiwa Rais, baada ya kuandikisha Wapiga Kura kwa kutumia BVR Kits kwa mafanikio, Tume imeanzisha utaratibu na imefanikiwa kuwa na Kanzidata itakayotumika katika kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura wa Chaguzi zijazo.

Kwa utaratibu huu wananchi wataweza kufanya marekebisho ya taarifa zao, kuwaondoa waliopoteza sifa, waliosajiliwa zaidi ya mara moja na kuwa na Daftari la Kudumu la Wapiga Kura la uhakika na la kuaminika.

Mheshimiwa Rais, Kwa ujumla, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inaamini kwamba Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 uliendeshwa na Tume kwa mafanikio makubwa ambayo pia yalichangiwa na Ushirikiano mkubwa wa Wadau mbalimbali katika mchakato mzima wa Uchaguzi. Kwa wadau wote, Tume inatoa shukrani zake za dhati.

Mheshimiwa Rais, kwa heshima na taadhima, Tume inaomba kuwasilisha kwako Taarifa ya Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani uliofanyika mwaka 2015.

Asante,

..........................................
Jaji (Mst.) Damian Z. Lubuva
Mwenyekiti

..........................................
Jaji Mkuu (Mst. Z) Hamid M. Hamid
Makamu Mwenyekiti

..........................................
Prof. Amon E. Chaligha
Mjumbe

..........................................
Mchanga H. Mjaka
Mjumbe

..........................................
Jaji (Mst.) John J. Mkwawa
Mjumbe

..........................................
Jaji (Mst.) Mary H. C. S. Longway
Mjumbe

..........................................
Asina A. Omari
Mjumbe

..........................................
Kailima Ramadhani Kombwey
Mkurugenzi wa Uchaguzi
na Katibu wa Tume

## DIBAJI

Tume ya Taifa ya Uchaguzi iliendesha na kusimamia Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. Kwa kuzingatia mzunguko wa Uchaguzi, kazi inayofuatia ni kuandaa Taarifa ya Uchaguzi na kuiwasilisha kwa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Taarifa hii ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, inaelezea kwa undani mchakato wa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na namna Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ulivyoendeshwa. Aidha, Taarifa hii inaelezea mafanikio na changamoto zilizojitokeza na mwisho inatoa mapendekezo ili kuboresha chaguzi zijazo.

Taarifa hii ina Sura 11 kama ifuatavyo:-

1. Utangulizi.
2. Maandalizi ya Uchaguzi.
3. Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.
4. Uteuzi wa Wagombea na Kampeni za Uchaguzi.
5. Upigaji Kura na Uhesabuji wa Kura Vituoni.
6. Kujumlisha Kura na Kutangaza Matokeo ya Uchaguzi.
7. Ushirikishwaji wa Wadau wa Uchaguzi.
8. Watazamaji wa Uchaguzi.
9. Tathmini Baada ya Uchaguzi Mkuu.
10. Mafanikio na Changamoto.
11. Hitimisho na Mapendekezo.

Ni matumaini yetu kwamba, Taarifa hii itakidhi matarajio ya wasomaji mbalimbali wa ndani na nje ya nchi. Aidha, Tume inaamini kwamba Wadau wa Uchaguzi, Watafiti na wasomaji wengine watanufaika na Taarifa hii.

## MUHTASARI WA TAARIFA

Taarifa hii inahusu Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Madiwani Tanzania Bara, ambao uliofanyika tarehe 25 Oktoba 2015, na imegawanyika katika Sura 11.

**Sura ya Kwanza,** inaelezea chimbuko la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na muundo wa kiutawala. Aidha, sehemu hii, inafafanua juu ya Mfumo wa Siasa na Mfumo wa Uchaguzi wa nchi, Mzunguko wa Uchaguzi, Mamlaka na Madaraka ya Tume. Pamoja na hayo, inaelezea muundo na majukumu ya Tume ambayo ndiyo msingi wa utekelezaji wa shughuli za uendeshaji Uchaguzi.

**Sura ya Pili,** inahusu Maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. Maandalizi hayo, ni pamoja na gharama zilizotumika katika Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ambazo zilifikia Shilingi **260,865,285,227/=** na gharama za Uchaguzi Mkuu Shilingi **273,634,130,372/=.** Kwa gharama hizi Serikali ilitoa asilimia **99.72** ya gharama za Uchaguzi. Vilevile, Washirika wa Maendeleo (UNDP) walichangia kiasi cha Shilingi **1,523,886,833** ambayo ni sawa na asilimia **0.28** ya gharama zote za Uchaguzi.

Sura hii, inaelezea kuhusu uandaaji wa Ratiba ya Uchaguzi Mkuu, Sheria, Kanuni na Maadili ya Uchaguzi. Pia, inazungumzia uanzishwaji wa Majimbo Mapya **25** ya Uchaguzi uliofanywa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi na hivyo kufanya idadi ya Majimbo ya Uchaguzi kuwa **264** Nchi nzima kutoka Majimbo **239** ya awali.

Aidha, Sura hii inaelezea kuhusu Watendaji wa Tume walioshiriki katika zoezi la Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, pamoja na namna Elimu ya Mpiga Kura ilivyotolewa.

**Sura ya Tatu,** inaeleza namna zoezi la Uandikishaji na Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura lilivyofanyika Nchi nzima. Aidha, Sura hii inafafanua namna teknolojia ya *Biometric Voter Registration* ilivyotumika wakati wa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na Changamoto zilizojitokeza.

**Sura ya Nne,** inazungumzia Uteuzi wa Wagombea na Kampeni za Uchaguzi. Tarehe 21 Agosti, 2015 ilikuwa ndiyo Siku ya Uteuzi wa Wagombea wa nafasi mbalimbali katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. Katika nafasi ya kiti cha Rais, Jumla ya Wagombea **11** walijitokeza. Kati ya hao, Wagombea **8** ndiyo walioteuliwa kuwania nafasi hiyo. Kwa nafasi ya Ubunge jumla ya Wagombea **1,237** waliteuliwa. Aidha, kwa nafasi ya Udiwani jumla ya Wagombea **10,152** waliteuliwa.

Sura hii pia, inaelezea tarehe ya kuanza kwa Kampeni za Uchaguzi na namna zilivyofanyika katika hali ya amani na utulivu. Kampeni hizo zilianza tarehe 22 Agosti, 2015 na kumalizika tarehe 24 Oktoba, 2015. Vile vile, Sura hii pia inazungumzia Sheria ya Gharama za Uchaguzi Na. 6 ya mwaka 2010.

**Sura ya Tano,** inaelezea juu ya zoezi la Kupiga na Kuhesabu Kura, ambapo Tume ilitangaza siku ya Kupiga Kura kuwa ni tarehe 25 Oktoba, 2015. Pamoja na kuzingatiwa kwa Sheria za Uchaguzi, Tume ilifanya maamuzi ya Kisera pale ambapo ilionekana kuna umuhimu wa kufanya hivyo ili kuleta ufanisi katika kutekeleza zoezi la Upigaji Kura. Miongoni mwa maamuzi hayo ya kisera yalihusu Wapiga Kura ambao Namba za Kadi zao zilikuwa zinatofautiana na namba zilizomo kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, Wapiga Kura ambao waliandikishwa na Tume na kisha kuhamishiwa kwenye maeneo mapya ya Kiutawala na Wapiga Kura ambao walikuwa na Kadi za Kupigia Kura lakini majina yao hayakuonekana kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

**Sura ya Sita,** inazungumzia kuhusu Kujumlisha na Kutangaza Matokeo ya Uchaguzi wa Rais na Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Madiwani wa Tanzania Bara. Kadhalika, Sura hii inaelezea matumizi ya Mfumo wa Menejimenti ya Matokeo uliotumika katika kuchakata na kujumlisha matokeo. Aidha, imefafanua kuhusu utaratibu wa kuwapata Wabunge na Madiwani Wanawake wa Viti Maalum.

**Sura ya Saba,** inahusu Ushirikishwaji wa Wadau katika maeneo mbalimbali ya Uchaguzi ambayo ni pamoja na Elimu ya Mpiga Kura, masuala ya ulinzi na Usalama wakati wote wa Uchaguzi na kamati mbalimbali zilizokuwa zinaratibu shughuli za Uchaguzi Mkuu.

**Sura ya Nane,** inaelezea juu ya Watazamaji wa Uchaguzi wa ndani na wa nje ya nchi, pia inatoa mwongozo kuhusu utaratibu na usajili wao. Tume ilitoa mialiko na kutoa vibali kwa Taasisi mbalimbali za ndani na nje ya nchi ambapo jumla ya Taasisi **124** za ndani na **34** za nje zilipatiwa kibali cha kutazama Uchaguzi. Aidha, Sura hii inaelezea maoni na mapendekezo ya baadhi ya Watazamaji wa Uchaguzi.

**Sura ya Tisa,** inazungumzia Tathmini Baada ya Uchaguzi Mkuu. Mara baada ya kukamilika kwa zoezi la Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, Tume kwa mara ya kwanza, ilifanya tathmini katika mikoa **22** kwa lengo la kutathmini zoezi zima la Uchaguzi Mkuu ulivyoendeshwa. Sura hii, imefafanua kuhusu lengo la kufanya tathmini, vigezo pamoja na matokeo ya tathmini.

**Sura ya Kumi,** inaainisha Mafanikio na Changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa zoezi la Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

**Sura ya Kumi na Moja,** inatoa Hitimisho na Mapendekezo ambayo yakizingatiwa yataboresha Chaguzi zijazo.

## SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI

### 1.1 Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Nchi inayojumuisha iliyokuwa Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar zilizoungana tarehe 26 Aprili, 1964. Tanganyika ilipata uhuru tarehe 9 Desemba, 1961 kutoka kwa Waingereza. Aidha, Zanzibar ilipata uhuru tarehe 10 Desemba, 1963 kutoka kwa Waingereza, na baadae ilijikomboa kutoka Utawala wa Kisultani kwa Mapinduzi ya tarehe 12 Januari, 1964.

Tanzania ipo katika Latitudi $0^0$ na $12^0$ Kusini mwa Ikweta; na Longitudi $25^0$ hadi $45^0$ Mashariki mwa Greenwich. Kaskazini Tanzania inapakana na Kenya na Uganda; Magharibi ni Rwanda, Burundi, Kongo (Kinshasa) na Zambia; Kusini ni Msumbiji na Malawi; upande wa Mashariki ni Bahari ya Hindi.

Tanzania ina eneo la ukubwa wa kilometa za mraba **945,203** ikiwemo sehemu ya Maziwa Makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa; pamoja na Mlima Kilimanjaro ambao ni mrefu kuliko yote Afrika. Nchi hii ina vivutio vingi vya kitalii vikiwemo mbuga za wanyama, hifadhi za taifa, fukwe za bahari, milima na Bonde la Ufa. Tanzania pia, ina rasilimali nyingi ambazo ni pamoja na ardhi, madini, gesi asilia, misitu, mazao ya kilimo, mifugo na samaki. Rasilimali hizi ndizo nguzo kuu za Uchumi wa Taifa.

Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012, Tanzania ilikuwa na watu wapatao Milioni **44.9**. Tanzania Zanzibar ilikuwa na jumla ya watu milioni **1.3** wakati Tanzania Bara ilikuwa na idadi ya watu milioni **43.6.** Kwa mujibu wa Taarifa kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu makadirio ya Idadi ya Watu kwa mwaka 2015 ni Milioni **48.7**, ambapo Tanzania Bara inakadiriwa kuwa na watu **47.3** Milioni na Tanzania Zanzibar inakadiriwa kuwa na watu Milioni **1.4.** Taifa hili linaundwa na watu wenye makabila zaidi ya **120**, wengi wao wakiwa ni makabila yenye asili ya Kibantu na yale yasiyo ya Kibantu kama vile: Wasandawe, Wamasai, Wachaga, Wahadzabe na Wabarbaig kwa upande wa Tanzania Bara na Watumbatu, Wamakunduchi na Wapemba kwa upande wa Tanzania Zanzibar. Pamoja na wingi wa makabila, kiungo kikuu cha Utaifa ni Lugha ya Kiswahili inayozungumzwa na Watanzania wote.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kiutawala, imegawanyika katika Mikoa **30** ambapo Tanzania Bara ina Mikoa **25**, Wilaya **133**, Halmashauri **181**, Kata **3,953**, Mitaa **4,037** na Vijiji **12,545**. Tanzania Zanzibar nayo ina Mikoa **5**, Wilaya **11** na Shehia **361**. Mihimili mikuu ya Dola ni Serikali, Bunge na Mahakama.

**Ramani Na. 1: Ramani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**



## 1.2 Mfumo wa Siasa Tanzania

Tanzania ni Nchi ya Kidemokrasia yenye kufuata Mfumo wa Vyama vingi vya Siasa. Kabla ya kupata Uhuru Mwaka 1961, Tanganyika (Tanzania Bara) ilikuwa na Mfumo wa Vyama vingi vya Siasa ambapo Vyama vitatu vya Tanganyika African National Union (TANU), United Tanganyika Party (UTP) na African National Congress (ANC) vilishiriki kwenye Chaguzi zilizofanyika wakati huo. Aidha, kwa Tanzania Zanzibar Vyama vinne vya Afro Shirazi Party (ASP), Zanzibar and Pemba People's Party (ZPPP), UMMA Party na Zanzibar Nationalist Party (ZNP) vilishiriki kwenye Chaguzi kabla ya mwaka 1964. Baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar 1964, mwaka uliofuata (1965) Mfumo wa Vyama vingi vya Siasa ulifutwa rasmi. Tanzania iliamua kufuata Mfumo wa Chama kimoja ambapo kwa upande wa Tanzania Bara ilibaki na Chama cha TANU na Tanzania Zanzibar ilibaki na Chama cha ASP. Kiuhalisia Vilibakia Vyama Viwili vya Siasa, TANU kwa Tanzania Bara na ASP kwa Tanzania Zanzibar.

Mwaka 1977, Vyama vya TANU na ASP viliungana na kuunda Chama kimoja cha Siasa ambacho ni Chama cha Mapinduzi (CCM).

Mwaka 1992, mfumo wa Vyama vingi vya Siasa ulirejeshwa nchini. Tangu kurejeshwa kwa Mfumo huo, zimefanyika jumla ya Chaguzi Kuu tano. Chaguzi hizo zilifanyika mwaka 1995, 2000, 2005, 2010 na 2015, ambapo Vyama mbalimbali vya Siasa vilishiriki.

Vyama vya Siasa husajiliwa kwa kufuata utaratibu ulioainishwa na Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258, ambapo Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ndiyo yenye jukumu la kusajili na kusimamia mwenendo wa Vyama hivyo. Hadi wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, Vyama vya Siasa **22** vilikuwa vimepata Usajili wa kudumu. Orodha ya Vyama vyenye Usajili wa Kudumu imeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 1.**

## 1.3 Mfumo wa Uchaguzi Tanzania

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, katika Ibara ya 21 inatoa haki kwa kila mwananchi kushiriki katika shughuli za utawala za nchi kwa kuchagua au kuchaguliwa. Kila Mtanzania aliyetimiza umri wa miaka 18 ana haki ya Kupiga Kura kuchagua kiongozi anayempenda. Hata hivyo, ili mtu aweze kuwa na sifa za kuchaguliwa ni lazima awe ametimiza umri usiopungua miaka 21 kwa nafasi ya Udiwani na Ubunge na miaka 40 kwa nafasi ya Urais.

Tanzania inatumia Mfumo wa Uchaguzi ambao mgombea anayepata Kura nyingi halali kuliko mgombea mwingine yeyote ndiye hutangazwa kuwa mshindi *(First – Past – the Post).* Hii, ni kwa mujibu wa Vifungu vya 35 F(8) na 80(1) vya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343.

Mfumo mwingine unaotumika ni ule wa Uwiano wa Kura *(Proportional Representation)* ambao hutumika kupata Wabunge na Madiwani Wanawake wa Viti Maalum. Ibara ya 66 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, inaelezea aina 6 za Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pamoja na Wabunge wa kuchaguliwa na Wabunge wa Viti maalum wapo pia Wabunge 5 waliochaguliwa na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar kutoka miongoni mwao, Mwanasheria Mkuu, Spika (iwapo hatakuwa amechaguliwa kutoka miongoni mwa Wabunge) na Wabunge wasiozidi kumi walioteuliwa na Rais.

Madiwani Wanawake wa Viti Maalum wanapatikana kwa uwiano wa Viti vya Udiwani ambavyo kila Chama kimeshinda katika Halmashauri husika. Hii, ni kwa mujibu wa Kifungu cha 35 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287 na Kifungu cha 19 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288.

### 1.4 Mzunguko wa Uchaguzi Tanzania

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ibara ya 65 inaelekeza kuwa Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani ufanyike kila baada ya kipindi cha miaka mitano (5).

Kama ilivyo kwa Nchi nyingine Duniani, katika kuendesha shughuli za Uchaguzi, Tanzania hutumia utaratibu wa mzunguko wa Uchaguzi ambao shughuli zake hugawanywa katika awamu tatu (3). Awamu hizo ni shughuli kabla, wakati na baada ya Uchaguzi.

Hivyo, Tume ya Taifa ya Uchaguzi imetekeleza mfumo wa mzunguko wa Uchaguzi kwa kufuata awamu hizo Tatu kama ifuatavyo:

#### (a) Kabla ya Uchaguzi

Shughuli zilizofanyika katika awamu kabla ya Uchaguzi ni pamoja na:

(i) Uandaaji wa Bajeti;

(ii) Uandikishaji wa Wapiga Kura;

(iii) Ununuzi wa Vifaa;

(iv) Uandaaji wa Kalenda na Mpango wa Utekelezaji;

(v) Marekebisho ya Sheria na Maelekezo ya Watendaji na Wadau wa Uchaguzi;

(vi) Mafunzo kwa Watendaji wa Uchaguzi;

(vii) Kutoa Elimu ya Mpiga Kura; na

#### (b) Wakati wa Uchaguzi

Katika awamu hii, Tume ilifanya shughuli zifuatazo:

(i) Uteuzi wa Wagombea;

(ii) Uratibu wa Kampeni za Wagombea;

(iii) Utekelezaji wa Kamati za Maadili;

(iv) Usajili wa Watazamaji wa Uchaguzi.

(v) Kuchapa na kusambaza Karatasi za Kura;

(vi) Kusambaza Vifaa vya Uchaguzi;Upigaji Kura;

(vii) Kuhesabu Kura; na

(viii) Kutangaza Matokeo.

**(c) Baada ya Uchaguzi**

Katika awamu hii, Tume inafanya shughuli zifuatazo:

(i) Tathmini baada ya Uchaguzi Mkuu;

(ii) Kushughulikia Kesi za Uchaguzi; na

(iii) Kuandaa Taarifa ya Uchaguzi Mkuu.

(iv) Marekebisho ya Sheria za Uchaguzi;

(v) Kupitia na kuboresha Daftari la Wapiga Kura;

(vi) Kupitia na kuboresha Mifumo ya Uchaguzi;

(vii) Kupitia na kuboresha mipaka ya Majimbo ya Uchaguzi;

(viii) Kupitia na kuboresha Muundo wa Tume;

(ix) Ukaguzi wa matumizi ya fedha na vifaa vilivyotumika katika Uchaguzi Mkuu;

(x) Kupitia Mpango Mkakati; na

(xi) Kuandaa Mpango Kazi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu unaofuata.

**Mchoro Na. 1: Mzunguko wa Uchaguzi**




## 1.5 Tume ya Taifa ya Uchaguzi

Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilianzishwa tarehe 13 Januari, 1993, kufuatia kurejeshwa Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa mnamo mwaka 1992. Kwa mujibu wa Ibara ya 74(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Tume inaongozwa na Mwenyekiti na inakuwa na Wajumbe wanaoteuliwa na Rais. Hayati Jaji (Mst) Lewis M. Makame alikuwa Mwenyekiti wa kwanza wa Tume kuanzia tarehe 13 Januari, 1993 hadi 14 Juni, 2011, akifuatiwa na Mhe. Jaji (Mst) Damian Z. Lubuva ambaye alianza muda wake tarehe 19 Desemba, 2011 hadi sasa. Tume ndiyo yenye mamlaka ya kusimamia na Kuratibu Uendeshaji wa Uchaguzi wa Rais na Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Madiwani kwa Tanzania Bara.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi ni Idara huru inayojitegemea. Hii ni kwa mujibu wa Ibara ya 74(7) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Ibara ya 74(11) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaelekeza kuwa Tume

katika kutekeleza majukumu yake ya Kikatiba haitalazimika kupokea maelekezo au amri kutoka kwa mtu yeyote au Idara yoyote ya Serikali au kufuata maoni ya Chama chochote cha Siasa.

Kwa Mujibu wa Ibara ya 74 (12) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Mahakama yoyote hairuhusiwi kuchunguza jambo lolote lililotendwa na Tume katika utekelezaji wa Majukumu yake.

### 1.5.1 Muundo wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi

Tume inaundwa na Wajumbe saba (7), miongoni mwao wakiwemo Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti ambao wanapaswa kuwa na sifa ya Jaji wa Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufani. Katika Uteuzi, Rais anazingatia kuwa endapo Mwenyekiti ni mtu anayetoka sehemu moja ya Muungano, Makamu wake atakuwa ni mtu anayetoka sehemu ya pili ya Muungano. Hii, ni kwa mujibu wa Ibara ya 74(1) na (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, na Kifungu cha 4(1) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343.

Aidha, Mjumbe mmoja anateuliwa kutoka miongoni mwa Wanachama wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (*Tanganyika Law Society* - TLS) na Wajumbe wengine wanne (4) wanatakiwa wawe na uelewa wa kutosha kuhusiana na kusimamia na kuendesha Uchaguzi wa Wabunge au sifa nyingine kama ambavyo Rais wa Jamhuri ya Muungano atakavyoona inafaa kwa ajili ya kuendesha shughuli za Tume.

Kwa sasa, Tume ina jumla ya Wajumbe saba (7) kama inavyoonesha kwenye **Jedwali Na. 1.**

**Jedwali Na. 1: Wajumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi**

| Na. | Jina | Wadhifa |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Jaji (Mst.) Damian Z. Lubuva | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Jaji Mkuu (Mst. Z) Hamid M. Hamid | Makamu Mweyekiti |
| 3. | Mhe. Prof. Amon E. Chaligha | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Mchanga H. Mjaka | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Jaji (Mst.) John J. Mkwawa | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Jaji (Mst.) Mary H.C.S Longway | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Asina A. Omari | Mjumbe |

Wajumbe wa Tume hukaa Madarakani kwa kipindi cha miaka mitano tangu kuteuliwa kwao, lakini Rais anaweza kuwateua tena kwa kipindi kingine kadri atakavyoona inafaa.

Katika utekelezaji wa majukumu yake, Tume husaidiwa na Sekretarieti inayoongozwa na Mkurugenzi wa Uchaguzi ambaye ndiye Mtendaji Mkuu na Katibu wa Tume. Kwa sasa Mkurugenzi wa Uchaguzi ni Bwana Kailima R. Kombwey.

Aidha, Tume ina Idara 5 na Vitengo 4 vinayoongozwa na Naibu Katibu na Wakurugenzi kama ifuatavyo:-

(i) Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu;
(ii) Idara ya Mipango;
(iii) Idara ya Daftari la Kudumu la Wapiga Kura;
(iv) Idara ya Uendeshaji Uchaguzi;
(v) Idara ya Habari na Elimu ya Mpiga Kura;
(vi) Kitengo cha Fedha na Uhasibu;
(vii) Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani;
(viii) Kitengo cha Huduma za Sheria; na
(ix) Kitengo cha Ununuzi, Ugavi na Lojistiki. (Rejea Muundo wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika **Mchoro Na. 2)**

**Mchoro Na. 2: Muundo wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi**



### 1.5.2 Dira na Dhima ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi

Katika kutekeleza majukumu yake, Tume inaongozwa na Dira na Dhima ili kufanikisha malengo na matarajio yake.

#### 1.5.2.1 Dira

Kuwa chombo Huru chenye uwezo wa Kuimarisha Demokrasia ya kweli katika Nchi kwa kuendesha Chaguzi zilizo Huru, Haki na Zinazoaminika.

#### 1.5.2.2 Dhima

Kuratibu, kuendesha na kusimamia Uchaguzi wa Rais na Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Madiwani wa Tanzania Bara, na pia kufanya shughuli nyingine za uchaguzi kwa kushirikiana na Wadau wa Uchaguzi ili kukuza Demokrasia, utawala bora na maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii.

### 1.5.3 Majukumu ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi

Majukumu ya Tume yameainishwa katika Ibara ya 74 (6) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Majukumu hayo ni:

(i) Kusimamia na Kuratibu Uandikishaji wa Wapiga Kura katika Uchaguzi wa Rais na Wabunge katika Jamhuri ya Muungano;

(ii) Kusimamia na Kuratibu Uendeshaji wa Uchaguzi wa Rais na Wabunge;

(iii) Kuchunguza Mipaka na Kuigawa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya Uchaguzi wa Wabunge;

(iv) Kusimamia na Kuratibu Uandikishaji wa Wapiga Kura na Uendeshaji wa Uchaguzi wa Madiwani; na

(v) Kutekeleza majukumu mengine yoyote kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge.

Majukumu mengine ya Tume kwa mujibu wa Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura 343, na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, ni pamoja na yafuatayo:-

(vi) Kutoa Elimu ya Mpiga Kura kwa nchi nzima, Kuratibu, Kusimamia Taasisi na watu wanaotoa Elimu hiyo; na

(vii) Kuteua na kuwatangaza Wabunge na Madiwani Wanawake wa Viti Maalum.

## SURA YA PILI

## MAANDALIZI YA UCHAGUZI

### 2.1 Gharama za Uboreshaji wa Daftari la Wapiga Kura na Uchaguzi Mkuu

Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilitumia jumla ya Shilingi **534,499,415,599/=** kwa ajili ya shughuli za Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na Uendeshaji wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015. Aidha, Tume ilitumia kiasi cha Shilingi **1,523,886,833/=** kutoka kwa washirika wa Maendeleo kupitia Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa kwa Shughuli za Uchaguzi. Mchanganuo wa fedha kutoka Serikalini umeoneshwa katika **Jedwali Na. 2.**

**Jedwali Na. 2: Fedha zilizoombwa na kupokelewa kutoka Serikalini**

| Na. | Matumizi | Fedha Zilizoombwa (Sh.) | Fedha Zilizopokelewa (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1. | Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura | 330,290,786,381.40 | 260,865,285,227.00 |
| 2. | Uchaguzi Mkuu | 273,648,993,370.00 | 273,634,130,372.00 |
| **JUMLA** | | **603,939,779,751.40** | **534,499,415,599.00** |

### 2.1.1 Gharama za Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura

Tume ilipokea jumla ya Shilingi **260,865,285,227/=** kwa ajili ya Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kati ya shilingi **330,290,786,381.40** zilizoombwa. Fedha hizo zilitumika kwa ajili ya Ununuzi wa "BVR *Kits*", Mafunzo kwa Watendaji na kuendesha zoezi la Uandikishaji.

#### 2.1.1.1 Ununuzi wa Vifaa vya Uboreshaji wa Daftari la Wapiga Kura

Ununuzi wa Vifaa kwa ajili ya Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ulifanywa na Tume kwa kufuata Sheria ya Manunuzi ya Umma Na. 7 ya Mwaka 2011 na Kanuni zake za Mwaka 2013. Vifaa vingine vilinunuliwa na Washirika wa Maendeleo kupitia Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (United Nations Development Programme -UNDP).

Vifaa vilivyonunuliwa kwa ajili ya Uboreshaji wa Daftari la Wapiga Kura ni pamoja na "BVR *Kits*" 8,000, Machapisho na Fomu mbalimbali zilizotumika kwenye Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, Shajara, Vifungashio (Packing boxes), Fulana, Kofia na Mabegi, *Printers, GIS Hardware, GPS Handsets, Servers* na wino wa *Printer* aina mbalimbali.

Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) kwa kutumia Mradi wake wa *Democratic Empowement Project* (DEP) liligharamia na kuipatia Tume Vifaa mbalimbali kwa ajili ya Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ikiwemo Kuboresha Mifumo mbalimbali ya Kompyuta kama vile Mfumo wa Utunzaji Kumbukumbu na Usambazaji wa Vifaa *(Warehouse Management Systems*) na Machapisho ya vipeperushi kwa ajili ya utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura.

### 2.1.2 Gharama za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015.

Katika zoezi la Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilikadiria kutumia kiasi cha Shilingi **273,648,993,370/=** fedha ambazo zilijumuisha, Mafunzo kwa Watendaji, Lojistiki, Malipo kwa Watendaji wa Uchaguzi, Maandalizi ya Vituo vya Kupigia Kura, Elimu ya Mpiga Kura, Ununuzi na Uchapishaji wa Vifaa vya Uchaguzi Mkuu, Tathmini baada ya Uchaguzi Mkuu na Uandaaji na Uchapishaji wa Taarifa ya mwisho ya Uchaguzi Mkuu. Pia, Tume ilitumia fedha hizo katika kuandaa Kituo cha Taifa cha kupokea na kutangaza Matokeo ya Uchaguzi na kugharamia uendeshaji wa Kesi za Uchaguzi.

Hadi kufikia mwezi Oktoba, 2015, fedha za Uchaguzi Mkuu zilizokuwa zimetolewa ni Shilingi **273,634,130,372/=** ambayo ni sawa na asilimia **99.99** ya fedha zote zilizoom



*Uhakiki wa Vifaa vilivyopokelewa kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015*.

#### 2.1.2.2 Uchapishaji wa Nyaraka za Uchaguzi

Tume ilichapisha nyaraka mbalimbali zilizotumika katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. Nyaraka zilizochapishwa ni Daftari na Orodha ya Wapiga Kura, fomu mbalimbali, karatasi za kura, kifaa kilichowasaidia Wapiga Kura Wasioona kupiga kura (*tactile ballot folder*), fomu za matokeo, mfano wa karatasi za kura, nyaraka za kisheria, mabango ya Elimu ya Mpiga Kura, mabango ya Vituo vya Kupigia Kura na *stickers.*

### 2.1.3 Mchango wa Washirika wa Maendeleo

Washirika wa Maendeleo kupitia mradi wa DEP unaosimamiwa na UNDP walitoa kiasi cha Shilingi **1,523,886,833/=** kwa ajili ya kugharamia zoezi la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, ukarabati wa Kituo cha Kuchakata taarifa za Wapiga Kura (*Data Processing Center),* uchapishaji wa Maadili ya Uchaguzi, Maelekezo kwa Watazamaji, mabango ya uhamashishaji wa uandikishaji kwa Mkoa wa Dar es salaam.

Aidha, UNDP walitoa baadhi ya vifaa kwa ajili ya shughuli za Uchaguzi. Vifaa hivyo, ni pamoja na *projector* saba kwa ajili ya mafunzo kwa Watendaji wa Uchaguzi, kompyuta sita kwa ajili ya Kituo cha Habari za Uchaguzi, kompyuta 171 na *printer* 171 kwa ajili ya kuwezesha mifumo iliyotumika katika kusajili wagombea, Kituo cha kujumlisha na kutangaza Matokeo katika Halmashauri. Vile vile, waligharamia ununuzi wa vifaa na uanzishwaji wa Kituo cha Mawasiliano (*Call Center)* na Kituo cha Kusajili Watazamaji wa Uchaguzi.



*Mkurugenzi wa Uchaguzi, Bw. Kailima R. Kombwey (kushoto) na Mkurungenzi Mkazi wa UNDP nchini Bi. Awa Dabo, wakikata utepe kuashiria uzinduzi wa Kituo cha Mawasiliano.*

## 2.2 Ratiba ya Uchaguzi Mkuu

Tume ya Taifa ya Uchaguzi hupanga Ratiba ya Uchaguzi Mkuu kwa kuzingatia siku ya Uteuzi kama iliyoanishiwa na kifungu cha 37(1)(a) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, ambacho kinaitaka Tume kupanga Siku ya Uteuzi wa wagombea iwe si chini ya siku **5** na si zaidi ya siku 25, baada ya kuvunjwa kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa mujibu wa Ibara ya 65 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bunge lilivunjwa rasmi tarehe 15 Agosti, 2015. Hivyo, kwa kuzingatia kifungu cha 37(1)(a) pamoja na tarehe ya kuvunjwa kwa Bunge, Tume ilipanga Ratiba ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015 kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 3.**

**Jedwali Na. 3: Ratiba ya Uchaguzi Mkuu 2015**

| Na. | Tukio | Tarehe |
|---|---|---|
| 1 | Siku ya Uteuzi wa Wagombea (Urais, Ubunge na Udiwani) | 21 Agosti, 2015 |
| 2 | Kampeni za Uchaguzi | 22 Agosti hadi 24 Oktoba, 2015 |
| 3 | Siku ya Kupiga Kura | 25 Oktoba, 2015 |

Pamoja na Ratiba ya Uchaguzi kutangazwa katika Tangazo la Serikali (*Government Notice* - GN) Na. 327, lililotolewa kwenye Gazeti la Serikali (*Government Gazette*) la tarehe 14 Agosti, 2015 pia ilitangazwa kwenye Vyombo mbalimbali vya Habari ili kuwawezesha Wadau wa Uchaguzi na Wananchi kwa ujumla kujua Ratiba kamili na hivyo kushiriki zoezi la Uchaguzi kikamilifu.

### 2.3 Marekebisho ya Sheria na Nyaraka nyingine za Uchaguzi

Tathmini iliyofanyika Baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 ilionesha kuwa kulikuwa na haja ya kufanyika marekebisho ya Sheria za Uchaguzi, Kanuni, Maadili ya Uchaguzi na Maelekezo kwa Watendaji na Wadau wa Uchaguzi.

#### 2.3.1 Sheria za Uchaguzi

Katika kuboresha Sheria za Uchaguzi, Tume ilipendekeza kufanya marekebisho katika maeneo yafuatayo:-

(i) Kupanga Siku ya Uchaguzi Mkuu isiwe siku ya ibada na itangazwe kuwa siku ya mapumziko;

(ii) Kufuta kifungu kinachoruhusu kufanyika Kampeni za nyumba kwa nyumba;

(iii) Mawakala wa Vyama vya Siasa kutoka katika Kata au Majimbo wanakoishi;

(iv) Kuruhusu Wanahabari kuingia ndani ya Vituo vya Kupigia Kura.

(v) Kuweka kipindi maalum cha kutangaza Matokeo ya Uchaguzi;

(vi) Kuruhusu mtu anayeweza kulipa fedha za dhamana katika Kesi ya Uchaguzi kulipa bila kupeleka maombi mahakamani;

(vii) Kumalizika kwa Kesi baada ya mdai kushindwa kulipa dhamana;

(viii) Kuongeza muda wa kusikiliza Kesi za Ubunge katika Mahakama Kuu; na

(ix) Kurekebisha Kifungu kinachotaka Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuahirisha Uchaguzi pale inapotokea Mgombea Mwenza amefariki dunia.

Mapendekezo ya Maboresho hayo yaliwasilishwa Serikalini. Hata hivyo, Sheria hazikuweza kubadilishwa kutokana na Mchakato uliokuwa unaendelea wa Katiba Inayopendekezwa.

#### 2.3.2 Kanuni za Uchaguzi

Katika kuhakikisha Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 unakuwa na ufanisi yalifanyika Marekebisho katika Kanuni za Uchaguzi za mwaka 2010. Marekebisho yaliyofanyika ni pamoja na:-

(i) Kuweka vifungu vya Kanuni kwa ajili ya usajili wa Watazamaji wa Uchaguzi ikiwa ni pamoja na kuwataka kuwasilisha taarifa za uangalizi ndani ya miezi mitatu;

(ii) Kuufanya Mwongozo wa Watazamaji wa Uchaguzi utambulike kama mojawapo ya kanuni za Uchaguzi;

(iii) Kuvitaka Vyama kuwasilisha barua za utambulisho wa Wagombea wao kwa Mamlaka za Uteuzi;

(iv) Tume kuainisha tarehe za Uteuzi; na

(v) Sheria ya Gharama za Uchaguzi Na. 6 ya mwaka 2010, kutambuliwa ndani ya Kanuni.

Aidha, Marekebisho hayo yalijumuisha kupata maoni kutoka kwa Wadau wa Uchaguzi, hususan Vyama vya Siasa. Kukamilika kwa Marekebisho hayo ya Kanuni za Uchaguzi za Mwaka 2010, kulipelekea Kanuni hizo kufutwa na kutangazwa kwa Kanuni mpya za Uchaguzi za mwaka 2015, kwenye Tangazo la Serikali Na. 307 lililotolewa kwenye Gazeti la Serikali la tarehe 31 Julai, 2015.

### 2.3.3 Maadili ya Uchaguzi

Kwa mujibu wa Kifungu cha 124A cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, na Kifungu cha 125 cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura 292, Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kushauriana na Serikali na Vyama vya Siasa ilifanya maboresho ya Maadili ya Uchaguzi ya mwaka 2010.

Mara baada ya kufanyika kwa marekebisho Maadili ya Uchaguzi yalisainiwa tarehe 27 Julai, 2015 na Wadau wote wa Maadili ambao ni Vyama vyote **22** vya Siasa, Tume na Serikali. Maadili hayo ya mwaka 2015, yalitangazwa katika Tangazo la Serikali Na. 294/2015.

Maboresho yalifanyika katika maeneo yafuatayo:-

(i) Kuongeza wigo wa matumizi ya Maadili ili kujumuisha Chaguzi ndogo zitakazofuata baada ya Uchaguzi Mkuu;

(ii) Kufanya marekebisho ya muda wa matumizi ya vipaza sauti kabla na baada ya kumalizika kwa Kampeni;

(iii) Kuongeza kipengele cha kuzuia Vyama na Wagombea wao kutumia lugha za uvunjaji wa amani au kuashiria ubaguzi wa kijinsia, ulemavu au maumbile kwenye Mikutano ya Kampeni;

(iv) Kuzuia Vyama kuonyesha ishara za Vyama vyao au kuvaa sare kwenye Mikutano ya Vyama vingine;

(v) Kuvitaka Vyama vya Siasa na Wagombea wahakikishe kuwa Mawakala wao wanakula viapo siku 7 kabla ya siku ya Upigaji Kura;

(vi) Kuongeza vipengele vya kuitaka Serikali izingatie mahitaji na Usalama wa Makundi Maalum, kama watu wenye Ulemavu, Wazee, na Wajawazito;

(vii) Kuwaongeza Wakuu wa Wilaya katika orodha ya Watendaji wa Serikali wanaotakiwa kuzingatia Maadili ya Uchaguzi;

(viii) Tume kuandaa na kupeleka kwa wakati vifaa vya kutosha kwenye Vituo vya Kupigia Kura ikiwa ni pamoja na vifaa vya watu wenye mahitaji maalum; na

(ix) Tume kuwawajibisha Wasimamizi wa Uchaguzi na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi kwa makosa yanayofanywa wakati wa Uchaguzi.

### 2.3.4 Maelekezo kwa Watendaji na Wadau wa Uchaguzi

Tume iliandaa Maelekezo kwa ajili ya Watendaji na Wadau wa Uchaguzi katika ngazi mbalimbali ili kuwawezesha kusimamia Zoezi la Uchaguzi kwa ufanisi. Maelekezo hayo ni;-

(i) Maelekezo kwa Wasimamizi wa Uchaguzi;

(ii) Maelekezo kwa Wasimamizi wa Vituo vya Kupigia Kura;

(iii) Maelekezo kwa Makarani Waongozaji wa Wapiga Kura;

(iv) Maelekezo kwa Vyama vya Siasa na Wagombea;

(v) Maelekezo kwa Mawakala wa Upigaji Kura;

(vi) Maadili ya Utoaji Elimu ya Mpiga Kura;

(vii) Mwongozo wa Utoaji Elimu ya Mpiga Kura; na

(viii) Mwongozo kwa Watazamaji wa Uchaguzi.

## 2.4 Majimbo ya Uchaguzi

Kwa mujibu wa Ibara ya 75(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ina jukumu la kuchunguza na kuigawa Jamhuri ya Muungano katika Majimbo ya Uchaguzi. Kwa ajili ya maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, Tume ilifanya uchunguzi wa Mipaka na kuanzisha jumla ya Majimbo mapya ya Uchaguzi **25**. Hivyo, katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, kulikuwa na jumla ya Majimbo **264,** ambapo Majimbo **214** yalikuwa ni ya Tanzania Bara na Majimbo **50** ni ya Tanzania Zanzibar. Idadi ya Majimbo hayo Kimkoa kwa Tanzania nzima ni kama yanavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 2** na **Ramani Na. 2.**

## Ramani Na. 2: Idadi ya Majimbo ya Uchaguzi Kimkoa.



### 2.4.1 Vigezo vya Ugawaji Majimbo

Katika kutekeleza zoezi la Ugawaji Majimbo, Tume ilibainisha vigezo vitakavyotumika katika kuchunguza mipaka na kugawa Majimbo ya Uchaguzi. Vigezo vilivyobainishwa ni vile vilivyopo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ambavyo ni idadi ya watu, upatikanaji wa mawasiliano na hali ya kijiografia.

Mwaka 2010, Tume ilifanya utafiti katika Jumuiya ya nchi zilizopo Kusini mwa Bara la Afrika, ili kujua vigezo vingine vinavyotumika katika nchi hizo kwa lengo la kutekeleza jukumu lake la kuchunguza mipaka na kugawa majimbo kwa ufanisi zaidi.

Baada ya utafiti huo, na kwa kuzingatia mashauriano na wadau mbalimbali, Tume iliongeza vigezo vingine na kuviingiza katika Jedwali la 3 la Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2010 ambavyo ni:-

(i) Wastani wa Idadi ya Watu (*Population Quota*);

(ii) Hali ya Kiuchumi;

(iii) Ukubwa wa Eneo la Jimbo husika;

(iv) Mipaka ya Kiutawala;

(v) Jimbo moja lisiwe ndani ya Wilaya/Halmashauri mbili;

(vi) Kata moja isiwe ndani ya Majimbo Mawili;

(vii) Mpangilio wa Maeneo ya Makazi ya Watu;

(viii) Mazingira ya Muungano;

(ix) Uwezo wa Ukumbi wa Bunge; na

(x) Idadi ya Viti Maalum vya Wanawake.

Aidha, kwa kuzingatia Ibara ya 75(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, katika Uchaguzi wa mwaka 2015, Tume ilitumia vigezo vitatu ambavyo ni:

(i) Idadi ya Watu, ambapo Tume iliamua kuyagawa Majimbo yote yaliyokuwa na idadi ya Watu zaidi ya 400,000;

(ii) Ukubwa wa Ukumbi wa Bunge; na

(iii) Mipaka ya Kiutawala.

### 2.4.2 Taratibu za Ugawaji wa Majimbo

Tume ilitangaza kuanza kwa mchakato wa ugawaji wa majimbo kwa kupokea maombi kuanzia tarehe 28 Aprili, 2015 na mwisho wa kuwasilisha maombi ilikuwa tarehe 30 Mei, 2015.

Katika tangazo hilo, Tume ilibainisha utaratibu uliopaswa kufuatwa na Halmashauri zote katika kuwasilisha maombi ya kuchunguza mipaka na kugawa majimbo. Utaratibu huo ulikuwa ni kama ifuatavyo:-

(i) Maombi ya Kuchunguza Mipaka na Kugawa Majimbo kuwasilishwa kwa Mkurugenzi wa Halmashauri husika kwa ajili ya kujadiliwa katika vikao rasmi vya Halmashauri husika;

(ii) Mkurugenzi wa Halmashauri husika kuwasilisha maombi kwa Katibu Tawala wa Mkoa;

(iii) Katibu Tawala wa Mkoa kuwasilisha maombi katika Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa ;

(iv) Baada ya kupitishwa na Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa, maombi hayo kuwasilishwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi;

(v) Tume kupitia maombi yaliyowasilishwa;

(vi) Tume kutembelea Majimbo yote yaliyokidhi vigezo kwa ajili ya uhakiki; na

(vii) Tume kutangaza Majimbo Mapya.

### 2.4.3 Majimbo Mapya ya Uchaguzi

Halmashauri **37** ziliwasilisha maombi ya kuchunguza na kugawa majimbo ya Uchaguzi. Katika Halmashauri hizo ni Majimbo **42** yaliombewa kugawanywa. Tume ilitembelea majimbo yote yaliyokidhi vigezo na kustahili kugawanywa ambapo ilikutana na wadau na kupata maoni yao juu ya jimbo husika. Tume iliona umuhimu wa kugawanywa kwa majimbo hayo na hivyo kufikia uamuzi wa kuanzisha majimbo mengine mapya.

Kwa kuzingatia vigezo vya wastani wa idadi ya watu, mipaka ya kiutawala na uwezo wa ukumbi wa Bunge na kwa mujibu wa Ibara ya 75(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Tume iliamua kuanzisha majimbo mapya **25** ambapo:-

(i) Majimbo **19** yalianzishwa kutokana na ongezeko la Halmashauri mpya (mipaka ya kiutawala kubadilika); kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 4**.

(ii) Majimbo **6** yalianzishwa kutokana na kigezo cha wastani wa idadi ya watu kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 5**.

**Jedwali Na. 4: Orodha ya Majimbo yaliyotokana na Ongezeko la Halmashauri**

| Na. | Halmashauri | Jimbo lililogawanywa | Jimbo Jipya |
|---|---|---|---|
| 1. | Mji Handeni | Handeni | Handeni Mjini |
| 2. | Mji Nanyamba | Mtwara Vijijini | Nanyamba |
| 3. | Mji Makambako | Njombe Kaskazini | Makambako |
| 4. | Mji Butiama | Musoma Vijijini | Butiama |
| 5. | Mji Tarime | Tarime | Tarime Mjini |
| 6. | Mji Tunduma | Mbozi | Tunduma |
| 7. | Wilaya ya Nsimbo | Mpanda Vijijini | Nsimbo |
| 8. | Wilaya ya Mpimbwe | Mlele | Kavuu |
| 9. | Mji Geita | Geita | Geita Mjini |
| 10. | Mji Mafinga | Mufindi Kaskazini | Mafinga Mjini |
| 11. | Mji Kahama | Kahama | Kahama Mjini |
| 12. | Wilaya ya Ushetu | Kahama | Ushetu |
| 13. | Mji Nzega | Nzega | Nzega Mjini |
| 14. | Mji Kondoa | Kondoa | Kondoa Mjini |
| 15. | Mji Newala | Newala | Newala Mjini |
| 16. | Mji Mbulu | Mbulu | Mbulu Mjini |
| 17. | Mji Bunda | Bunda | Bunda Mjini |
| 18. | Wilaya ya Masasi | Lulindi | Ndanda |
| 19. | Wilaya ya Madaba | Peramiho | Madaba |

**Jedwali Na. 5: Orodha ya Majimbo yaliyotokana na kigezo cha idadi ya Watu**

| Na. | Halmashauri | Jimbo Lililogawanywa | Jimbo Jipya |
|---|---|---|---|
| 1. | Manispaa ya Temeke | Temeke | Mbagala |
| 2. | Wilaya ya Mbozi | Mbozi Magharibi | Vwawa |
| 3. | Wilaya ya Igunga | Igunga | Manonga |
| 4. | Manispaa ya Kinondoni | Kinondoni/Ubungo | Kibamba |
| 5. | Wilaya ya Kilombero | Kilombero | Mlimba |
| 6. | Wilaya ya Tabora (Uyui) | Tabora Kaskazini | Ulyankulu |

Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar iliongeza majimbo na kufikia **54**, lakini Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilibakia na majimbo **50.**

Hii ilitokana na matakwa ya kikatiba kwa kuzingatia Ibara ya 98 (1) (b) inayoeleza kuwa mabadiliko yoyote yaliyopo katika Orodha ya Pili kwenye Nyongeza ya Pili ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, yatapitishwa iwapo

yameungwa mkono na theluthi mbili ya Wabunge wote wa Tanzania Bara na theluthi mbili ya Wabunge wote wa Zanzibar.

Tume haikuongeza majimbo ya Zanzibar kufikia **54**, kwa sababu wakati Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar inaongeza Majimbo, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilikuwa linamaliza vikao vyake na kwa kuzingatia muda uliobakia, Tume ya Taifa ya Uchaguzi haikuweza kuanzisha mchakato wa kuongeza majimbo ya Zanzibar kufikia **54**.

Kulingana na matakwa ya kikatiba kama ilivyotangulia kuelezwa, Tume iliamua kubaki na majimbo **50** kwa upande wa Tanzania Zanzibar.

Kwa maana ya kubakia na majimbo **50** kwa upande wa Tanzania Zanzibar, Tume ya Taifa ya Uchaguzi iliamua kuunganisha majimbo manne (4) kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 6.**

**Jedwali Na. 6: Majimbo yaliyounganishwa kwa Upande wa Tanzania Zanzibar**

| Na. | Majimbo Yaliyounganishwa | Jina la Jimbo |
|---|---|---|
| 1. | Mtoni na Bububu | Bububu |
| 2. | Mtopepo na Mwera | Mwera |
| 3. | Kiembesamaki na Chukwani | Chukwani |
| 4. | Pangawe na Kijitoupele | Kijitoupele |

### 2.4.4 Majimbo yaliyobadilishwa Majina

Pamoja na Tume kupokea maombi ya kugawanya Majimbo, pia ilipokea jumla ya Majimbo 11 yaliyoomba kubadilisha majina. Majimbo hayo ni kama yanavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 7.**

**Jedwali Na. 7: Orodha ya Majimbo yaliyobadilishwa Majina kwa Tanzania Bara**

| Na. | Halmashauri | Jina la awali | Jina jipya |
|---|---|---|---|
| 1. | Wilaya ya Busokelo | Rungwe Mashariki | Busokelo |
| 2. | Wilaya ya Rungwe | Rungwe Magharibi | Rungwe |
| 3. | Wilaya ya Kaliua | Urambo Magharibi | Kaliua |
| 4. | Wanging'ombe | Njombe Magharibi | Wanging'ombe |
| 5. | Wilaya ya Urambo | Urambo Mashariki | Urambo |
| 6. | Wilaya ya Njombe | Njombe Kusini | Lupembe |
| 7. | Wilaya ya Bariadi | Bariadi Mashariki | Itilima |
| 8. | Mji wa Bariadi | Bariadi Magharibi | Bariadi |
| 9. | Wilaya ya Kondoa | Kondoa Kaskazini | Kondoa |
| 10 | Wilaya ya Chemba | Kondoa Kusini | Chemba |
| 11 | Wilaya ya Singida | Singida Mashariki | Ikungi |

## 2.5 Kutangazwa kwa Kata za Uchaguzi

Baada ya kukamilika kwa zoezi la ugawaji wa Majimbo na kupokea taarifa ya Mipaka ya Kiutawala hususan Kata mpya zilizoanzishwa katika Halmashauri mbalimbali za Tanzania Bara, Tume iliandaa Taarifa (*Notice*) kwa ajili ya kutangaza katika Gazeti la Serikali Majimbo na Kata za Uchaguzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

Majimbo na Kata za Uchaguzi yalitangazwa rasmi katika Gazeti la Serikali Namba 295 la tarehe 23 Julai, 2015 ambapo yalichapishwa jumla ya Majimbo **264** na Kata **3,957.**

Hata hivyo, ilibainika kuwa Kata 4 za Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu hazikusimamisha Wagombea katika Uchaguzi wa Madiwani, hiyo ilitokana na Mabadiliko ya Mipaka ya Kiutawala. Aidha, Kata **7** zilikuwa zinajirudia katika Halmashauri mbalimbali. Hivyo, jumla ya Kata zilizofanya Uchaguzi wa Madiwani ni Kata **3,946** badala ya Kata **3,957** zilizotangazwa.

## 2.6 Ugawaji na Usambazaji wa Vifaa

Ugawaji na usafirishaji wa vifaa kwenda majimboni ulifanyika mapema ili kutoa nafasi kwa Maafisa Waandikishaji kuhakiki vifaa hivyo na kupata muda wa kukabiliana na upungufu wa vifaa iwapo ungejitokeza. Vifaa vya uandikishaji vilipokelewa kwa nyakati tofauti kadiri Zoezi la Uandikishaji lilivyokuwa likifanyika kwenye mikoa husika.

Kwa upande wa vifaa vya uchaguzi, ugawaji na usambazaji wa vifaa hivyo ulifanyika kwa kuzingatia mahitaji na umbali wa kutoka Makao Makuu ya Tume Dar es Salaam mpaka kwenye Kanda kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 8**. Hivyo, vifaa vilianza kusambazwa kwenye Halmashauri za mbali. Mpaka kufikia tarehe 23 Oktoba, 2015, Halmashauri zote zilikuwa zimepokea vifaa vya uchaguzi.

**Jedwali Na. 8: Ugawaji wa Vifaa kwa Kanda**

| Na. | Kanda | Mikoa |
|---|---|---|
| 1. | Ziwa | Mwanza, Mara, Kagera, Simiyu, Geita na Shinyanga |
| 2. | Kaskazini | Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara |
| 3. | Kati | Dodoma, Singida, Tabora na Kigoma |
| 4. | Kusini | Mtwara na Lindi |
| 5. | Nyanda za juu Kusini | Iringa, Njombe, Ruvuma, Mbeya, Katavi na Rukwa |
| 6. | Pwani | Dar Es Salaam, Pwani na Morogoro |
| 7. | Zanzibar | Unguja na Pemba |

### 2.7 Watendaji wa Uchaguzi

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imekuwa ikiwatumia Watendaji mbalimbali wakati wa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na Uchaguzi Mkuu. Watendaji hawa wa Uchaguzi wamegawanyika katika Sehemu Kuu mbili ambazo ni Watumishi wa Tume waliopo Makao Makuu na Watendaji wa Uchaguzi wa Mikoa, Halmashauri, Majimbo, Kata na Vituo.

#### 2.7.1. Watumishi wa Tume

Tume ya Taifa ya Uchaguzi ina jumla ya watumishi wa kudumu **143** ambao ndio waliotumika katika Zoezi la Uchaguzi Mkuu. Kutokana na upungufu wa rasilimali watu, Tume iliajiri kwa Mkataba Vibarua **869**, na Watumishi **68** walihamishiwa kwa muda kutoka katika Idara na Taasisi mbalimbali za Serikali kwa lengo la kusaidia kufanikisha shughuli za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

#### 2.7.2 Uteuzi wa Watendaji wa Uchaguzi ngazi ya Mkoa, Halmashauri, Jimbo, Kata na Vituo

Kwa kuzingatia Vifungu vya 7(1), 7(2) na 8(1) vya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na Vifungu vya 9(1) na 9(2) vya Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Tume ilifanya Uteuzi wa Watendaji mbalimbali waliosimamia shughuli za Uchaguzi katika ngazi za Mkoa, Halmashauri, Jimbo, Kata na Vituo vya Kupigia Kura ambao ni:-

**(i) Waratibu wa Uchaguzi wa Mikoa**

Tume iliteua Mratibu wa Uchaguzi kwa kila Mkoa wa Tanzania Bara na Waratibu wa Mkoa wawili kwa Tanzania Zanzibar (mmoja kwa mikoa miwili ya Pemba na mmoja kwa mikoa mitatu ya Unguja). Hivyo, Tume iliteua jumla ya Waratibu wa Mikoa **27.**

Waratibu wa Uchaguzi wa mikoa walikuwa na majukumu ya kuratibu masuala yote yanayohusu vifaa, mafunzo na taratibu zote za Uchaguzi katika mikoa yao. Pamoja na kushirikiana na kushauriana na Wasimamizi wa Uchaguzi waliopo katika mikoa yao.

**(ii) Wasimamizi wa Uchaguzi katika Halmashauri**

Tume iliteua Msimamizi wa Uchaguzi mmoja katika Halmashauri **179** zilizohusika na Uchaguzi Tanzania Bara na Wasimamizi wa Uchaguzi **10** Tanzania Zanzibar. Hivyo, kulikuwa na jumla ya Wasimamizi wa Uchaguzi **189** katika uchaguzi wa mwaka 2015.

Majukumu ya Msimamizi wa Uchaguzi yalikuwa ni kuratibu masuala yote yanayohusiana na usimamizi wa fedha, vifaa, mafunzo na taratibu za uchaguzi katika Halmashauri zao.

**(iii) Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya Jimbo.**

Tume iliwateua Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi watatu (3) kwa kila jimbo kwa Tanzania Bara na wawili (2) kwa kila jimbo kwa Tanzania Zanzibar. Katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, Tanzania Bara ilikuwa na jumla ya Wasimamizi Wasaidizi ngazi ya jimbo **642** na Tanzania Zanzibar **100**. Hivyo, kufanya jumla ya Watendaji kuwa **742.**

**(iv) Maafisa Uchaguzi**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilianza kuwatumia Maafisa Uchaguzi katika kila Halmashauri nchini katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010. Katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, Tume iliendelea kuwatumia Maafisa Uchaguzi ngazi ya Halmashauri Tanzania Bara ambao walikuwa na jukumu la kuwasaidia Wasimamizi wa Uchaguzi katika Kuratibu mambo mbalimbali yanayohusiana na uchaguzi. Jumla ya Maafisa Uchaguzi **179** Tanzania Bara walishiriki katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

**(v) Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya Kata.**

Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya Kata walikuwa na jukumu la kusimamia Uchaguzi katika Kata zao wakishirikiana na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya Jimbo. Aidha, Tume iliamua kuwa na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi wawili kwa kila Kata, kwa Tanzania Bara. Jumla ya Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya Kata ilikuwa **7,892.**

**(vi) Watendaji Katika Vituo Vya Kupigia Kura.**

Katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, Tume iliandaa jumla ya Vituo vya Kupigia Kura **65,105** ambapo Vituo **63,525** vilikuwa Tanzania Bara na Vituo **1,580** vilikuwa Tanzania Zanzibar. Katika kila Kituo cha Kupigia Kura kulikuwa na jumla ya Watendaji watano ambao waliteuliwa na Wasimamizi wa Uchaguzi kufanya kazi za Uchaguzi Vituoni. Watendaji hao ni:-

(a) Msimamizi wa Kituo mmoja;

(b) Wasimamizi Wasaidizi wa Kituo wawili;

(c) Karani Mwongozaji wa Wapiga Kura mmoja;

(d) Mlinzi mmoja;

(e) Wasimamizi Wasaidizi wa Kituo wa Akiba wawili kwa kila Kata; na

(f) Makarani Waongozaji Wapiga Kura wa Akiba wawili kila Kata.

Hivyo, kulikuwa na jumla ya Watendaji **341,309** wa Uchaguzi Vituoni. Orodha na idadi yao ni kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 9.**

**Jedwali Na. 9: Idadi ya Watendaji wa Uchaguzi Vituoni**

| Na | Watendaji | Idadi |
|---|---|---|
| 1. | Wasimamizi wa Vituo | 65,105 |
| 2. | Wasimamizi Wasaidizi wa Kituo | 130,210 |
| 3. | Makarani Waongozaji Wapiga Kura | 65,105 |
| 4. | Mlinzi mmoja wa Kituo | 65,105 |
| 5. | Wasimamizi Wasaidizi wa Akiba | 7,892 |
| 6. | Makarani Waongozaji wa Akiba | 7,892 |
| **Jumla** | | **341,309** |

### 2.8 Mafunzo kwa Watendaji

Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilitoa Mafunzo kwa Watendaji wote wa Uchaguzi kabla ya kuanza kwa zoezi la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na wakati wa maandalizi ya Uchaguzi Mkuu. Lengo la Mafunzo hayo ni kuwajengea uelewa na uwezo wa kusimamia shughuli hizo. Mafunzo yalitolewa kwa awamu kuanzia na Watendaji wa Tume Makao Makuu na baadae Watendaji wa shughuli za Uandikishaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na Uchaguzi ngazi ya Jimbo na hatimae Maafisa ngazi ya Jimbo kufikisha mafunzo hayo ngazi ya Kata na Vituo.

#### 2.8.1 Mafunzo kwa Watumishi wa Tume Makao Makuu

Tume iliandaa mafunzo kwa watumishi wake wa kada mbalimbali kwa lengo la kuwajengea uwezo ili waweze kutoa elimu hiyo kwa Watendaji wa Uandikishaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na Watendaji wa Uchaguzi wa ngazi ya Mkoa na Halmashauri. Mafunzo hayo yalikuwa mafunzo kwa wakufunzi (*Training of Trainers* - TOT).

Wakati wa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, mafunzo yaliyotolewa yalijumuisha Ujazaji wa Fomu za Uandikishaji Wapiga Kura na matumizi ya BVR *Kits* katika kuandikisha Wapiga Kura.

Wakati wa maandalizi ya Uchaguzi Mkuu, mafunzo yaliyotolewa yalijumuisha Uteuzi wa Wagombea, Taratibu za Upigaji Kura, Kuhesabu Kura, Kujumlisha Kura, Mfumo wa Menejimenti ya Wagombea na Mfumo wa Menejimenti ya Matokeo na Kutangaza Matokeo.

### 2.8.2 Mafunzo kwa Watendaji wa Ngazi ya Mkoa, Halmashauri, Kata na Vituo.

**(i) Mafunzo kwa Watendaji Ngazi ya Mkoa na Halmashauri**

Wakati wa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, Wakufunzi wa Tume waliwapatia mafunzo Waratibu wa Uandikishaji wa Mikoa, Maafisa Uandikishaji wa Halmashauri, Maafisa Waandikishaji Wasaidizi na Wataalamu wa TEHAMA wa Halmashauri.

Vile vile, wakati wa Uchaguzi Mkuu, Wakufunzi kutoka Tume walitoa Mafunzo kwa Waratibu wa Uchaguzi wa Mikoa, Wasimamizi wa Uchaguzi, Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya jimbo na Maafisa Uchaguzi wa Halmashauri.

**(ii) Mafunzo kwa Watendaji Ngazi ya Kata**

Mafunzo kwa ajili ya Maafisa Waandikishaji Wasaidizi ngazi ya Kata yalitolewa na Maafisa Waandikishaji wakisaidiana na Maafisa Waandikishaji Wasaidizi ngazi ya Halmashauri wakati wa Uboreshaji wa Daftari.

Aidha, wakati wa Uchaguzi Mkuu, Mafunzo kwa ajili ya Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya Kata yalitolewa na Wasimamizi wa Uchaguzi wakisaidiana na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya Jimbo. Mafunzo haya yaliendeshwa kwa ngazi ya Halmashauri kwa Tanzania Bara.

**(iii) Mafunzo kwa Watendaji wa Uchaguzi ngazi ya Vituo**

Wakati wa maandalizi ya zoezi la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Maafisa Waandikishaji ngazi ya Kata waliendesha mafunzo kwa Maafisa Waandikishaji Wapiga Kura wa Vituo na BVR *Kit Operators*.

Aidha, wakati wa Uchaguzi Mkuu, mafunzo yalitolewa kwa Wasimamizi wa Vituo, Wasimamizi Wasaidizi wa Vituo na Makarani Waongozaji wa Wapiga Kura. Mafunzo haya yaliratibiwa na kutolewa na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya Kata wakishirikiana na wale wa ngazi ya Jimbo.

## 2.9 Elimu ya Mpiga Kura

Kutoa na Kuratibu Elimu ya Mpiga Kura ni moja ya majukumu ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Hii, ni kwa mujibu wa Kifungu cha 4C cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343. Elimu hii ni muhimu kwa kuwa huwaelimisha Wapiga Kura juu ya umuhimu na namna ya kutumia haki yao ya Kikatiba na kuwahamasisha kushiriki katika mchakato wa uchaguzi, ili kutumia haki yao ya Kupiga Kura kikamilifu.

### 2.9.1 Utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura katika Uchaguzi wa mwaka 2015

Katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilitoa Elimu ya Mpiga Kura ili kuwahamasisha Wapiga Kura kujitokeza kushiriki kikamilifu katika hatua zote za Uchaguzi. Kabla ya kuanza kutoa elimu hiyo, Tume ilifanya maandalizi

yaliyolenga kufanikisha utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura. Maandalizi hayo yalihusisha uandaaji wa Mkakati wa Elimu ya Mpiga Kura.

Mkakati huo ulikuwa ndio nyenzo kuu ya kuiwezesha Tume kufanikisha jukumu la utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura nchi nzima. Aidha, uliweka utaratibu wa Tume kuratibu Asasi na Taasisi zitakazohusika na utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura.

Maandalizi mengine yaliyofanyika ni kuandaa Mwongozo na Maadili kwa ajili ya Asasi/Taasisi zilizotoa Elimu ya Mpiga Kura. Asasi zilizoomba na kupata Kibali cha kutoa Elimu ya Mpiga Kura, zililazimika kufuata na kutekeleza Mwongozo na Maadili hayo.

Elimu ya Mpiga Kura ilitolewa kwa njia mbalimbali ili kuweza kuwafikia Wapiga Kura wa Makundi yote na katika maeneo mbalimbali na ikiwa ni pamoja na maeneo ya Vijijini. Utoaji wa Elimu hiyo ulifanyika katika kipindi cha Uboreshaji na Uchaguzi Mkuu. Njia zilizotumika kutoa Elimu ya Mpiga Kura ni pamoja na:-

**(i) Uendeshaji wa Mikutano na Wadau wa Uchaguzi**

Tume iliandaa na kuendesha mikutano mbalimbali na Wadau wa Uchaguzi. Mikutano hiyo iliwahusisha Viongozi wa Dini, Vyama vya Siasa, Wamiliki na Wahariri wa Vyombo vya Habari, Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu. Lengo la mikutano hiyo lilikuwa ni kuhamasisha na kuelimisha juu ya taratibu za Uchaguzi. Mikutano hiyo ilifanyika katika kipindi cha kuanzia uandikishaji wa Wapiga Kura hadi Uchaguzi.



*Baadhi ya Washiriki wa Mkutano wa Wadau wa Uchaguzi kutoka Makundi ya Watu wenye Mahitaji Maalum.*

**(ii) Vipindi vya Redio na Runinga**

Tume iliandaa na kushiriki katika vipindi mbalimbali vya Redio na Runinga kuhusu masuala ya uchaguzi. Vipindi hivyo vililenga kuelimisha Wapiga Kura juu ya Sheria mbalimbali za Uchaguzi, umuhimu wa kujitokeza kujiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, Maadili ya Uchaguzi, Uteuzi wa Wagombea, Kampeni za Uchaguzi, Taratibu za Upigaji Kura, Kuhesabu, Kujumlisha na Kutangaza Matokeo. Vipindi hivyo ni pamoja na;-

(a) TBC1 vipindi vya Tuambie, Kura yangu na Jambo Tanzania

(b) Azam TV vipindi vya *Morning Trumpet* na Funguka

(c) Channel Ten kipindi cha Tufunge Safari

(d) Clouds Redio kipindi cha Temino na *Power Breakfast*

(e) Micheweni FM Kipindi cha Majadiliano ya Uchaguzi

(f) Zanzibar Broadcasting Corporation (ZBC) Uchaguzi Mkuu

(g) East African TV kipindi cha kikaangoni

(h) TBC Taifa kipindi cha Tuambie na Jambo Tanzania

(i) Voice of America kipindi cha *Straight Talk Africa*

(j) BBC kipindi cha *Focus on Africa*

(k) ITV kipindi cha Mtiti wa Uchaguzi

(l) Star TV kipindi cha Tuongee Asubuhi

**(iii) Machapisho na Makala**

Kwa Mujibu wa Kanuni ya 5(1) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2015, Tume iliandaa machapisho ya uelimishaji kama: Maswali yaulizwayo mara kwa mara, Wagombea na Vyama vya Siasa, Uchaguzi Huru ni Kielelezo cha Demokrasia. Aidha, makala kadhaa ziliandaliwa na kutolewa katika magazeti kama vile Wanawake na Uchaguzi.

**(iv) Tovuti na Mitandao ya kijamii**

Tume ilitumia tovuti yake ya www.nec.go.tz, Mitandao ya Kijamii (Facebook, Twitter na HulkShare) na MyRadioStream.com katika kuelimisha na kutoa Elimu ya Mpiga Kura kwa Wadau.

**(v) Mabango**

Tume iliandaa mabango ya uhamasishaji kama vile, Bango Mchakato na Bango Taarifa ambayo yalisambazwa maeneo mbalimbali ya Nchi kwa ajili ya kutoa Elimu ya Mpiga Kura na kuhamasisha wananchi kushiriki katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka

2015. Pia, mabango ya barabarani yaliandaliwa hasa katika miji mikubwa kwa lengo la uhamasishaji.

**(vi) Kituo cha Mawasiliano**

Tume ilianzisha Kituo cha Mawasiliano na Wapiga Kura kwa ajili ya kutoa taarifa za Uchaguzi Mkuu. Kituo hicho kilikuwa na madhumuni ya kupokea malalamiko na kutoa ufafanuzi wa maswali yanayohusu masuala ya Uchaguzi. Kituo kilizinduliwa tarehe 12 Oktoba, 2015 na namba **0800782100** ilitolewa ambapo Wananchi walipiga simu pasipo malipo na kupatiwa ufafanuzi uliohitajika.

Hadi Kituo kilipofungwa tarehe 30 Oktoba, 2015 kilikuwa kimepokea simu **78,911** kutoka kwa wananchi mbalimbali.

**(vii) Matangazo ya Redio, Runinga na Magazeti**

Tume iliandaa matangazo ya Redio (*jingles*) na Runinga (*TV spots*) ambayo yalitolewa katika Vituo vya Runinga **10** na Redio za Kijamii **47**. Aidha, matangazo yalitolewa katika magazeti mbalimbali ili kuhakikisha kila mwananchi anapata taarifa sahihi za kumuwezesha Kupiga Kura.

### 2.9.2 Uratibu wa Asasi za kutoa Elimu ya Mpiga Kura

Kwa mujibu wa Kifungu cha 4C cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, Tume ilitoa fursa kwa Asasi za Kiraia kuwasilisha maombi ya kutoa Elimu ya Mpiga Kura katika maeneo mbalimbali nchini. Tume ilipitia na kuchambua maombi yaliyowasilishwa ili kujiridhisha iwapo Asasi hizo zimekidhi vigezo vilivyowekwa. Kati ya Asasi **451** zilizoomba kutoa Elimu ya Mpiga Kura ni Asasi **447** tu, zilikidhi vigezo na kupewa kibali kwa ajili ya kutoa Elimu ya Mpiga Kura katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

Asasi zilizopewa kibali cha kutoa Elimu ya Mpiga Kura zilitakiwa kufuata Mwongozo wa utoaji Elimu ya Mpiga Kura na Maadili ya utoaji wa elimu hiyo.

## SURA YA TATU

## UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA

### 3.1 Daftari la Kudumu la Wapiga Kura

Daftari la Kudumu la Wapiga Kura lilianzishwa mwaka 2004 kwa mujibu wa Ibara ya 5(3)(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Aidha, Daftari hili lilitumika kwa mara ya kwanza katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005.

Kifungu cha 15(5) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, kinaitaka Tume ya Taifa ya Uchaguzi kufanya Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura mara mbili kati ya Uchaguzi Mkuu mmoja na mwingine. Mara baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 na kabla ya kufanyika kwa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015**,** Tume ilifanya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa mara moja tu na siyo mara mbili kama Sheria inavyoelekeza. Hii ni kutokana na kutokupatikana fedha kwa wakati kwa ajili ya ununuzi wa vifaa.

### 3.1.1 Teknolojia iliyotumika Kuandikisha Wapiga Kura

Wakati wa uanzishwaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilitumia Teknolojia ya *Optical Mark Recognition* (OMR) kuandikisha Wapiga Kura. Teknolojia hiyo ilihusisha kuingiza na kusahihisha taarifa za Wapiga Kura kwa kutumia fomu maalum. Fomu hizo zilitumika kuingiza taarifa (baada ya kuwa *scanned*) kwenye Kanzidata kwa ajili ya kuandaa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Tume iliamua kuacha kutumia Teknolojia ya OMR baada ya kuonekana kuwa na changamoto, kama vile:-

(i) Teknolojia hiyo kushindwa kutambua Wapiga Kura waliojiandikisha zaidi ya mara moja;

(ii) Teknolojia hiyo kushindwa kuhuisha taarifa za Wapiga Kura waliohama kutoka sehemu moja kwenda nyingine;

(iii) Teknolojia ya OMR ililazimu fomu za uandikishaji kusafirishwa kutoka katika Vituo vya kuandikishia hadi makao makuu ya Tume, hivyo kulikuwa na uwezekano mkubwa wa Taarifa hizo kupotea kabla ya kuingizwa kwenye Kanzidata; na

(iv) Urahisi wa kughushi Kadi za Wapiga Kura ulikuwa mkubwa.

Ili kuondoa upungufu huo na kuwezesha kuwa na Daftari la Kudumu la Wapiga Kura linaloaminika, Tume iliamua kuandikisha Wapiga Kura kwa kutumia Teknolojia ya *Biometric Voters Registration* (BVR).

Huu ni mfumo wa kuandikisha Wapiga Kura kwa kuchukua na kuhakiki taarifa za kibaiolojia kama vile alama za vidole vya mkono, picha na saini za Mpiga Kura na kuzihifadhi kwenye Kanzidata kwa ajili ya utambuzi. Matumizi makubwa ya teknolojia hii ni kumtambulisha Mpiga Kura kwa kutumia taarifa zake binafsi. *Biometric Voters Registration Kit* ni kama inavyoonekana kwenye **Mchoro Na. 3.**

## Mchoro Na. 3: Biometric Voters Registration Kit



### 3.1.2 Upokeaji wa BVR *Kits*

Tume ilipokea **BVR *Kits* 8,000** kwa awamu tofauti kama inavyoonesha katika **Jedwali Na. 10.**

**Jedwali Na. 10: Ratiba ya Upokeaji wa BVR *Kits***

| Na. | Maelezo | Tarehe za Upokeaji | Idadi ya BVR *Kits* |
|---|---|---|---|
| 1. | BVR *Kits* za mafunzo | 22 Oktoba, 2014 | 10 |
| 2. | BVR *Kits* za zoezi la majaribio | 9 Desemba, 2014 | 240 |
| 3. | Awamu ya Kwanza | 12 Aprili, 2015 | 248 |
| 4. | Awamu ya Pili | 17 Aprili, 2015 | 1,600 |
| 5. | Awamu ya Tatu | 25 Aprili, 2015 | 1,600 |
| 6. | Awamu ya Nne | 3 Mei, 2015 | 1,152 |
| 7. | Awamu ya Tano | 20 Mei, 2015 | 1,580 |
| 8. | Awamu ya Sita | 29 Mei, 2015 | 1,570 |
| **Jumla** | | | **8,000** |



*Baadhi ya BVR Kits zilizotumika kwenye Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura zikiwa zimehifadhiwa ghalani*

### 3.2 Uandikishaji wa Majaribio.

Kabla ya kuanza zoezi la Uandikishaji wa Wapiga Kura, Tume ilifanya zoezi la Uandikishaji wa majaribio kwa kutumia teknolojia ya BVR ili kubaini ufanisi na changamoto zinazoweza kujitokeza na kuzipatia ufumbuzi. Katika zoezi hilo la majaribio zilitumika BVR *Kits* **250.** Majaribio ya Uandikishaji yalifanyika katika maeneo matatu ambayo ni:-

(i) Mkoa wa Dar es Salaam - Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, katika Kata za Bunju na Mbweni kuanzia tarehe 16 hadi 22 Desemba, 2014 ambapo BVR *Kits* **90** zilitumika.

(ii) Mkoa wa Morogoro - Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero, katika Kata za Ifakara, Katindiuka, Lipangalala, Mlabani na Viwanja Sitini kuanzia tarehe 15 hadi 21 Desemba, 2014 ambapo BVR Kits 80 zilitumika.

(iii) Mkoa wa Katavi - Halmashauri ya Wilaya ya Mlele, katika Kata za Ikuba, Usevya na Kibaoni kuanzia tarehe 17 hadi 23 Desemba, 2014 ambapo BVR Kits 80 zilitumika.

#### 3.2.1 Matokeo ya Uandikishaji wa Majaribio.

Katika zoezi la majaribio Tume ilikadiria kuandikisha Wapiga Kura **42,706** ambapo ilifanikiwa kuandikisha Wapiga Kura **45,521** ambayo ni ziada ya Wapiga Kura **2,815** ya waliokadiriwa kuandikishwa kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 11.**

**Jedwali Na. 11: Idadi ya walioandikishwa kwenye zoezi la majaribio**

| Na. | Halmashauri | Lengo la Uandikishaji | Walioandikishwa | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Manispaa ya Kinondoni | 14,312 | 15,123 | 105.66 |
| 2. | Wilaya ya Mlele | 11,104 | 11,210 | 100.95 |
| 3. | Wilaya ya Kilombero | 17,290 | 19,188 | 110.97 |
| | **JUMLA** | **42,706** | **45,521** | **106.59** |

Kutokana na Uandikishaji wa majaribio, Tume ilifanikiwa kubaini mapungufu mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Hali ya hewa katika baadhi ya maeneo yenye mvua ilisababisha BVR *Kits* kushindwa kufanya kazi kutokana na kukosa umeme wa jua wa kutosha;

(ii) BVR *Kits* kushindwa kufanya kazi kwa ufanisi katika maeneo yenye joto kali mfano Dar es Salaam; na

(iii) Kutokana na teknolojia mpya ya BVR na uzoefu mdogo, Watendaji walifanya kazi kwa kasi ndogo siku za mwanzo.

### 3.2.2 Hatua zilizochukuliwa

Katika kukabiliana na changamoto zilizojitokeza wakati wa majaribio, Tume ilichukua hatua zifuatazo:

(i) Kuwapa Watendaji (BVR *Kit Operators*) mafunzo zaidi kuhusu namna ya kutumia na kurekebisha matatizo madogo madogo yanayoweza kujitokeza;

(ii) Kuwezesha Mfumo wa Uandikishaji kuonyesha idadi halisi ya Wapiga Kura walioandikishwa kwa siku. Hii, ilisaidia kuonesha utendaji kazi wa BVR *Kit Operators* na kusaidia kuratibu wanaoandikishwa;

(iii) Mfumo wa BVR uliwezeshwa kuifanya kompyuta mpakato (Laptop) kuonesha hali ya kila kifaa kilichomo ndani ya BVR *Kit*, hivyo kusaidia kubaini tatizo kwa haraka;

(iv) Kuiboresha BVR *Kit* ili kuweza kufanya kazi kwenye mazingira ya joto bila ya usumbufu; na

(v) Kuongeza jenereta kwa maeneo ambayo hayakuwa na umeme.

### 3.3 Uandikishaji wa Wapiga Kura

Tume ya Taifa ya Uchaguzi iliendesha zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kuanzia tarehe 23 Februari hadi tarehe 04 Agosti, 2015 katika mikoa yote ya Tanzania kwa awamu. Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ulianza mara baada ya kupokea BVR *Kits* **250** ambazo zilitumika katika Halmashauri ya Mji wa Makambako katika Mkoa wa Njombe.

Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ulifanyika kwa kuandikisha Wapiga Kura wote waliotimiza umri wa miaka **18** ikiwemo wale waliowahi kuandikishwa awali na wale ambao walitarajiwa kutimiza umri wa miaka **18** ifikapo siku ya Uchaguzi, yaani tarehe 25 Oktoba, 2015.



*Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete (Kushoto) akichukuliwa alama za vidole wakati akiandikishwa kuwa Mpiga Kura katika Kijiji cha Msoga, Wilaya ya Bagamoyo, Mkoa wa Pwani.*

## 3.4 Uwekaji Wazi Daftari la Awali la Wapiga Kura

Kwa mujibu wa Kifungu cha 22(2) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilipanga muda wa siku 5 za Uwekaji Wazi wa Daftari la Awali la Wapiga Kura katika Makao Makuu ya Kata. Mpiga Kura aliweza kukagua usahihi wa taarifa zilizomo kwenye Daftari na kufanya marekebisho kwa namna ambavyo ilielekezwa na Tume. Aidha, Uwekaji Wazi wa Daftari uliwapa wananchi waliojiandikisha fursa ya kuweka pingamizi kwa wale wasio na sifa za kuwepo kwenye Daftari hilo.

Katika kuwarahisishia wananchi kuhakiki taarifa zao Tume pia, iliweka utaratibu wa kuwawezesha Wapiga Kura kuhakiki taarifa zao. Utaratibu uliotumika ni pamoja na matumizi ya simu za Kiganjani, ambapo Mpiga Kura alipaswa kubofya namba ***152*00#** na kufuata maelekezo.

Njia nyingine ni matumizi ya Tovuti ya Tume (www.nec.go.tz) na kupiga simu moja kwa moja katika Kituo cha Mawasiliano cha Tume.

Ratiba ya Uwekaji Wazi Daftari ilizingatia mikoa ambayo tayari ilikuwa imekamilisha Uandikishaji. Zoezi la Uwekaji Wazi Daftari lilianza tarehe 7 Agosti, 2015, na kukamilika mnamo tarehe 19 Agosti, 2015. Ratiba hiyo ilikuwa kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 12.**

**Jedwali Na. 12: Ratiba ya Uwekaji Wazi Daftari la Awali la Wapiga Kura**

| Na. | Mikoa | Tarehe |
|---|---|---|
| 1. | Njombe, Lindi, Mtwara, Iringa, Ruvuma, Katavi, Rukwa, Mbeya, Dodoma, Singida, Tabora, Kigoma, Kagera, Simiyu, Shinyanga, Geita, Mwanza, Mara, Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Tanga na Morogoro | 7 hadi 11Agosti, 2015 |
| 2. | Pwani | 12 hadi 16 Agosti, 2015 |
| 3 | Dar es Salaam na Zanzibar | 15 hadi 19 Agosti, 2015 |

### 3.4.1 Matokeo ya Zoezi la Uwekaji Wazi Daftari la Awali la Wapiga Kura

Baada ya zoezi la Uwekaji Wazi wa Daftari la Awali, dosari kadhaa zilibainika kama ifuatavyo:-

(i) Baadhi ya waliojiandikisha hawakuwa na sifa za Mpiga Kura;

(ii) Uwepo wa makosa katika majina ya waliojiandikisha;

(iii) Wapiga Kura waliojiandikisha katika Kata/Halmashauri moja kukuta majina yao yapo kwenye Kata/Halmashauri nyingine kutokana na mabadiliko ya Mipaka ya Kiutawala. Hii ilitokea kwenye Kata/ Halmashauri ambazo Mipaka ya Kiutawala ilibadilika baada ya Uandikishaji; na

(iv) Baadhi ya Wapiga Kura waligundulika kuwa wamejiandikisha zaidi ya mara moja.

Katika Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, Tume ilikadiria kuandikisha Wapiga Kura **23,491,471.** Hata hivyo, baada ya zoezi la Uboreshaji kukamilika, Tume ilifanikiwa kuandikisha idadi ya Wapiga Kura **22,658,247** kwa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar ambayo ni sawa na asilimia **94.8.** Aidha, kwa Upande wa Tanzania Zanzibar, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) iliandikisha Wapiga Kura **503,193** idadi ambayo inafanya jumla ya Wapiga Kura kuwa **23,161,440** sawa na asilimia **96.9** kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 13.**

**Jedwali Na. 13: Idadi ya Wapiga Kura waliokadiriwa na walioandikishwa**

| Na. | Mkoa | Makadirio ya Wapiga Kura waliotarajiwa kuandikishwa, mwaka, 2015 | Idadi ya Wapiga Kura Walioandikishwa, mwaka, 2015 | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Arusha | 948,737 | 1,002,023 | 105.6 |
| 2. | Dar Es Salaam | 2,936,938 | 2,802,956 | 95.4 |
| 3. | Dodoma | 1,099,326 | 1,064,999 | 96.9 |
| 4. | Geita | 812,345 | 883,181 | 108.7 |
| 5. | Iringa | 528,398 | 525,734 | 99.5 |
| 6. | Kagera | 1,221,396 | 1,046,710 | 85.7 |
| 7. | Katavi | 275,168 | 321,885 | 117.0 |
| 8. | Kigoma | 1,036,169 | 789,828 | 76.2 |
| 9. | Kilimanjaro | 980,011 | 797,885 | 81.4 |
| 10. | Lindi | 522,238 | 509,926 | 97.6 |
| 11. | Manyara | 748,579 | 670,922 | 89.6 |
| 12. | Mara | 838,588 | 888,418 | 105.9 |
| 13. | Mbeya | 1,481,373 | 1,391,306 | 93.9 |
| 14. | Morogoro | 1,268,837 | 1,256,582 | 99.0 |
| 15. | Mtwara | 777,297 | 723,847 | 93.1 |
| 16. | Mwanza | 1,407,751 | 1,442,441 | 102.5 |
| 17. | Njombe | 396,642 | 379,340 | 95.6 |
| 18. | Pwani | 648,848 | 694,892 | 107.1 |
| 19. | Rukwa | 476,804 | 460,207 | 96.5 |
| 20. | Ruvuma | 787,304 | 734,842 | 93.3 |
| 21. | Shinyanga | 766,325 | 768,647 | 100.3 |
| 22. | Simiyu | 718,765 | 713,230 | 99.2 |
| 23. | Singida | 702,918 | 644,529 | 91.7 |
| 24. | Tabora | 1,128,175 | 1,092,023 | 96.8 |
| 25. | Tanga | 1,082,294 | 1,002,420 | 92.6 |
| 26. | Kaskazini Pemba | 41,955 | 11,529 | 27.5 |
| 27. | Kaskazini Unguja | 42,483 | 9,567 | 22.5 |
| 28. | Kusini Pemba | 37,772 | 9,268 | 24.5 |
| 29. | Kusini Unguja | 24,773 | 5,413 | 21.9 |
| 30. | Mjini Magharibi | 163,262 | 13,697 | 8.4 |
| **Jumla ndogo** | | **23,901,471** | **22,658,247** | **94.8** |
| | Wapiga Kura walioandikishwa na ZEC | | 503,193 | |
| **JUMLA KUU** | | | **23,161,440** | **96.9** |

**Ramani Na. 3: Asilimia ya Wapiga Kura Walioandikishwa Kimkoa**



### 3.4.2 Uchapishaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na Orodha ya Wapiga Kura

Baada ya zoezi la Uwekaji Wazi wa Daftari la Awali kukamilika na marekebisho ya taarifa za Wapiga Kura kufanyika, Daftari la Kudumu la Wapiga Kura pamoja na Orodha ya Wapiga Kura kwa kila Kituo vilichapishwa. Uchapishaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na Orodha ya Wapiga Kura ulifanyika baada ya ugawaji wa Wapiga Kura katika Vituo vya Kupigia Kura ambapo kila Kituo kilitakiwa kuwa na Wapiga Kura wasiozidi **500.**

Daftari la Kudumu la Wapiga Kura lilichapishwa na kukamilika tarehe 14 Oktoba, 2015. Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilichapisha nakala moja ya Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na nakala mbili za Orodha ya Wapiga Kura. Nakala moja ya Orodha ilitumika kwa ajili ya kubandika Kituoni siku **8** kabla ya Siku ya Uchaguzi kama Sheria za Uchaguzi zinavyoelekeza. Nakala ya pili ya Orodha ya Wapiga Kura ilitumiwa na Karani Mwongozaji Siku ya Uchaguzi Mkuu. Aidha, Vyama vya Siasa vilipewa nakala tete *(soft copy)* ya Daftari la Kudumu la Wapiga Kura la nchi nzima.

## 3.5 Mafanikio ya Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura

Pamoja na changamoto kadhaa ambazo Tume ilikutana nazo katika zoezi la Uboreshaji ikiwemo idadi ndogo ya BVR *Kits,* idadi kubwa ya Wapiga Kura na muda mfupi wa kuandikisha Wapiga Kura, Tume ilikamilisha zoezi hili kwa mafanikio makubwa.

## SURA YA NNE

## UTEUZI WA WAGOMBEA NA KAMPENI ZA UCHAGUZI

### 4.1 Uteuzi wa Wagombea

Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilitangaza tarehe 21 Agosti, 2015, kuwa Siku ya Uteuzi wa Wagombea wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. Wagombea wote waliopendekezwa na Vyama walitakiwa kuwasilisha Fomu za Uteuzi katika Ofisi za Tume kabla ya saa kumi kamili (10:00) jioni, siku hiyo ya Uteuzi.

### 4.2 Uteuzi wa Wagombea wa Nafasi ya Kiti cha Rais na Makamu wa Rais

Kwa Mujibu wa Kifungu cha 30 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, Uteuzi wa Wagombea wa nafasi ya Kiti cha Rais na Makamu wa Rais unafanywa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Fomu za Uteuzi wa Wagombea Urais Na. 8A na Fomu ya Maadili Na. 10 zilipangwa zitolewa kuanzia tarehe 1 hadi 21 Agosti, 2015.

Jumla ya Wagombea 11 walichukua Fomu. Wagombea hao ni kutoka Vyama vya Alliance for Change and Transparency (ACT-Wazalendo), Alliance for Democratic Change (ADC), The African Democratic Alliance - Tanzania Democratic Alliance (ADA-TADEA), Chama Cha Kijamii (CCK), Chama Cha Mapinduzi (CCM), Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Chama Cha Ukombozi wa Umma ( CHAUMMA), Democratic Party (DP), National Reconstruction Alliance (NRA), Tanzania Labour Party (TLP) na United People's Democratic Party (UPDP).



*Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Mhe. Jaji (Mst) Damian Z. Lubuva (Kulia), akipokea Fomu za Uteuzi kutoka kwa Mgombea wa Kiti cha Rais kwa tiketi ya CCM, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, katikati ni Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Mhe. Jaji Mkuu (Mst-Z) Hamid M. Hamid.*



*Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Mhe. Jaji (Mst) Damian Z. Lubuva (Kulia), akipokea Fomu za Uteuzi kutoka kwa Mgombea wa Kiti cha Rais kwa tiketi ya ACT – Wazalendo, Bi. Anna Elisha Mghwira, kushoto ni Mgembea mwenza wa Urais Mhe. Hamad Mussa Yussuf na kwa mbali ni Bi. Clothilde Komba Mkuu wa Idara ya Uchaguzi, Tume.*



*Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Mhe. Jaji Mstaafu Damian Z. Lubuva (Kulia) akipokea Fomu za Uteuzi kutoka kwa Mgombea wa Kiti cha Rais kwa tiketi ya CHADEMA Ndugu Edward Ngoyai Lowassa, katikati ni Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Mhe. Jaji Mkuu (Mst-Z) Hamid M. Hamid.*

Fomu za Uteuzi wa Wagombea zilirejeshwa tarehe 21 Agosti, 2015, kuanzia saa 1:30 asubuhi hadi saa 10:00 jioni katika Ofisi za Tume. Aidha, Tume ilitoa nafasi kwa Wagombea kuwasilisha Fomu zao siku tatu kabla ya Siku ya Uteuzi kwa

Mkurugenzi wa Uchaguzi kwa ajili ya kukaguliwa na kuona kama zimekidhi vigezo na masharti yaliyowekwa kwa mujibu wa sheria. Hii ilikuwa ni kutoa nafasi kwa Wagombea kuhakikiwa Fomu zao ili kama zina dosari wapate fursa ya kurekebisha kabla ya Siku ya Uteuzi.

Kati ya wagombea wote 11 waliochukua Fomu za Uteuzi, ni wagombea 8 tu ndio waliorudisha Fomu zao. Nao ni kutoka Vyama vya ACT-Wazalendo, CCM, ADC, CHADEMA, CHAUMMA, NRA, TLP na UPDP na ndiyo waliokidhi masharti ya Uteuzi kwa mujibu wa Ibara ya 39(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Mwenyekiti wa Tume aliwatangaza rasmi kuwa wagombea walioteuliwa kugombea nafasi ya kiti cha Rais katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2015. Aidha, wagombea kutoka vyama viwili vya CCK na ADA - TADEA hawakurudisha Fomu zao. Mgombea wa Chama cha DP alirejesha Fomu yake baada ya muda wa uteuzi kuwa umepita. Orodha ya wagombea wa nafasi ya Kiti cha Rais ni kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 14.**

**Jedwali Na. 14: Majina ya Wagombea wa Nafasi ya Kiti cha Rais na Makamu wa Rais**

| Na. | Jina la Mgombea | Jinsi | Chama Cha Siasa |
|---|---|---|---|
| 1. | Anna Elisha Mghwira | KE | ACT-Wazalendo |
| | **Mgombea Mwenza:** Hamad Mussa Yussuf | ME | |
| 2. | Chief Lutalosa Yemba | ME | ADC |
| | **Mgombea Mwenza:** Said Miraj Abdallah | ME | |
| 3. | Dkt. John Pombe Magufuli | ME | CCM |
| | **Mgombea Mwenza:** Samia Suluhu Hassan | KE | |
| 4. | Edward Ngoyai Lowassa | ME | CHADEMA |
| | **Mgombea Mwenza** Duni Juma Haji | ME | |
| 5. | Hashim Rungwe Spunda | ME | CHAUMMA |
| | **Mgombea Mwenza:** Issa Abas Hussein | ME | |
| 6. | Lyimo Macmillan Elifatio | ME | TLP |
| | **Mgombea Mwenza:** Hussein Juma Salum | ME | |
| 7. | Kasambala Janken Malik | ME | NRA |
| | **Mgombea Mwenza:** Simai Abdulrahman Abdul | ME | |
| 8. | Dovutwa Fahmi Nassoro | ME | UPDP |
| | **Mgombea Mwenza:** Hamadi Mohamed Ibrahim | ME | |

### 4.2.1 Pingamizi kwa Wagombea wa Nafasi ya Kiti cha Rais

Kifungu cha 40 (1) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, kinatoa nafasi ya kuweka pingamizi kwa wagombea walioteuliwa kugombea nafasi ya Kiti cha Rais ndani ya saa **24** baada ya muda wa uteuzi kumalizika. Hata hivyo, hapakuwa na pingamizi lolote lililowekwa kwa wagombea wa nafasi ya Kiti cha Rais.

## 4.3 Uteuzi wa Wagombea Ubunge

Fomu Na. 8B za Uteuzi wa wagombea Ubunge na Fomu Na. 10 za Maadili ya Uchaguzi zilitolewa na Wasimamizi wa Uchaguzi kuanzia tarehe 8 hadi 21 Agosti 2015.

Katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, jumla ya Wagombea **1,209** waliteuliwa kuwania nafasi ya Ubunge. Kati yao wanaume ni **976** sawa na asilimia **81** na wanawake ni **233** sawa na asilimia **19** kama ilivyoainishwa kwenye **Jedwali Na. 15, Chati Na. 1** na **Chati Na. 2.**

**Jedwali Na. 15: Wagombea Ubunge kwa Jinsi na kwa Chama**

| Na. | Chama cha Siasa | Idadi ya Wagombea | Asilimia kulingana na Idadi ya Viti vya Ubunge | Idadi kwa Jinsi | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | ME | KE |
| 1. | ACT-Wazalendo | 203 | 76.9 | 173 | 30 |
| 2. | ADA – TADEA | 17 | 6.4 | 15 | 2 |
| 3. | ADC | 61 | 23.1 | 45 | 16 |
| 4. | AFP | 27 | 10.2 | 19 | 8 |
| 5. | APPT - Maendeleo | 14 | 5.3 | 7 | 7 |
| 6. | CCK | 11 | 4.2 | 7 | 4 |
| 7. | CCM | 264 | 100.0 | 240 | 24 |
| 8. | CHADEMA | 184 | 69.7 | 171 | 13 |
| 9. | CHAUMMA | 23 | 8.7 | 14 | 9 |
| 10. | CHAUSTA | 19 | 7.2 | 7 | 12 |
| 11. | CUF | 135 | 51.1 | 120 | 15 |
| 12. | DEMOKRASIA MAKINI | 13 | 14.0 | 8 | 5 |
| 13. | DP | 37 | 8.0 | 27 | 10 |
| 14. | JAHAZI ASILIA | 21 | 4.9 | 17 | 4 |
| 15. | NCCR-Mageuzi | 27 | 10.2 | 21 | 6 |
| 16. | NLD | 4 | 1.5 | 3 | 1 |
| 17. | NRA | 17 | 6.4 | 16 | 1 |
| 18. | SAU | 8 | 3.0 | 7 | 1 |
| 19. | TLP | 29 | 11.0 | 18 | 11 |
| 20. | UDP | 25 | 9.5 | 15 | 10 |
| 21. | UMD | 29 | 11.0 | 12 | 17 |
| 22. | UPDP | 41 | 15.5 | 14 | 27 |
| **Jumla** | | **1,209** | | **976** | **233** |

**Chati Na. 1: Wagombea Ubunge kwa kila Chama kulingana na Viti vya Ubunge**




**Chati Na. 2: Wagombea Ubunge kwa jinsi**



#### 4.3.1 Pingamizi dhidi ya Uteuzi wa Wagombea Ubunge

Kifungu cha 40 (1) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, kinatoa fursa ya kuweka pingamizi za Uteuzi katika nafasi ya Ubunge. Pingamizi hizi hupokelewa, husikilizwa na kuamuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi. Jumla ya pingamizi **158** za Ubunge zilipokelewa na kusikilizwa na Wasimamizi wa Uchaguzi. Aidha, iwapo mlalamikaji au mlalamikiwa hakuridhika na uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi alipata nafasi ya kukata Rufaa Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

#### 4.3.2 Rufaa kwa Tume

Kifungu cha 40 (6) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, kinawaruhusu Wagombea kukata Rufaa Tume ya Taifa ya Uchaguzi kupinga Uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi kuhusu pingamizi dhidi ya Mgombea.

Tume ilipokea jumla ya Rufaa **57** kutoka katika Majimbo mbalimbali kupinga Uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi. Rufaa **36** zilitaka Wagombea kuenguliwa na Rufaa **17** zilitaka Wagombea waendelee kuwa Wagombea. Rufaa 4 hazikuamuliwa kwa kuwa hazikutimiza masharti ya Kisheria. Mchanganuo wa Rufaa zilizopokelewa na Maamuzi ya Tume umeoneshwa katika **Jedwali Na. 16.**

**Jedwali Na. 16: Mchanganuo wa Rufaa za Ubunge**

| Na. | Jina la Chama/Msimamizi wa Uchaguzi | Idadi ya Rufaa Zilizowasilishwa | Idadi ya Wagombea ambao Waliondolewa | Idadi ya Wagombea Waliorejeshwa |
|---|---|---|---|---|
| 1. | ACT-Wazalendo | 6 | 0 | 3 |
| 2. | ADA-TADEA | 1 | 0 | 1 |
| 3. | CCM | 11 | 0 | 0 |
| 4. | CHADEMA | 17 | 0 | 7 |
| 5. | CHAUMA | 1 | 1 | 0 |
| 6. | CUF | 10 | 0 | 2 |
| 7. | DP | 2 | 0 | 0 |
| 8. | NCCR-Mageuzi | 3 | 0 | 0 |
| 9. | SAU | 1 | 0 | 1 |
| 10. | UDP | 1 | 0 | 0 |
| 11. | UPDP | 1 | 1 | 0 |
| 12. | Rufaa dhidi ya Msimamizi wa Uchaguzi | 3 | 0 | 0 |
| **Jumla** | | **57** | **2** | **14** |

#### 4.3.3 Mgombea Aliyepita Bila Kupingwa

Kwa mujibu wa Kifungu cha 44 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, ambacho kinaainisha, endapo Mgombea aliyeteuliwa ni mmoja tu, Mgombea huyo atatangazwa kwenye Gazeti la Serikali kuwa amepita bila kupingwa na Uchaguzi hautafanyika katika Jimbo hilo. Katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, ni **Ndugu Abdallah Chikota,** Mgombea wa Chama cha Mapinduzi Jimbo la Nanyamba pekee, ndiye aliyepita bila kupingwa.

### 4.4 Uteuzi wa Wagombea Udiwani

Uteuzi wa Wagombea Udiwani ulifanyika katika ngazi ya Kata na Wasimamizi Wasaidizi ngazi ya Kata walihusika na Uteuzi huo. Uteuzi huo ulifanyika katika Kata **3,946** ambapo jumla ya Wagombea **10,716** waliteuliwa kuwania nafasi ya Viti vya Udiwani. Kati yao wagombea **10,046** walikuwa wanaume, sawa na asilimia **94** na wagombea **670** walikuwa wanawake, sawa na asilimia **6.** Rejea **Jedwali Na. 17, Chati Na.3 na Chati Na. 4** kwa ufafanuzi zaidi.

**Jedwali Na. 17: Wagombea kwa nafasi ya Udiwani kwa Jinsi na kwa Chama**

| Na. | Jina la Chama | Wagombea | Asilimia kulingana viti vya Udiwani | Wagombea kwa Jinsi | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | ME | KE |
| 1. | ACT- Wazalendo | 1,359 | 34.44 | 1,309 | 50 |
| 2. | ADA - TADEA | 37 | 0.94 | 30 | 7 |
| 3. | ADC | 97 | 2.46 | 86 | 11 |
| 4. | AFP | 22 | 0.56 | 17 | 5 |
| 5. | APPT - Maendeleo | 26 | 0.66 | 15 | 11 |
| 6. | CCK | 12 | 0.30 | 5 | 7 |
| 7. | CCM | 3,946 | 100.00 | 3,682 | 264 |
| 8. | CHADEMA | 3,335 | 84.52 | 3,228 | 107 |
| 9. | CHAUMMA | 27 | 0.68 | 24 | 3 |
| 10. | CHAUSTA | 15 | 0.38 | 7 | 8 |
| 11. | CUF | 1,111 | 28.16 | 1,060 | 51 |
| 12. | DEMOKRASIA MAKINI | 20 | 1.19 | 11 | 9 |
| 13. | DP | 47 | 1.01 | 42 | 5 |
| 14. | JAHAZI ASILIA | 40 | 0.51 | 13 | 27 |
| 15. | NCCR-Mageuzi | 254 | 6.44 | 245 | 9 |
| 16. | NLD | 23 | 0.58 | 17 | 6 |
| 17. | NRA | 19 | 0.48 | 18 | 1 |
| 18. | SAU | 24 | 0.61 | 17 | 7 |
| 19. | TLP | 95 | 2.41 | 82 | 13 |
| 20. | UDP | 95 | 2.41 | 87 | 8 |
| 21. | UMD | 61 | 1.55 | 20 | 41 |
| 22. | UPDP | 51 | 1.29 | 31 | 20 |
| | **JUMLA** | **10,716** | | **10,046** | **670** |

**Chati Na. 3: Wagombea Udiwani kwa kila Chama Kulingana na Viti vya Udiwani**




**Chati Na. 4: Wagombea Udiwani kwa Jinsi**



### 4.4.1 Pingamizi Dhidi ya Uteuzi wa Wagombea Udiwani

Kifungu cha **44(1 - 4), (4A) na (4B)** cha Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Sura ya 292, kinatoa fursa ya kuweka pingamizi kupinga Uteuzi wa Mgombea. Pingamizi hizi hupokelewa, husikilizwa na kuamuliwa na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi. Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya Kata baada ya kupokea pingamizi na kufanya uamuzi anatakiwa amfahamishe Msimamizi wa Uchaguzi juu ya uamuzi huo ili aupitie na kuona kama umezingatia Sheria. Msimamizi wa Uchaguzi ana mamlaka ya kubadili uamuzi huo kama itabainika kuwa haukuzingatia matakwa ya kisheria.

Katika Uchaguzi wa mwaka 2015, jumla ya pingamizi **428** za Udiwani ziliwasilishwa na kufanyiwa maamuzi katika ngazi ya Kata.

### 4.4.2 Rufaa Dhidi ya Wagombea Udiwani

Kifungu cha 44 (5) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, kinaruhusu Wagombea kukata Rufaa Tume ya Taifa ya Uchaguzi kupinga uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi kuhusu pingamizi dhidi ya Mgombea.

Tume ilipokea jumla ya rufaa za wagombea Udiwani **223** kutoka katika Kata mbalimbali kupinga uamuzi wa Wasimamizi wa Uchaguzi. Kati ya hizo, rufaa **175** zilizowasilishwa zilitaka kuenguliwa kwa wagombea na rufaa **45** zilitaka kurejeshwa kwa wagombea waliokuwa wameenguliwa. Aidha, rufaa **3** ziliwasilishwa kama malalamiko, hivyo hazikufanyiwa kazi kwa kutotimiza matakwa ya kisheria. Katika rufaa **175** zilizotaka wagombea kuenguliwa, wagombea **11** walienguliwa na **164** waliendelea kugombea. Kwa upande wa rufaa zilizotaka wagombea kurejeshwa, wagombea **39** walirejeshwa na wagombea **6** walikataliwa. Rejea **Jedwali Na. 18 na Jedwali Na. 19.**

**Jedwali Na. 18: Mchanganuo wa Rufaa za Wagombea Nafasi ya Udiwani**

| Na. | Jina la Chama/Wasimamizi wa Uchaguzi | Idadi ya Rufaa |
|---|---|---|
| 1. | ACT-Wazalendo | 11 |
| 2. | ADA-TADEA | 1 |
| 3. | ADC | 1 |
| 4. | CCM | 83 |
| 5. | CHADEMA | 87 |
| 6. | CUF | 22 |
| 7. | JAHAZI ASILIA | 1 |
| 8. | NCCR-Mageuzi | 3 |
| 9. | NLD | 5 |
| 10. | Rufaa dhidi ya maamuzi ya Wasimamizi wa Uchaguzi | 6 |
| 11. | Malalamiko yaliyowasilishwa kama Rufaa | 3 |
| **Jumla** | | **223** |

**Jedwali Na. 19: Wagombea Waliorejeshwa na Walioondolewa Baada ya Uamuzi wa Tume**

| Na. | Jina la Chama | Idadi ya Wagombea Waliorejeshwa | Idadi ya Wagombea Walioondolewa |
|---|---|---|---|
| 1. | ACT- Wazalendo | 1 | 0 |
| 2. | ADA-TADEA | - | 1 |
| 3. | ADC | 1 | 0 |
| 4. | CCM | 1 | 0 |
| 5. | CHADEMA | 29 | 9 |
| 6. | CUF | 6 | 0 |
| 7. | JAHAZI ASILIA | 1 | 0 |
| 8. | NCCR-Mageuzi | - | 1 |
| 9. | NLD | - | 0 |
| **Jumla** | | **39** | **11** |

Pingamizi na/au Rufaa zilizopokelewa kwa Kiti cha Rais, Ubunge na Udiwani kwa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015 ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 20.**

**Jedwali Na. 20: Muhtasari wa Idadi ya Wagombea, Pingamizi na Rufaa katika Uchaguzi wa Mwaka 2015**

| Na. | Nafasi Inayogombewa | Idadi ya Nafasi zinazogombewa | Idadi ya Wagombea | Idadi ya Pingamizi | Idadi ya Rufaa |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Urais | 1 | 8 | 0 | 0 |
| 2. | Ubunge | 264 | 1,209 | 158 | 57 |
| 3. | Udiwani | 3,946 | 10,716 | 428 | 223 |

### 4.4.3 Wagombea wa Nafasi ya Udiwani Waliopita Bila Kupingwa

Katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015, jumla ya Wagombea **71** walipita bila kupingwa. Wagombea hao wote walitoka Chama Cha Mapinduzi. Hivyo, Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi katika Kata hizo waliwatangaza washindi kwa kuzingatia Kifungu cha 45(2) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292. Kata ambazo Wagombea walipita bila kupingwa zinaoneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 3.**

## 4.5 Mfumo wa Menejimenti ya Wagombea

Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilitumia Mfumo wa kielektroniki wa kuchukua na kuhifadhi taarifa za Wagombea (*Candidates Management System*-**CMS**). Mfumo huu ulitumika kuchukua na kuhifadhi taarifa za wagombea wote wa ngazi ya Urais, Ubunge pamoja na Udiwani. Tofauti na ilivyokuwa awali ambapo Fomu zote za Uteuzi zililetwa Makao Makuu ya Tume kwa ajili ya uchakataji. Kwa ngazi ya Urais

wagombea walisajiliwa katika Ofisi za Tume Makao Makuu na wagombea wa ngazi za Udiwani na Ubunge walisajiliwa katika Halmashauri husika. Vifaa vyote vinavyohusiana na Mfumo vilisambazwa katika Halmashauri zote kwa ajili ya utekelezaji wa Usajili wa Wagombea. Aidha, Wataalam kutoka Tume walifika katika Halmashauri zote ili kusajili Wagombea.

Mfumo wa Menejimenti ya Wagombea uliiwezesha Tume kuchukua Taarifa za Wagombea wote kwa muda mfupi na kurahisisha maandalizi ya Karatasi za Kura kufanyika kwa wakati.

### 4.6 Kampeni za Uchaguzi

Katika hali ya kawaida, Kampeni za Uchaguzi huendeshwa na Mgombea. Hata hivyo, Mawakala na Vyama vya Siasa wanaweza kuendesha Kampeni za Uchaguzi kwa niaba ya Wagombea endapo watakubaliana na Wagombea. Kampeni za Uchaguzi zilifanyika kwa njia ya mikuatano ya hadhara, kampeni za nyumba kwa nyumba, matangazo kupitia Vyombo vya Habari na kwa njia ya mabango.

#### 4.6.1 Ratiba za Kampeni

Kipindi cha Kampeni huanza siku moja baada ya Siku ya Uteuzi wa Wagombea na kumalizika siku moja kabla ya Siku ya Uchaguzi. Kwa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, Tume ilitangaza Kipindi cha Kampeni kuanzia tarehe 22 Agosti, 2015 hadi tarehe 24 Oktoba, 2015.

Kwa kuzingatia Kanuni za 40 - 43 ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2015, na Kanuni za 35 - 37 ya Kanuni za Uchaguzi wa Madiwani za mwaka 2015, Vyama vya Siasa vyenye wagombea wa nafasi mbalimbali vilipendekeza Ratiba za Kampeni na kuziwasilisha Tume kwa ajili ya uratibu wakati wote wa Kipindi cha Kampeni.

Kwa ngazi ya Urais Ratiba ziliwasilishwa kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi, kwa ngazi ya Ubunge ziliwasilishwa kwa Msimamizi wa Uchaguzi na kwa ngazi ya Udiwani ziliwasilishwa kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya Kata.

##### 4.6.1.1 Uratibu wa Kampeni za Nafasi ya Kiti cha Rais

Tume iliunda Kamati ya Kuratibu Ratiba ya Mikutano ya Kampeni za wagombea Urais. Kamati hiyo iliyohusisha wawakilishi kutoka katika kila Chama cha Siasa ambacho kilisimamisha Mgombea katika nafasi ya Rais. Kamati hiyo ilipitia na kujadili mapendekezo ya Ratiba za Mikutano ya Kampeni kutoka Vyama **8** vya Siasa vilivyoshiriki Uchaguzi ngazi ya Rais.

Kamati ilikubaliana kukutana Jumanne ya kila Wiki na ililazimika kukutana kwa dharura pale ambapo palijitokeza ulazima wa Chama kufanya mabadiliko ya Ratiba kabla ya muda wa kikao uliopangwa kufika. Tume ilisambaza nakala ya Ratiba iliyoratibiwa kwa Waratibu wote Uchaguzi wa Mikoa nchini ambao walikuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa inawafikia Wasimamizi, Wasimamizi Wasaidizi wa

Uchaguzi. Aidha, ilimpatia nakala kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi ambaye alikuwa anawapatia Makamanda wote wa Polisi wa Mikoa na Wilaya nakala ya Ratiba hiyo kwa ajili ya kuratibu ulinzi na usalama katika mikutano ya kampeni.

#### 4.6.1.2 Uratibu wa Kampeni za Ubunge na Udiwani

Vyama vya Siasa vyenye Wagombea katika maeneo husika viliwasilisha mapendekezo ya Ratiba za Kampeni kwa Msimamizi wa Uchaguzi siku **7** kabla ya Siku ya Uteuzi. Vyama ambavyo vilihitaji kufanya mabadiliko ya tarehe au maeneo ya kufanyia Kampeni, vilitoa taarifa kwa Wasimamizi wa Uchaguzi au Wasimamizi wasaidizi ambao waliitisha Mikutano na Vyama vyote vya Siasa vilivyoshiriki Uchaguzi, ili kukubaliana juu ya mabadiliko hayo. Baada ya kukubaliana na Ratiba, nakala ya Ratiba iliyokubaliwa ilipelekwa kwa Mkuu wa Wilaya kwa taarifa na Kamanda wa Polisi wa Wilaya ili watoe ulinzi katika mikutano ya kampeni.

## 4.7 Mambo Yaliyozingatiwa Wakati wa Kampeni

Katika kuhakikisha kunakuwa na usawa kwenye Mikutano ya Kampeni miongoni mwa Vyama vya Siasa, Wagombea walipaswa kuzingatia Sheria ya Gharama za Uchaguzi Na. 6 ya mwaka 2010 na Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Ubunge na Madiwani ya mwaka 2015.

### 4.7.1 Sheria ya Gharama za Uchaguzi Na. 6 ya Mwaka 2010

Sheria ya Gharama za Uchaguzi pamoja na mambo mengine imelenga kudhibiti matumizi mabaya ya fedha katika shughuli za Uchaguzi. Sheria inahitaji uwepo wa uwazi wa vyanzo vya mapato, matumizi, michango pamoja na kiwango cha mwisho cha fedha zinazotumika katika Uchaguzi ili kudhibiti vitendo vya rushwa ndani ya Vyama vya Siasa na Uchaguzi kwa ujumla. Utekelezaji wa Sheria hii unasimamiwa na Msajili wa Vyama vya Siasa.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 20(1-4) cha Sheria ya Gharama za Uchaguzi, Msajili wa Vyama vya Siasa anaweza kumwekea pingamizi Mgombea yeyote au Chama cha Siasa kilicho kiuka Sheria hiyo kwa Tume. Hata hivyo, katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, Tume haikupokea pingamizi lolote kutoka kwa Msajili wa Vyama vya Siasa.

### 4.7.2 Maadili ya Uchaguzi

Tume ya Taifa ya Uchaguzi iliandaa Maadili ya Uchaguzi ya mwaka 2015 kama ilivyoainishwa katika Kifungu cha 124A cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura 343. Lengo la Maadili hayo ni kuweka usawa katika uwanja wa ushindani na kuwawezesha wananchi kupata nafasi ya kusikiliza Sera za Wagombea wa Vyama vya Siasa wakati wote wa Kampeni za Uchaguzi.

#### 4.7.2.1 Kamati za Maadili ya Uchaguzi

Kwa mujibu wa Sehemu ya Tano ya Maadili ya Uchaguzi ya mwaka 2015, ziliundwa Kamati ngazi ya Kata, Jimbo, Taifa na Rufaa ili, kusimamia na kutekeleza Maadili ya Uchaguzi katika ngazi hizo. Kamati zilizoundwa ni kama inavyooneshwa kwenye

**Jedwali Na. 21.**

**Jedwali Na. 21: Kamati za Maadili Zilizoundwa katika Ngazi mbalimbali**

| Na. | Kamati | Idadi |
|---|---|---|
| 1. | Kamati ya Rufaa | 1 |
| 2. | Kamati ngazi ya Taifa | 1 |
| 3. | Kamati ngazi ya Jimbo | 254* |
| 4. | Kamati ngazi ya Kata | 3,946 |

*Kamati za Maadili ngazi ya Jimbo zilikuwa **254** badala ya **264** kutokana baadhi ya Halmashauri kuwa na Jimbo zaidi ya moja.

#### 4.7.2.2 Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Kamati za Maadili ya Uchaguzi

Tume ya Taifa ya Uchaguzi ndiyo yenye jukumu la kusimamia utekelezaji wa Maadili ya Uchaguzi. Katika kutekeleza jukumu hili, Watendaji wa Tume walifanya ufuatiliaji katika Majimbo na Kata zote kuangalia namna ambavyo Kamati zilivyokuwa zinafanya kazi.

Katika kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Maadili ya Uchaguzi, Tume ilibaini ukiukwaji wa Maadili ya Uchaguzi kwa baadhi ya maeneo kama vile: -

(i) Lugha za kashfa na matusi zilizotolewa na wagombea na viongozi wa Vyama vya Siasa wakati wa Kampeni;

(ii) Kuzidisha muda wa Kampeni;

(iii) Ukiukwaji wa Ratiba ya Kampeni;

(iv) Maandamano ya wafuasi wa Vyama vya Siasa yasiyokuwa na Kibali kabla na baada ya Kampeni;

(v) Wafuasi wa Vyama kuharibu mabango ya Wagombea wa Vyama vingine;

(vi) Baadhi ya Watendaji wa Serikali kuingilia shughuli za Vyama vya Siasa;

(vii) Vurugu dhidi ya Vyama na Wagombea katika baadhi ya maeneo;

(viii) Kubandika picha za Wagombea juu ya picha za Wagombea wa Vyama vingine;

(ix) Wafuasi wa Vyama na Wagombea kuingilia Mikutano ya Wagombea wa Vyama vingine; na

(x) Kutoa kauli zisizoweza kuthibitishwa.

Kutokana na vitendo vya ukiukwaji wa Maadili vilivyojitokeza, Kamati za Maadili zilichukua hatua mbalimbali ikiwemo kutoa karipio, kuwaelekeza Wagombea/Vyama kuomba msamaha na kumsimamisha Mgombea mmoja kutofanya Kampeni.

Pamoja na changamoto zilizojitokeza, uwepo wa Kamati za Maadili ulifanikisha kuwepo kwa amani na utulivu katika Mikutano ya Kampeni za Uchaguzi. Kamati hizo zilitumika kumaliza tofauti na migogoro miongoni mwa Vyama na Wagombea. Aidha, Kamati zilipelekea kuimarika kwa mahusiano kati ya Tume, Serikali, Vyama vya Siasa na Wagombea wakati wote wa Kampeni za Uchaguzi.

## SURA YA TANO

## KUPIGA NA KUHESABU KURA

### 5.1 Siku ya Uchaguzi

Siku ya Kupiga Kura kwa ajili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Madiwani kwa Tanzania Bara ilikuwa ni tarehe 25 Oktoba, 2015. Upigaji Kura ulihusisha Wapiga Kura walioandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.



*Mpiga Kura akipiga Kura Siku ya Uchaguzi Mkuu, tarehe Oktoba 25, 2015.*

#### 5.1.1 Vituo vya Kupigia Kura

Wasimamizi wa Uchaguzi walihakikisha kwamba, maandalizi ya Vituo vya kupigia Kura yamekamilika kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu. Maandalizi hayo yalihusisha uhakiki na ujenzi wa Vituo vya muda katika maeneo ambayo hayakuwa na majengo ya Umma.

Uchaguzi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ule wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ulifanyika katika siku moja tarehe 25 Oktoba, 2015 Vituo vya Kupigia Kura vilivyotumika kwa Uchaguzi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar vilitumika pia kwa Uchaguzi wa Rais na Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata hivyo, kila Tume ilikuwa na Watendaji wake na vifaa vyake katika Vituo hivyo. Idadi ya Vituo vya Kupigia Kura kwa Tanzania Bara ilikuwa ni **63,525** na Tanzania Zanzibar ilikuwa ni **1,580**. Kila Kituo cha Kupigia Kura kilikuwa na Wapiga Kura wasiozidi **500.**

### 5.1.2 Tangazo la Uchaguzi

Kwa kuzingatia Kifungu cha 47(1) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, na Kifungu cha 49(1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Tangazo la Uchaguzi (*Notice of Election*) lilitolewa siku **8** kabla ya Siku ya Upigaji Kura.

Tangazo hilo, lilionesha Siku ya Upigaji Kura, Saa ya Kufungua na Kufungwa kwa zoezi la Upigaji Kura, Anuani ya Kituo au Vituo vya Kupigia Kura, Mfano wa Karatasi za Kura pamoja na Orodha ya Wapiga Kura waliopangiwa kupiga Kura katika kila Kituo.

Aidha, Tangazo lilibandikwa katika Ofisi za Wasimamizi wa Uchaguzi, Ofisi za Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya Kata na katika kila Kituo cha Kupigia Kura.

### 5.1.3 Wapiga Kura kutambua Vituo vya Kupigia Kura

Ili kuhakikisha kila Mpiga Kura anatambua Kituo alichopangiwa kupigia Kura mapema kabla ya Siku ya Uchaguzi, Tume iliweka utaratibu wa kuwezesha zoezi hilo kama ifuatavyo:-

(i) Tume iliwatangazia Wapiga Kura, kupitia Vyombo vya Habari na Magari ya Matangazo, kwenda katika Vituo walivyojiandikisha kuangalia orodha zilizobandikwa ili kutambua Vituo walivyopangiwa Kupiga Kura; na

(ii) Tume iliweka Mfumo wa Utambuzi wa Vituo vya Kupigia Kura (*Voters Interaction System*- VIS) kupitia ujumbe mfupi wa maandishi kwa njia ya simu (SMS) pamoja na Tovuti ya Tume. Utaratibu huo ulimsaidia Mpiga Kura kutambua Kituo alichopangiwa Kupigia Kura kupitia simu ya kiganjani au Tovuti, badala ya kwenda katika Kituo alichojiandikisha. Kwa wale ambao hawakuona taarifa zao waliwasiliana na Tume kupitia Kituo cha Mawasiliano (*call centre*) kwa ajili ya kupatiwa ufumbuzi.

### 5.1.4 Maamuzi ya Kisera kuhusu Upigaji Kura

Pamoja na utaratibu uliowekwa kisheria kuhusiana na taratibu za Upigaji Kura, Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa mamlaka iliyopewa kisheria, ilitoa maelekezo ya nyongeza ya kisera kulingana na mazingira. Hii, ilikuwa ni kwa ajili ya kurahisisha mwenendo mzima wa Upigaji Kura na kuhakikisha amani na utulivu unakuwepo. Maelekezo hayo ni kama ifuatavyo:

(i) Kwa Mpiga Kura ambaye atakuwa na Kadi ya Mpiga Kura ila namba ya Kadi ikatofautiana na namba iliyo kwenye Daftari la Kituo: **Aruhusiwe Kupiga Kura;**

(ii) Kwa Wapiga Kura ambao picha zao hazikuonekana vizuri au kutoonekana kabisa kwenye Kadi ya Mpiga Kura: Waruhusiwe Kupiga Kura hata pale ambapo picha zao hazitotokea kwenye Daftari;

(iii) Kwa Wapiga Kura walioandikishwa na Tume waliopo kwenye maeneo mapya kiutawala na majina ya maeneo hayo yanatofautiana na majina yaliyopo kwenye Kadi zao: Waruhusiwe Kupiga Kura;

(iv) Majina ya Wapiga Kura kuandaliwa katika Mfumo wa orodha bila kuwa na picha na kupelekwa katika Vituo walivyojiandikisha: Waruhusiwe Kupiga Kura;

(v) Wapiga Kura ambao majina yao yamo kwenye Daftari la Kituo lakini hawana Kadi ya Kupigia Kura: Wasiruhusiwe Kupiga Kura; na

(vi) Kwa Wapiga Kura ambao wana Kadi ya Kupigia Kura lakini hawapo katika Daftari: **Wasiruhusiwe Kupiga Kura.**

### 5.1.5 Mawakala wa Upigaji Kura

Vyama vya Siasa viliwasilisha kwa Msimamizi wa Uchaguzi orodha ya majina ya Mawakala na Vituo walivyopangiwa si zaidi ya siku **7** kabla ya siku ya Uchaguzi. Mawakala walikuwa na wajibu wa kulinda maslahi ya Wagombea na Vyama vyao vya Siasa katika Vituo vya Upigaji Kura. Hata hivyo, baadhi ya Vyama vya Siasa havikuweka Mawakala.

### 5.1.6 Usalama wa Vituo vya Kupigia Kura

Wasimamizi wa Uchaguzi walihakikisha kuwa Vituo vyote vya Kupigia Kura vinakuwa katika mazingira salama na yenye kufaa kwa ajili ya Kupiga Kura. Katika kutekeleza jukumu hili walishirikiana na Makamanda wa Polisi wa Wilaya na Washauri wa Mgambo wa Wilaya katika kupanga na kuandaa Walinzi kwa ajili ya kulinda Vituo vya Kupigia Kura. Siku ya Kupiga Kura kila Kituo cha Kupigia Kura kilikuwa na Mlinzi mmoja.

### 5.1.7 Risala ya Mwenyekiti wa Tume kwa Wapiga Kura

Siku moja kabla ya Uchaguzi, Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi kupitia Vyombo vya Habari alitoa wito kwa wananchi kujitokeza kwa wingi Kupiga Kura katika Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani. Vile vile, aliwakumbusha na kuwasisitiza kuhusu utaratibu wa Upigaji Kura hususan, muda wa kufungua na kufunga Vituo vya Kupigia Kura, Kuhesabu Kura, Kujumlisha Kura na Kutangaza Matokeo ya Uchaguzi. Aidha, Risala hiyo ilieleza mambo yanayopaswa na yasiyopaswa kufanywa na Mpiga Kura Siku ya Uchaguzi. Angalia **Kiambatisho Na. 4.**

## 5.2 Utaratibu wa Upigaji Kura

Upigaji Kura ulifanyika tarehe 25 Oktoba, 2015 kuanzia saa 1:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni. Kwa mujibu wa maelekezo yaliyotolewa na Tume ilipofika saa 10:00 jioni Mlinzi wa Kituo alisimama nyuma ya Mpiga Kura wa mwisho aliyekuwa kwenye mstari. Wapiga Kura ambao walikuwa katika Vituo vya Kupigia Kura kabla ya saa 10:00 jioni waliruhusiwa kuendelea Kupiga Kura.

Mawakala wa Upigaji Kura walipewa fursa ya kueleza kuridhika au kutoridhika kwao na mwenendo wa Upigaji Kura kwa kujaza Fomu Na.14.

Ili kurahisisha mwenendo wa Upigaji Kura, kuepuka fujo na msongamano, Wapiga Kura wote walijipanga katika mistari miwili, yaani; mstari wa wanawake na mstari wa wanaume. Kipaumbele kilitolewa kwa watu wenye Ulemavu, Wagonjwa, Wazee, Wajawazito na akina mama wenye Watoto Wachanga. Kwa Watu Wasioona, Tume iliweka utaratibu wa Kupiga Kura kwa kutumia kifaa maalum cha Kupigia Kura chenye maandishi ya nukta nundu (*tactile ballot folder*) na wale ambao hawakuwa na uwezo wa kutumia kifaa hicho, waliruhusiwa kuja na msaidizi. Kwa mujibu wa Sheria za Uchaguzi kwa Wapiga Kura Wasioona, Wasiojua kusoma na wasioweza kupiga kura wao wenyewe wanaruhusiwa kwenda kituoni na mtu atakayewasaidia Kupiga Kura. Endapo katika familia kuna mtu zaidi ya mmoja anyehitaji msaada wa kupiga kura watasaidiwa na mtu mmoja kutoka katika hiyo familia. Aidha, Tume ilitoa maelekezo kuwa baada ya Kupiga Kura Wapiga Kura warudi majumbani kuendelea na shughuli zao.

### 5.3 Kuahirisha Uchaguzi katika baadhi ya Majimbo na Kata

Kutokana na kufariki dunia kwa baadhi ya Wagombea na sababu zingine mbalimbali katika baadhi ya maeneo, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ililazimika kuahirisha Uchaguzi wa Wabunge katika Majimbo **8** na Uchaguzi wa Madiwani katika Kata **33** kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 22** na **Jedwali Na. 23.**

**Jedwali Na. 22: Orodha ya Majimbo ambayo Uchaguzi wa Wabunge Uliahirishwa**

| Na. | Mkoa | Halmashauri | Jimbo | Sababu |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mtwara | Wilaya ya Masasi | Lulindi | Kasoro mbalimbali |
| 2. | Mjini Magharibi | Wilaya ya Magharibi ‘B’ | Kijitoupele | Kasoro mbalimbali |
| 3. | Tanga | Wilaya ya Lushoto | Lushoto | Mgombea Kufariki (CCM) |
| 4. | Morogoro | Wilaya ya Ulanga | Ulanga Mashariki | Mgombea Kufariki (CCM) |
| 5. | Tanga | Mji Handeni | Handeni Mjini | Mgombea Kufariki (CCM) |
| 6. | Njombe | Wilaya ya Ludewa | Ludewa | Mgombea Kufariki (CCM) |
| 7. | Arusha | Jiji la Arusha | Arusha Mjini | Mgombea Kufariki (ACT – Wazalendo) |
| 8. | Mtwara | Mji Masasi | Masasi Mjini | Mgombea Kufariki ( NLD) |

**Jedwali Na. 23: Orodha ya Kata ambazo Uchaguzi Uliahirishwa**

| Na. | Halmashauri | Jimbo | Kata | Sababu |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Wilaya ya Ngorongoro | Ngorongoro | Malambo | Kasoro mbalimbali |
| | | | Ngaresero | Kasoro mbalimbali |
| 2. | Mji wa Korogwe | Korogwe Mjini | Majengo | Kasoro mbalimbali |
| 3. | Wilaya ya Kilindi | Kilindi | Songwe | Kasoro mbalimbali |
| 4. | Wilaya ya Kwimba | Kwimba | Bupamwa | Kasoro mbalimbali |
| 5. | Wilaya ya Bariadi | Bariadi | Matongo | Kasoro mbalimbali |
| 6. | Wilaya ya Urambo | Urambo | Kiloleni | Kasoro mbalimbali |
| 7. | Majispaa Kigoma/Ujiji | Kigoma Mjini | Kagera | Kasoro mbalimbali |
| 8. | Wilaya ya Nzega | Nzega Vijijini | Mizibaziba | Kasoro mbalimbali |
| | | Nzega Vijijini | Tongi | Kasoro mbalimbali |
| 9. | Wilaya ya Geita | Busanda | Ludutwa | Kasoro mbalimbali |
| 10. | Wilaya ya Rorya | Rorya | Bukula | Kasoro mbalimbali |
| 11. | Wilaya ya Chunya | Songwe | Mwambani | Kasoro mbalimbali |
| | | Lupa | Itewe | Kasoro mbalimbali |
| | | Lupa | Mkola | Kasoro mbalimbali |
| | | Songwe | Mbuyuni | Kasoro mbalimbali |
| 12. | Wilaya ya Mbarari | Mbarali | Rujewa | Kasoro mbalimbali |
| 13. | Wilaya ya Sumbawanga | Kwela | Milepa | Kasoro mbalimbali |
| 14. | Wilaya Mpanda | Mpanda | Magamba | Kasoro mbalimbali |
| 15. | Wilaya ya Namtumbo | Namtumbo | Mkongo - Gulioni | Kasoro mbalimbali |
| | | | Lisimonji | Kasoro mbalimbali |
| 16. | Wilaya ya Ludewa | Ludewa | Mkongobaki | Kasoro mbalimbali |
| 17. | Wilaya ya Madaba | Madaba | Mahanje | Kasoro mbalimbali |
| 18. | Manispaa ya Kinondoni | Kibamba | Saranga | Kasoro mbalimbali |
| 19. | Jiji la Mbeya | Mbeya Mjini | Uyole | Mgombea Kufariki |
| 20. | Wilaya ya Hai | Hai | Bomang'ombe | Mgombea Kufariki (CCM) |
| 21. | Wilaya ya Shinyanga | Solwa | Bukene | Mgombea Kufariki (CCM) |
| 22. | Wilaya ya Mvomero | Mvomero | Mvomero | Mgombea Kufariki (CCM) |
| 23. | Manispaa ya Dodoma | Dodoma Mjini | Ipala | Mgombea Kufariki (CHADEMA) |
| 24. | Wilaya ya | Iramba | Msingi | Mgombea Kufariki |

| Na. | Halmashauri | Jimbo | Kata | Sababu |
|---|---|---|---|---|
| | Mkalama | Mashariki | | (CHADEMA) |
| 25. | Wilaya ya Geita | Busanda | Nyamwilolelwa | Mgombea Kufariki (CCM) |
| 26. | Wilaya ya Muleba | Muleba Kusini | Muleba | Mgombea Kufariki (CCM) |
| 27. | Wilaya ya Ngara | Ngara | Kasulo | Mgombea Kufariki (ACT) |

**NB:** *Kasoro mbalimbali inajumuisha upungufu wa Karatasi za Kupigia Kura, kukosewa kwa jina la mgombea katika Karatasi za Kupigia Kura, kuharibiwa kwa vifaa vya Kupigia Kura na kuchelewa kufika kwa Karatasi za Kupigia Kura.*

### 5.4 Ratiba ya Uteuzi na Uchaguzi kwa Majimbo ambayo Uchaguzi Uliahirishwa

Tume ilitangaza Ratiba ya Uteuzi wa wagombea wa nafasi za Ubunge na Uchaguzi katika majimbo ambayo Chaguzi zake ziliahirishwa. Ratiba ya Uteuzi wa wagombea na Uchaguzi ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 24.**

**Jedwali Na. 24: Ratiba ya Uteuzi na Uchaguzi katika Majimbo Yaliyoahirishwa**

| Na. | Mkoa | Halmashauri | Jimbo | Tarehe ya Uteuzi | Tarehe ya Uchaguzi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Mtwara | Wilaya ya Masasi | Lulindi | 21 Agosti, 2015 | 15 Novemba, 2015 |
| 2. | Mjini Magharibi | Wilaya ya Magharibi 'B' | Kijitoupele | 21 Agosti, 2015 | 20 Machi, 2015 |
| 3. | Tanga | Wilaya ya Lushoto | Lushoto | 12 Oktoba, 2015 | 22 Novemba, 2015 |
| 4. | Morogoro | Wilaya ya Ulanga | Ulanga Mashariki | 12 Oktoba, 2015 | 22 Novemba, 2015 |
| 5. | Tanga | Mji Handeni | Handeni Mjini | 4 Novemba, 2015 | 13 Desemba, 2015 |
| 6. | Njombe | Wilaya ya Ludewa | Ludewa | 4 Novemba, 2015 | 20 Desemba, 2015 |
| 7. | Arusha | Jiji la Arusha | Arusha Mjini | 4 Novemba, 2015 | 13 Desemba, 2015 |
| 8. | Mtwara | Mji Masasi | Masasi Mjini | 4 Novemba, 2015 | 20 Desemba, 2015 |

### 5.5 Kuhesabu Kura

Baada ya Upigaji Kura kukamilika na taratibu za kufunga Kituo kukamilika, Kituo cha Kupigia Kura kilibadilika na kuwa Kituo cha Kuhesabu Kura. Kura za Rais zilianza kuhesabiwa mwanzo, zikifuata Kura za Wabunge na mwisho Kura za Madiwani. Msimamizi wa Kituo alifuata utaratibu ufuatao:-

(i) Alikagua Masanduku ya Kura ili kuthibitisha kuwa lakiri hazijafunguliwa, kisha alifungua masanduku kwa kukata lakiri zilizopo pembeni tu;

(ii) Alimimina Kura zote juu ya meza na kuanza kuhesabu Kura moja baada ya nyingine kwa sauti iliyosikika na kila mtu. Kura ambazo zilizoonekana kwenye sanduku ambalo sio lake, zilihesabiwa katika Kura za sanduku linalohusika;

(iii) Aliandika katika Daftari la kuandikia (*Drafting Pad*) idadi ya Kura zote zilizopatikana katika kila Sanduku la Kura;

(iv) Alikunjua Kura moja baada ya nyingine kwa kuonesha upande wa juu wa picha za Wagombea na alitangaza kwa sauti iliyosikika na kila mtu aliyekuwepo ndani ya Kituo akitaja Mgombea aliyepigiwa Kura. Aidha, alionesha Karatasi ya Kura ambayo haikuwa na alama yoyote au iliyoharibika. Kura zilipangwa kwa mafungu tofauti kwa kila Mgombea na upande wa picha ukiwa juu;

(v) Alihesabu kwa sauti iliyosikika na kila mtu na kuandika idadi ya Kura kwa kila fungu. Idadi ya Kura alizopata kila Mgombea, Kura zilizokataliwa, Kura zenye mgogoro zililinganishwa na idadi ya Kura zilizopatikana katika Sanduku la Kura zilizopigwa katika Kituo;

(vi) Baada ya kumaliza Kuhesabu Kura, alizifunga na kuziweka kwenye bahasha tofauti, ambapo Kura zenye Mgogoro ziliwekwa katika Bahasha Na. 5A, 5B na 5C. Kura zilizokataliwa ziliwekwa katika Bahasha Na. 6A, 6B na 6C. Kura Halali ziliwekwa katika Bahasha Na. 7A, 7B na 7C;

(vii) Alijaza Matokeo ya Uchaguzi wa Rais katika Fomu Na. 21A, Wabunge katika Fomu Na. 21B na Madiwani katika Fomu Na. 21C ambazo zilisainiwa na Msimamizi wa Kituo cha Kupigia Kura na Wagombea/Mawakala wa Kuhesabu Kura waliokuwepo. Hata hivyo, Wagombea/Mawakala kutosaini fomu hizo hakubatilishi matokeo ya Uchaguzi;

(viii) Alibandika mahali pa wazi Fomu za Matokeo ya Urais, Wabunge na Madiwani na kisha aliwapatia Mawakala nakala za Taarifa za Matokeo ya Uchaguzi; na

(ix) Aliweka Bahasha za Kura Halali, Kura zenye Mgogoro na Kura Zilizokataliwa kwenye masanduku ya Kura za Uchaguzi unaohusika na kuyafunga. Bahasha ya Kituo cha Kupigia Kura na Fomu zote za Matokeo hazikuwekwa ndani ya sanduku.

Aidha, Mawakala wa Kuhesabu Kura walitakiwa na Msimamizi wa Kituo Kujaza Fomu Na. 16 katika kila hatua ya Kuhesabu Kura kuonesha kama waliridhika au wana malalamiko.

Masanduku ya Kura na Fomu za Matokeo ya Nafasi ya Kiti cha Rais na Ubunge yalisafirishwa na kukabidhiwa kwa Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Jimbo katika Kituo cha Kujumlishia Kura ngazi ya Halmashauri. Aidha, Masanduku na Fomu za Matokeo ya Nafasi ya Kiti cha Udiwani yalisafirishwa na kukabidhiwa kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi wa Kata katika Kituo cha Kujumlishia Matokeo ngazi ya Kata. Utaratibu wa kusafirisha masanduku ya Kura ulihusisha Mawakala wa Vyama pamoja na Askari.

## SURA YA SITA

## KUJUMLISHA KURA NA KUTANGAZA MATOKEO YA UCHAGUZI

### 6.1 Kujumlisha Kura

Zoezi la Kujumlisha Kura lilianza katika Vituo vya Kujumlishia Kura mara baada ya kupokea Masanduku ya Kura na Fomu za Matokeo ya Uchaguzi kutoka katika Vituo vya Kuhesabia Kura. Aidha, wagombea na Vyama vya Siasa vilivyoshiriki Uchaguzi walipewa taarifa ya muda na mahali zoezi la Kujumlisha Kura litakapofanyika**.** Kura za Uchaguzi wa Madiwani zilijumlishiwa katika ngazi ya Kata na Kura za Urais na Ubunge zilijumlishiwa katika ngazi ya Jimbo.

#### 6.1.1 Utaratibu wa Kujumlisha Kura

Zoezi la kujumlisha Kura za Uchaguzi wa Rais, Ubunge na Udiwani lilifanyika kwa mujibu wa Kifungu cha 80 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, na Kifungu cha 81 cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura 292.

Mara baada ya Msimamizi wa Uchaguzi kupokea masanduku yote ya Kura na Fomu zote za Matokeo alitoa uamuzi wa mwisho kuhusu Kura zenye mgogoro. Kisha, zoezi la kujumlisha Kura lilifanyika ambapo Msimamizi wa Uchaguzi/Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi alitangaza kwa sauti Matokeo ya kila Kituo cha Kupigia Kura. Wakati wa Kujumlisha Matokeo ya Uchaguzi ngazi ya Jimbo, Msimamizi wa Uchaguzi/Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi alijumlisha Kura za Uchaguzi wa Rais kwanza na kisha Kura za Mbunge.

Mara baada ya kukamilisha Ujumlishaji wa Kura, Msimamizi wa Uchaguzi/Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi alithibitisha Matokeo ya Jimbo au Kata husika na kujaza Fomu Na. 24A kwa Matokeo ya Urais, Fomu Na. 24B kwa Matokeo ya Ubunge na Fomu Na. 24C kwa Matokeo ya Udiwani.

Matokeo ya Uchaguzi wa Rais yalitumwa kwa kutumia Mfumo wa Menejimenti ya Matokeo (RMS) kwenda Kituo cha Kujumlishia Kura za Uchaguzi wa Rais*.* Zoezi la Kujumlisha Kura za Uchaguzi wa Rais lilifanywa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika Kituo cha Kujumlishia na Kutangaza Matokeo kilichokuwa Dar es Salaam katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere (*Julius Nyerere International Convention Center* – JNICC).

Kwa Matokeo ya Uchaguzi wa Ubunge na Udiwani Msimamizi wa Uchaguzi/Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi alitoa Taarifa ya Matokeo hadharani na kumtangaza Mshindi. Baada ya hapo, alimtaarifu Mgombea aliyeshinda na kumpatia Hati ya Kuchaguliwa. Nakala ya Fomu za Matokeo ya Uchaguzi wa Rais, Ubunge na Udiwani ilibandikwa katika ubao wa Matangazo nje ya Kituo cha Kujumlishia Kura na Nakala yake walipatiwa Mawakala au Wagombea waliokuwepo katika Kituo cha Kujumlishia Kura.

Katika hatua zote za Ujumlishaji Kura za Uchaguzi wa Rais, Ubunge na Udiwani Mawakala wa Kujumlisha Kura na Wagombea waliruhusiwa kushiriki.

#### 6.1.2 Mfumo wa Menejimenti ya Matokeo ( *Results Management System* – RMS)

Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilitumia Mfumo wa Menejimenti ya Matokeo (RMS) katika kujumlisha na kutangaza Matokeo ya Urais na Ubunge katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. Mfumo huu ulifanikisha upatikanaji wa Matokeo kwa urahisi, usahihi, uwazi na kwa wakati. Aidha, Tume iliandaa Mfumo kupitia programu ya *Microsoft Excel* ambao ulitumika kama Mfumo mbadala wa RMS.

### 6.2 Kutangaza Matokeo ya Uchaguzi.

Kwa mujibu wa Kifungu Na. 35F (7) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ina jukumu la Kutangaza Matokeo ya nafasi ya Kiti cha Rais. Aidha, Kifungu cha 81(a) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, Msimamizi wa Uchaguzi ana jukumu la Kutangaza Matokeo ya nafasi ya Ubunge. Vilevile, Wasimamizi wa Uchaguzi au Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya Kata ndiyo wenye jukumu la kutangaza Matokeo nafasi ya Udiwani kwa mujibu wa Kifungu cha 82(a) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292.



*Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Mhe. Jaji Mkuu (Mst - Z) Hamid M. Hamid* **(***wa pili kushoto) akitangaza Matokeo ya Awali ya Kiti cha Rais kwenye Kituo cha Kutangaza Matokeo cha JNICC, Dar Es Salaam*

### 6.2.1 Matokeo ya Uchaguzi wa Rais

Matokeo ya Uchaguzi wa Rais ya Awali (*Partial Results)* kutoka katika majimbo yalianza kupokelewa kuanzia tarehe 26 Oktoba, 2015 alfajiri. Matokeo hayo yalihakikiwa na kuanza kutangazwa na Tume kadri yalivyopokelewa. Tume ilitangaza rasmi matokeo ya Uchaguzi wa Rais Tarehe 29 Oktoba, 2015 saa 10:00 jioni, ikiwa ni saa **72** tangu Uchaguzi ulipomalizika saa 10:00 jioni ya tarehe 25 Oktoba, 2015. Tume ilitimiza ahadi yake ya kutangaza matokeo kama ilivyopanga.

Katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, idadi ya Wapiga Kura walioandikishwa walikuwa **23,161,440** waliopiga kura katika Uchaguzi wa Kiti cha Rais walikuwa **15,596,110** sawa na asilimia **67.34** ya walioandikishwa. Kura halali zilikuwa **15,193,862** sawa na asilimia **97.42** ya waliopiga Kura na Kura zilizokataliwa zilikuwa **402,248** sawa na asilimia **2.58** ya waliopiga Kura. Wapiga Kura ambao hawakujitokeza kupiga Kura walikuwa **7,565,330** sawa na asilimia **32.66** ya walioandikishwa.

Tume ilimtangaza **Dkt. John Pombe Joseph Magufuli** aliyekuwa Mgombea kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi kuwa mshindi wa Kiti cha Rais kwa kupata Kura **8,882,935** ambazo ni sawa na asilimia **58.46** ya Kura zote halali zilizopigwa. Tarehe 30 Oktoba, 2015 Tume ilimkabidhi mshindi wa kiti cha Urais Hati ya Kuchaguliwa. Matokeo ya kura alizopata kila Mgombea wa Kiti cha Rais ni kama yanavyoonekana katika **Jedwali Na. 25** na **Chati Na. 5**



*Mawakala wa Vyama vya Siasa na Tume wakihakiki Matokeo ya Kiti cha Rais wakishuhudiwa na Watazamaji wa Uchaguzi kwenye Kituo cha Kutangaza Matokeo cha JNICC, Dar es Salaam.*



*Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Mhe. Jaji (Mst.) Damian Z. Lubuva (Mbele katikati) akitangaza Matokeo ya Kiti cha Rais kwenye Kituo cha Kutangaza Matokeo cha JNICC, Dar Es Salaam.*

**Jedwali Na. 25: Matokeo ya kura alizopata kila Mgombea wa Kiti cha Rais**

| Na. | Chama cha Siasa | Jina la Mgombea | Idadi ya Kura | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1. | ACT-Wazalendo | Anna Elisha Mghwira | 98,763 | 0.65 |
| 2. | ADC | Chief Lutalosa Yemba | 66,049 | 0.43 |
| 3. | CCM | Dkt. John Pombe Joseph Magufuli | 8,882,935 | 58.46 |
| 4. | CHADEMA | Edward Ngoyai Lowassa | 6,072,848 | 39.97 |
| 5. | CHAUMMA | Hashim Spunda Rungwe | 49,256 | 0.32 |
| 6. | NRA | Kasambala Janken Malik | 8,028 | 0.05 |
| 7. | TLP | Elifatio Macmillan Lyimo | 8,198 | 0.05 |
| 8. | UPDP | Dovutwa Fahmi Nassoro | 7,785 | 0.05 |
| **Jumla** | | | **15,193,862** | **100** |

## Chati Na. 5: Matokeo ya Kiti cha Rais kwa kila Chama






*Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Mhe. Jaji (Mst.) Damian Z. Lubuva (kulia) akimkabidhi Cheti cha Ushindi Rais Mteule wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli katika hafla iliyofanyika kwenye Ukumbi wa Diamond Jubilee, Jijini Dar Es Salaam. Kushoto ni Makamu wa Rais Mteule  Mhe. Samia Suluhu Hassan.*

### 6.2.2 Matokeo ya Uchaguzi wa Ubunge

Wasimamizi wa Uchaguzi walianza kutangaza Matokeo ya Ubunge katika Majimbo mbalimbali mara baada ya hatua ya kujumlisha Kura kukamilika. Katika Uchaguzi wa Wabunge, CCM ilipata asilimia **73.86**, CHADEMA asilimia **13.26,** CUF asilimia **12.12** na Vyama vya ACT-Wazalendo na NCCR-Mageuzi vilipata asilimia **0.38** kila kimoja. Kati ya Wabunge **264** wa kuchaguliwa**,** wanawake ni **26** ambao ni sawa na asilimia **10** na wanaume ni **238** sawa na asilimia **90** kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 26** na **Chati Na. 6.** Aidha, Orodha ya Wabunge walioshinda Uchaguzi wa mwaka 2015 ni kama inavyooneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 5.**

**Jedwali Na. 26: Matokeo ya Ubunge kwa kila Chama cha Siasa**

| Na. | Jina la Chama | Idadi ya Wabunge | Asilimia | Jinsi | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Me | Ke |
| 1. | ACT – Wazalendo | 1 | 0.38 | 1 | 0 |
| 2. | CCM | 195 | 73.86 | 177 | 18 |
| 3. | CHADEMA | 35 | 13.26 | 29 | 6 |
| 4. | CUF | 32 | 12.12 | 30 | 2 |
| 5. | NCCR-Mageuzi | 1 | 0.38 | 1 | 0 |
| **Jumla** | | **264** | | **238** | **26** |

**Chati Na. 6: Matokeo ya Ubunge kwa kila Chama**



### 6.2.3 Matokeo ya Udiwani.

Matokeo ya Udiwani yalianza kutangazwa kwenye Kata husika mara baada ya zoezi la kujumlisha Kura kukamilika. CCM ilipata asilimia **72. 86**, CHADEMA asilimia **20.3**, CUF asilimia **5.37**, ACT-Wazalendo asilimia **0.81**, NCCR-Mageuzi asilimia **0.58,** NLD asilimia **0.03** na TLP ilipata asilimia **0.05.** Aidha, Idadi ya Madiwani Wanawake wa kuchaguliwa ni **204** ambayo ni sawa na asilimia **5.2** ya Madiwani Wote. Idadi ya viti vya Udiwani kwa kila chama ni kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 27** na **Chati Na. 7.**

**Jedwali Na. 27: Matokeo ya Udiwani kwa kila Chama**

| Na. | Chama cha Siasa | Idadi ya walioshinda | Asilimia | Jinsi | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Me | Ke |
| 1. | ACT – Wazalendo | 32 | 0.81 | 32 | 0 |
| 2. | CCM | 2,875 | 72.86 | 2,700 | 175 |
| 3. | CHADEMA | 801 | 20.30 | 779 | 22 |
| 4. | CUF | 212 | 5.37 | 205 | 7 |
| 5. | NCCR-Mageuzi | 23 | 0.58 | 23 | 0 |
| 6. | NLD | 1 | 0.03 | 1 | 0 |
| 7. | TLP | 2 | 0.05 | 2 | 0 |
| | **JUMLA** | **3,946** | **100** | **3,742** | **204** |

**Chati Na. 7: Matokeo ya Madiwani kwa Chama**



### 6.3 Uteuzi wa Wabunge na Madiwani Wanawake wa Viti Maalum

Ibara ya 66 (1) (b) na Ibara ya 78 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Kifungu cha 86A cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, vinatambua uwepo wa Wabunge Wanawake wa Viti Maalum wasiopungua asilimia **30** ya Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata hivyo, kutokana na uamuzi wa Serikali kuongeza Idadi ya Wabunge Wanawake wa Viti Maalum, idadi yao imeongezeka kutoka asilimia **30** hadi kufikia asilimia **40** ya Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Uwepo wa Madiwani Wanawake wa Viti Maalum katika Baraza la Halmashauri wasiopungua theluthi moja (1/3) ya Wajumbe wote wa Halmashauri husika unaelezwa katika Kifungu cha 35 (1) (c) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287, Kifungu cha 19 (1) (c) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura 288, pamoja na Kifungu cha 86A cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura 292.

#### 6.3.1 Uteuzi wa Wabunge Wanawake wa Viti Maalum

Kwa madhumuni ya kupata idadi ya Wabunge Wanawake wa Viti Maalum idadi ya Wabunge iliyotumika kukokotoa Idadi ya Wabunge wa Viti Maalum ni **281** waliopatikana kwa utaratibu ufuatao:

(i) Wabunge wa Majimbo **264;**

(ii) Wabunge **5** kutoka Baraza la Wawakilishi;

(iii) Wabunge **10** wa Kuteuliwa na Rais;

(iv) Mwanasheria Mkuu wa Serikali; na

(v) Spika, akiwa siyo Mbunge.

Kwa madhumuni ya kupata Wabunge Wanawake wa Viti Maalum ifuatayo ni Kanuni ya namna ya kupata idadi yao:-

***Idadi ya Wabunge wote* x *Asilimia 40***

***Idadi = 281* x *40/100 = 112.4 ≈113***

Hivyo, Jumla ya Wabunge Wanawake wa Viti Maalum ni **113.**

Kwa mujibu wa Ibara ya 78 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Vyama vya Siasa vilivyoshiriki katika Uchaguzi Mkuu kwa kufuata utaratibu uliowekwa, na kupata angalau asilimia **5** ya Kura zote halali za Wabunge vilipendekeza kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi majina ya Wanawake kwa kuzingatia uwiano wa Kura ambazo kila Chama kimepata katika Uchaguzi wa Wabunge.

Jinsi ya kupata asilimia **5** ya Kura zote za Ubunge ni kama inavyoonekana katika kanuni ifuatayo:-

| |
|---|
| *Idadi ya Kura zote halali za Ubunge za Vyama vyote x 5/100*<br>*= 5% ya Kura zote* |

Hivyo asilimia **5** ni: **15,604,523 x 5/100**

**=780,226**

Hivyo, kila Chama kilichoshiriki Uchaguzi wa Ubunge na kupata angalau kura **780,226** ambayo ni sawa na asilimia **5** kilipata Viti Maalum vya Ubunge.

#### 6.3.1.1 Mgawanyo wa Viti Maalum vya Ubunge kwa Chama

Baada ya ukokotoaji wa Matokeo ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, Vyama **3** vya CCM, CHADEMA na CUF tu ndivyo vilifanikiwa kufikisha asilimia **5** ya Kura za Wabunge. Kwa kuzingatia Kanuni iliyoainishwa hapo juu, mgawanyo wa Viti **113** ulikuwa kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 28 na Chati Na. 8.** Orodha ya Wabunge Wanawake wa Viti Maalum ni kama inavyooneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 6.**

**Jedwali Na. 28: Idadi ya Wabunge Wanawake wa Viti Maalum kwa Chama**

| Na. | Chama cha Siasa | Idadi ya Kura Halali | Idadi ya Viti | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1. | CCM | 8,495,488 | 66 | 58 |
| 2. | CHADEMA | 4,720,881 | 37 | 33 |
| 3. | CUF | 1,274,911 | 10 | 9 |
| **Jumla** | | **14,491,280** | **113** | **100** |

**Chati Na. 8: Wabunge Wanawake wa Viti Maalum kwa Chama**



### 6.3.2 Uteuzi wa Madiwani Wanawake Viti Maalum

Tume ilifanya Uteuzi wa Madiwani wanawake Viti Maalum katika Halmashauri zote nchini kwa kuzingatia ushindi wa chama katika Halmashauri.

**Kanuni ya kupata idadi ya Madiwani Wanawake Viti Maalum kwenye Halmashauri ni kama ifuatavyo:**

***(Idadi ya Kata katika Halmashauri + Mbunge au Wabunge)* x *1/3***

Jumla ya Kata zote ni **3,946** na Majimbo (Wabunge) yote ni **264.**

**= (3,946 + 264) x 1/3**

**=(4,210) x 1/3= 1,404**

Hivyo, jumla ya Viti Maalum vya Madiwani kwa Nchi nzima ni **1,404**.

Aidha, Kanuni ya Mgawanyo wa Madiwani Wanawake Viti Maalum kwa kila Chama katika Halmashauri ni kama ifuatavyo:-

$$\frac{\textit{Idadi ya Kata ambazo Chama kimeshinda} \times \textit{Idadi ya Viti Maalum katika Halmashauri}}{\textit{Idadi ya Kata katika Halmashauri}}$$

#### 6.3.2.1 Mgawanyo wa Madiwani Wanawake Viti Maalum kwa Vyama

Baada ya ukokotoaji, imeonekana kuwa Viti Maalum vya Madiwani Wanawake vipo **1,404** katika Halmashauri zote Tanzania Bara. Hivyo, mgawanyo kwa kila Halmashauri ulitegemea wingi wa Kata kwenye Halmashauri husika. Aidha, Vyama vya Siasa vilipata Viti hivyo Maalum kwenye Halmashauri kwa kutegemea ushindi wa Kata kwenye Halmashauri husika.

Katika mgawanyo huo CCM ilipata viti **1,029** sawa na asilimia **73.29,** CHADEMA ilipata viti **279** sawa na asilimia **19.87,** CUF ilipata viti **78** sawa na asilimia **5.56,** ACT - Wazalendo ilipata viti **10** sawa na asilimia **0.71** na NCCR - Mageuzi ilipata viti **8** sawa na asilimia **0.57.**

Mgawanyo wa Viti Maalum na asilimia ya Madiwani Wanawake wa Viti Maalum kwa kila Chama ni kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 29** na **Chati Na. 9**

**Jedwali Na. 29: Mgawanyo wa Madiwani Wanawake Viti Maalum kwaChama**

| Na. | Chama cha Siasa | Idadi ya Viti | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 1. | ACT- Wazalendo | 10 | 0.71 |
| 2. | CCM | 1,029 | 73.29 |
| 3. | CHADEMA | 279 | 19.87 |
| 4. | CUF | 78 | 5.56 |
| 5. | NCCR-Mageuzi | 8 | 0.57 |
| **Jumla** | | **1,404** | **100** |

**Chati Na. 9: Madiwani Wanawake wa Viti Maalum kwa Chama**




### 6.4 Kesi za Kupinga Matokeo ya Ubunge na Udiwani

Kifungu cha 108 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na Kifungu cha 107 cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 vinatoa haki na nafasi ya kupinga Matokeo ya Uchaguzi wa Ubunge na Udiwani.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 111 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na Kifungu cha 110 cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, malalamiko ya Uchaguzi yanaweza kufunguliwa na mmojawapo wa hawa wafuatao:-

(i) Mtu ambaye alipiga Kura kwa mujibu wa Sheria au alikuwa ana haki ya Kupiga Kura katika Uchaguzi ambao unalalamikiwa;

(ii) Mtu ambaye anadai kuwa alikuwa na haki ya kuteuliwa kuwa mgombea au kuchaguliwa katika Uchaguzi huo;

(iii) Mtu ambaye anadai kuwa alikuwa mgombea katika Uchaguzi huo; na

(iv) Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mara baada ya kutangazwa kwa Matokeo ya Ubunge na Udiwani katika Majimbo na Kata mbalimbali, jumla ya Kesi **52** za kupinga Matokeo ya Ubunge zilifunguliwa katika Kanda mbalimbali za Mahakama Kuu. Kwa upande wa Uchaguzi wa Udiwani, zimefunguliwa jumla ya Kesi **194** kupinga Matokeo ya Udiwani katika Kata mbalimbali.

Aidha, Kifungu cha 113 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na Kifungu cha 112 cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, vinaeleza kuwa, iwapo itatokea Mahakama itakubaliana na madai ya malalamiko katika Kesi hizo na kuamua kutengua Matokeo ya Uchaguzi husika, Tume italazimika kuitisha, kusimamia na kuendesha upya Uchaguzi katika Jimbo au Kata husika.

## SURA YA SABA

## USHIRIKISHWAJI WA WADAU WA UCHAGUZI

### 7.1 Ushirikishwaji wa Wadau

Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika kutekeleza majukumu yake wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, iliwashirikisha wadau mbalimbali wa Uchaguzi katika kila hatua kadri ilivyoona inafaa. Lengo la ushirikishwaji ilikuwa ni kuongeza uwazi na uwajibikaji katika utekelezaji wa majukumu na kuwapa taarifa wadau hao juu ya hatua mbalimbali katika Uchaguzi na kupata maoni yao ili kuboresha mchakato wa Uchaguzi.

### 7.1.1 Wadau Walioshirikishwa

Wadau walioshirikishwa ni pamoja na Serikali, Vyama vya Siasa, Asasi za Kiraia, Vyombo vya Habari, Taasisi na Viongozi wa Dini, Makundi Maalum katika jamii, Taasisi za Ulinzi na Usalama, Washirika wa Maendeleo na Watazamaji wa Uchaguzi.

#### 7.1.1.1 Serikali

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake iliyopewa kikatiba na kisheria kwa kuipatia rasilimali na nyenzo muhimu za kuendeshea mchakato wa Uchaguzi. Hivyo, Tume ilikutana na Taasisi za Serikali kwa awamu mbalimbali katika kutekeleza majukumu yake. Taasisi hizo ni pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Fedha, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Ushirikiano wa Tume na Taasisi hizi za Serikali umefanyika katika hatua za maandalizi ya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na Uchaguzi Mkuu. Ushirikishwaji huo ni pamoja na wawakilishi wa Taasisi hizo kujumuishwa katika Kamati za Ushauri kama vile Kamati ya Ugawaji wa vifaa na Lojisitiki, ambapo kamati hii ilihusisha mwakilishi kutoka Mamlaka ya Bandari (*Tanzania Ports Authority* – TPA), Mamlaka ya Mapato (*Tanzania Revenue Authority* - TRA), Jeshi la Polisi na Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Kamati ya Watazamaji wa Uchaguzi na Mashirika ya Kimataifa ilijumuisha wawakilishi kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Ofisi ya Waziri Mkuu. Kamati ya Mahusiano ya Serikali na Vyama vya Siasa ilihusisha wawakilishi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa.

Aidha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali alishirikishwa katika uaandaji wa nyaraka mbalimbali za kisheria kuhusiana na Uchaguzi na katika uendeshaji wa kesi zilizohusiana na Uchaguzi Mkuu.

### 7.1.1.2 Vyama vya Siasa

Tume ilishirikisha Vyama vya Siasa katika hatua za Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na Uchaguzi Mkuu. Ushirikishwaji huo ni pamoja na mikutano ya mara kwa mara kwa lengo la kuwapa uelewa zaidi juu ya Teknolojia na Mifumo mbalimbali iliyotumiwa na Tume mfano, Teknolojia ya BVR kwa ajili ya Uandikishaji Wapiga Kura, Mfumo wa Menejimenti wa Matokeo (RMS) na Mfumo wa Menejimenti ya Wagombea (CMS). Vyama vya Siasa pia, vilishirikishwa katika uandaaji wa Maadili ya Uchaguzi kwa kutoa maoni yaliyosaidia kuboresha Kanuni na Maadili hayo.

Wawakilishi wa Vyama vya Siasa walishirikishwa katika Kamati za Maadili ya Uchaguzi, Kamati ya Kuratibu Kampeni za Uchaguzi, Kamati ya Mahusiano ya Serikali na Vyama vya Siasa, Kamati ya Mamlaka na Taratibu za Uendeshaji Uchaguzi, Kamati ya Upatikanaji na Ugawaji wa Vifaa na Kamati ya Watazamaji wa Uchaguzi na Mashirika ya Kimataifa, Kamati ya Elimu ya Mpiga Kura na Uratibu wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Kamati ya Habari na Mawasiliano. Katika vituo vya uandikishaji Wapiga Kura, Vituo vya Kupiga, Kuhesabu na Kujumlisha Kura, Mawakala wa Vyama na Wagombea walipewa nafasi ya kujiridhisha kila hatua iliyokuwa ikifanyika katika vituo hivyo na kutakiwa kujaza fomu maalum pale ambapo hawakuridhishwa na mwenendo katika vituo hivyo. Vilevile, kila baada ya kuhesabu na kujumlisha kura walipewa nakala ya matokeo.

### 7.1.1.3 Asasi za Kiraia

Tume wakati wa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na Uchaguzi Mkuu ilishirikisha Asasi za Kiraia. Asasi hizo zilipewa kibali na Tume cha kutoa Elimu ya Mpiga Kura.

Jumla ya Asasi **447** zilipewa kibali cha kutoa Elimu ya Mpiga Kura katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, Tume ilifanya mikutano na Asasi hizo kwa nyakati tofauti kuwapa uelewa na taarifa za Mchakato wa Uchaguzi.

### 7.1.1.4 Vyombo vya Habari

Tume ilitumia Vyombo vya Habari vya Serikali na binafsi katika kutoa Elimu ya Mpiga Kura na kutoa taarifa mbalimbali kwa Wananchi wakati wa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Mpiga Kura na wakati wa Uchaguzi Mkuu. Aidha, Tume ilikutana na Wamiliki, Wahariri na Waandishi wa Vyombo mbalimbali vya Habari ili kuwashirikisha, kuwapa taarifa, kuwasisitiza na kuwahamasisha Wananchi kujitokeza kushiriki katika Mchakato wa Uchaguzi.

Katika hatua hiyo, wananchi walielimishwa kupitia vipindi na makala za vyombo mbalimbali vya habari kama TBC1 *vipindi vya Tuambie, Kura yangu na Jambo Tanzania,* Azam TV *vipindi vya Morning Trumpet na Funguka,* Channel Ten *kipindi cha Tufunge Safari*, Clouds Redio *kipindi cha Temino na Power Breakfast,* Micheweni FM *Kipindi cha Majadiliano ya Uchaguzi,* Zanzibar Broadcasting Corporation (ZBC) *Uchaguzi Mkuu,* East African TV *kipindi cha kikaangoni,* TBC Taifa *kipindi cha*

*Tuambie na Jambo Tanzania,* Voice of America *kipindi cha Straight Talk Africa,* BBC *kipindi cha Focus on Africa,* ITV *kipindi cha Mtiti wa Uchaguzi na* Star TV *kipindi cha Tuongee Asubuhi.* Aidha, makala mbalimbali kama vile *Wanawake na Uchaguzi* ambayo ililenga kuhamasisha ushiriki wa Wanawake katika masuala ya Uchaguzi ziliandaliwa na kutolewa katika magazeti. Vile vile, Waandishi wa Habari waliwekewa utaratibu wa kujisajili na kupewa kibali cha kuwaruhusu kuingia katika Vituo vya Kupigia, Kuhesabu Kura na Kutangaza Matokeo.

#### 7.1.1.5 Taasisi na Viongozi wa Dini

Tume ilikutana na Taasisi na Viongozi wa Dini kwa nyakati tofauti kwa lengo la kuwashirikisha na kuwapa taarifa ya mwenendo wa mchakato wa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na Uchaguzi Mkuu. Kupitia mikutano hiyo, Tume iliwasihi Viongozi wa Dini na Taasisi hizo kuwaongoza waumini wao kushiriki Uchaguzi kwa amani na utulivu.

#### 7.1.1.6 Makundi Maalum katika Jamii.

Tume ilikutana na Wawakilishi wa Makundi Maalum katika jamii yaliyojumuisha Watu wenye Ulemavu, Wanawake na Vijana kwa ajili ya mashauriano na kubadilishana mawazo ya jinsi makundi hayo yatakavyojiandikisha kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na watakavyoshiriki katika Uchaguzi.

Katika kuwezesha Makundi hayo kushiriki Uandikishaji na Uchaguzi Mkuu kikamilifu, Tume iliweka utaratibu wa kuwarahisishia ushiriki wao. Mfano watu wasioona walitengenezewa kifaa maalum chenye maandishi ya Nukta Nundu (*Tactile Ballot Folder*) ili kuwawezesha Kupiga Kura wenyewe. Pia, Kituturi kilitengenezwa kwa namna ambayo iliwawezesha Watu wenye Ulemavu wasioweza kusimama Kupiga Kura bila usumbufu. Aidha, Wajawazito, Wazee, Wanawake wenye Watoto Wachanga na Watu wenye Ulemavu walipewa kipaumbele katika Kupiga Kura.

#### 7.1.1.7 Taasisi za Ulinzi na Usalama.

Ili kuhakikisha Uchaguzi unafanyika kwa Amani na Usalama, Tume iliandaa mkutano uliofanyika tarehe 7 Oktoba, 2015 ili kujadili na kuweka mkakati wa kufanikisha azma hiyo. Mkutano huo uliwahusisha Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP), Makamanda wa Polisi wa Mikoa, Waratibu wa Uchaguzi wa Mikoa na Wasimamizi wote wa Uchaguzi. Katika mkutano huo, Tume na Taasisi za Ulinzi na Usalama ziliandaa na kuweka mikakati ya Ulinzi na Usalama wa Vituo vya Kupigia Kura, usindikizaji wa masanduku ya kura, Vituo vya Kujumlishia Kura na Utangazaji matokeo, na ulinzi wa vifaa hasa karatasi za kura.

#### 7.1.1.8 Washirika wa Maendeleo.

Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) kupitia mradi wa DEP, ilishirikiana na Tume katika Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na mchakato wa Uchaguzi Mkuu. Ushiriki wake ulikuwa katika kugharamia fedha za

mafunzo ya kujenga uwezo kwa watendaji wa Uchaguzi na ununuzi wa baadhi ya vifaa vya Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na Uchaguzi Mkuu. Aidha, Mradi wa DEP ulisaidia kugharamia baadhi ya vifaa vilivyotumika katika Kituo cha Mawasiliano (*Call Centre*) kilichoanzishwa na Tume kwa ajili ya kutoa ufafanuzi kwa Wapiga Kura na Wananchi kwa ujumla. Vile vile, UNDP ilishiriki katika kuandaa Mifumo iliyotumiwa na Tume kama vile Mfumo wa Kusajili Watazamaji (*Observer Management System* - OMS) na Mfumo wa Menejimenti ya Matokeo (RMS).

UNDP kupitia mradi wake wa DEP iligharamia mikutano mbalimbali ya Tume na wadau. Pia, iligharamia Kituo cha kutangazia matokeo ya Rais na Kituo cha kusajili Watazam

**7.1.1.9 Watazamaji wa Uchaguzi**

Tume ilitoa mialiko kwa Watazamaji wa ndani na nje ya nchi kwa lengo la kutazama Uchaguzi Mkuu. Jumla ya Taasisi na Asasi **124** za ndani zilipewa kibali cha kuwa Watazamaji wa Uchaguzi. Aidha, Mashirika **34** ya Kimataifa na Balozi za Nchi mbalimbali zilipewa vibali vya kuwa Watazamaji wa Kimataifa wa Uchaguzi. Maelezo zaidi kuhusiana na Watazamaji wa Uchaguzi yanapatikana katika Sura ya Nane.

## SURA YA NANE

## WATAZAMAJI WA UCHAGUZI

### 8.1 Utazamaji wa Uchaguzi

Utazamaji wa Uchaguzi ni dhana inayohusu ushirikishwaji wa wadau mbalimbali katika Uchaguzi ili kutazama namna mchakato wa Uchaguzi unavyoendeshwa. Lengo kuu la kuwaruhusu Watazamaji lilikuwa ni kudhihirisha dhana ya Uchaguzi ulio **Huru**, **Wazi** na wa **Haki** kuwa imetekelezwa.

Sehemu ya V ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka, 2015 na Sehemu ya IV ya Kanuni za Uchaguzi wa Madiwani za mwaka, 2015 zinaweka msingi wa dhana nzima ya Watazamaji wa Uchaguzi kwa kuyazungumzia masuala yote muhimu yanayohusu Watazamaji wa Uchaguzi na namna Tume inavyotakiwa kusimamia na kuliendesha zoezi hilo.

#### 8.1.1 Kamati ya Watazamaji na Mashirika ya Kimataifa

Tume iliunda Kamati ya Kuratibu Utazamaji wa Uchaguzi, wajumbe wa kamati hii waliteuliwa na Tume kutoka Taasisi mbalimbali za Serikali na Vyama vya Siasa. Mara baada ya Tume kuanza utoaji wa vibali na usajili, Kamati ya Kitaifa ya Watazamaji ilikuwa na jukumu la kukutana mara kwa mara, ili kujadili masuala mbalimbali yahusuyo Watazamaji, ikiwemo mwenendo wao na iwapo wanafanya shughuli za utazamaji kwa kuzingatia Sheria za Uchaguzi, Maelekezo kwa Watazamaji wa Ndani na wa Kimataifa na Sheria nyingine za nchi kwa ujumla.

#### 8.1.2 Mialiko kwa Watazamaji wa Uchaguzi

Tume ilitoa mialiko kwa Taasisi na Mashirika ya ndani kupitia matangazo katika Vyombo vya Habari na taasisi za nje ya nchi kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa ajili ya kutazama Uchaguzi Mkuu. Vile vile, Tume iliandika barua kwa Tume za Uchaguzi marafiki na Mashirika ya Kikanda ambayo yana uhusiano na Tume, ili washiriki katika kutazama Uchaguzi.

Mara baada ya kuwatangazia wadau hao, Tume ilipokea maombi ya kuwa Watazamaji kutoka kwa taasisi za ndani na nje ya nchi zipatazo **179.**

#### 8.1.3 Usajili wa Watazamaji wa Uchaguzi

Tume iliandaa Kituo cha Kusajili Watazamaji ambacho kilikuwa katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere. Katika Kituo hicho, Taasisi na Mashirika yote yaliyotoka nje ya nchi pamoja na taasisi za ndani zilizopo Dar Es Salaam zilisajiliwa. Tume ilitumia Mfumo wa Kusajili Watazamaji wa Uchaguzi (*Observer Management System* – OMS) katika kusajili na kutoa vitambulisho vya Watazamaji wa Uchaguzi.

Tume ilisajili jumla ya taasisi za ndani **124** kuwa Watazamaji. Taasisi hizo zilikuwa na jumla ya Watazamaji **10,500**. Hata hivyo, katika kutekeleza zoezi hilo kwa ufanisi na wakati, Tume iliweka utaratibu wa kutoa vitambulisho na nyaraka mbalimbali kwa Taasisi zilizokuwa nje ya Dar Es Salaam kupitia Wasimamizi wa Uchaguzi katika Halmashauri husika. Kwa upande wa Taasisi za Kimataifa, zilisajiliwa Taasisi **34** ambazo zilikuwa na Watazamaji **700** ambao walifanyiwa Usajili na kupatiwa vitambulisho na Tume ya Taifa ya Uchaguzi Makao Makuu.

Aidha, Kituo kilisajili Mashirika na Vyombo vya Habari vilivyotaka kuripoti habari za Uchaguzi. Wanahabari **4,223** kutoka Vyombo vya Habari **83** walisajiliwa na kupatiwa Vitambulisho.




*Watazamaji wa Uchaguzi kutoka Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) wakiwa katika moja ya Mikutano ya kupeana Taarifa kuhusu Uchaguzi Mkuu 2015.*

### 8.1.4 Kuongeza Muda wa Utazamaji wa Uchaguzi

Kutokana na kuahirishwa kwa Uchaguzi wa Ubunge na Udiwani katika baadhi ya majimbo na kata, Tume ilipanga tarehe nyingine za Uchaguzi baada ya tarehe 25 Oktoba, 2015. Kwa kuwa muda wa awali wa vibali vya utazamaji ulikuwa umekwisha, Tume iliongeza muda wa utazamaji kwa Taasisi za Umoja wa Jumuiya ya Ulaya, Ubalozi wa Uingereza, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, East Africa Nguvu Kazi and Juakali Partners**,** Women -Widow Children and Fisheries Development Association na Tanganyika Centre For Development and Advocacy (TCDA) ambazo ziliomba kuongezewa muda wa utazamaji.

### 8.1.5 Mikutano ya Tume na Watazamaji wa Uchaguzi

Tume ilifanya mikutano na Watazamaji wa Uchaguzi kabla na wakati wa Uchaguzi ili kuwafahamisha juu ya maandalizi ya Uchaguzi Mkuu, Sheria za Uchaguzi na Kanuni zake, Maelekezo kwa Watazamaji, usalama wa nchi na hali ya hewa. Aidha, Tume iliwapatia Watazamaji Sheria za Uchaguzi na Kanuni zake, vitabu vya Maelekezo kwa Watazamaji, orodha na ramani za majimbo na orodha ya vituo vya kupigia kura.

## 8.2 Maoni na Ushauri wa Watazamaji wa Uchaguzi

Kwa mujibu wa Maelekezo kwa Watazamaji wa Uchaguzi, Kanuni ya 10(b), Watazamaji wa Uchaguzi wanatakiwa kuwasilisha taarifa za awali za utazamaji mara baada ya uchaguzi kukamilika. Taarifa kamili za utazamaji wa uchaguzi zinatakiwa ziwasilishwe ndani ya miezi mitatu baada ya kutangazwa kwa Matokeo. Hata hivyo, hadi Taarifa hii inaandikwa, ni Taasisi **13** tu kati ya **158** za Ndani na za Kimataifa zimewasilisha taarifa zao kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Kwa ujumla Taarifa zilizowasilishwa zina maoni kwamba Uchaguzi ulikuwa ni **Huru, Wazi** na wa **Haki**. Pamoja na maoni hayo ya jumla, walikuwa na ushauri ufuatao kwa Tume:

(i) Umuhimu wa kufanya zoezi la Uboreshaji wa Daftari mara kwa mara kati ya Chaguzi moja na nyingine;

(ii) Kuifanyia kazi Sheria ya Uchaguzi ili kuruhusu Watanzania waishio nje ya nchi kupiga Kura;

(iii) Tume kuimarisha mipango na mfumo wake wa usambazaji wa vifaa ili kuhakikisha vifaa vinafika kwa wakati; na

(iv) Kuboresha miundombinu ya vituoni na rasilimali watu kwa Wasimamizi na Watendaji mbalimbali wa Vituo vya Kupigia Kura.

Tume inatoa shukrani za dhati kwa Taasisi zote za ndani na za Kimataifa zilizofanya kazi ya Utazamaji wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. Aidha, Tume inatoa shukrani za kipekee kwa Taasisi za Watazamaji wa Uchaguzi ambazo mara baada ya kumalizika kwa zoezi la Uchaguzi Mkuu ziliwasilisha taarifa za Utazamaji. Tume pia, inatoa wito kwa Taasisi za Watazamaji kuwa zinawasilisha taarifa zao kwa wakati kwa sababu ni matakwa ya kisheria.

## SURA YA TISA

## TATHMINI BAADA YA UCHAGUZI MKUU

### 9.1 Tathmini ya Uchaguzi.

Tume ilifanya Tathmini Baada ya Uchaguzi Mkuu kuanzia tarehe 1 Februari, 2016 mpaka tarehe 26 Februari, 2016. Tathmini hii ni ya kwanza kufanyika tangu Tume ilipoanzishwa. Lengo la Tathmini lilikuwa kupata mrejesho wa namna Tume ilivyotekeleza zoezi zima la Uchaguzi Mkuu. Mrejesho wa tathmini hiyo, umeiwezesha Tume kujua mafanikio na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa majukumu yake Kabla, Wakati na Baada ya Uchaguzi. Sura hii inatoa matokeo ya Awali ya Tathmini, taarifa rasmi ya Tathmini itatolewa na Tume.

### 9.2 Maeneo ya Tathmini

Tathmini ilifanyika katika Mikoa **22** kati ya Mikoa **30** ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mikoa **20** ilikuwa ya Tanzania Bara na Mikoa **2** ya Tanzania Zanzibar. Halmashauri **60** kwa Tanzania Bara na Wilaya **4** kwa upande wa Tanzania Zanzibar zilihusika katika Tathmini hiyo. Aidha, katika kila Halmashauri/Wilaya zilihusishwa Kata/Shehia **3**. **Ramani Na. 4** inaonesha Halmashauri/Wilaya zilizofanyiwa Tathmini Baada ya Uchaguzi Mkuu wa 2015.

**Ramani Na. 4: Halmashauri zilizofanyiwa Tathmini Baada ya Uchaguzi**



## 9.3 Njia Zilizotumika Kufanya Tathmini

Katika kufanya tathmini, njia 2 zilitumika ambazo ni mahojiano ya ana kwa ana kwa kutumia dodoso na majadiliano kwa makundi ya wazee na vijana kwa kutumia Fomu maalum iliyotumika kuchukua hoja, maoni na mapendekezo kutoka katika majadiliano hayo.

Jumla ya watu **1,915** walihojiwa kati yao **1,029** walikuwa watendaji wa Uchaguzi, **499** Wapiga Kura na **387** walikuwa Watumishi wa Umma**.** Kati ya watu waliohojiwa wanaume walikuwa **1,184** sawa na asilimia **62** na wanawake **731** sawa na asilimia **38.** Mahojiano yalifanyika kwa kutumia dodoso kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 30**. Aidha, mchanganuo wa waliohojiwa kwa kuzingatia umri unaonesha kuwa Vijana (miaka **18 – 35**) walikuwa **767** sawa na asilimia **40**, umri kati ya miaka **36 – 60** asilimia **57** na umri zaidi ya miaka **60** walikuwa **63** sawa na asilimia **3** kama inavyoonesha kwenye **Jedwali Na. 31**.

**Jedwali Na. 30: Aina na Idadi ya Waliohojiwa kwa Jinsi**

| Na. | Waliohojiwa | Jinsi | | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| | | Wanaume | Wanawake | |
| 1. | Watendaji wa Uchaguzi | 670 | 359 | **1,029** |
| 2. | Wapiga Kura | 311 | 188 | **499** |
| 3. | Watumishi wa Umma | 203 | 184 | **387** |
| | **Jumla** | **1,184** | **731** | **1,915** |

**Jedwali Na. 31: Mgawanyo wa Waliohojiwa kwa Umri**

| Na. | Waliohojiwa | Umri | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 18-35 | 36-60 | Zaidi 60 | |
| 1. | Watendaji wa Uchaguzi | 451 | 575 | 3 | **1,029** |
| 2. | Wapiga Kura | 166 | 273 | 60 | **499** |
| 3. | Watumishi wa Umma | 150 | 237 | 0 | **387** |
| | **Jumla** | **767** | **1,085** | **63** | **1,915** |



*Afisa wa Tume akifanya mahojiano ya ana kwa ana kwa kutumia dodoso na mmoja wa Wapiga Kura katika Kata ya Nyasura, Bunda Mjini.*

Njia ya majadiliano kwa makundi maalum (*Focused Group Discussion - FGD*) ilitumika. Makundi hayo yalijumuisha watu wenye umri wa zaidi ya miaka 60 na wale wenye umri wa kati ya miaka 18 hadi 35. Majadiliano hayo yalilenga katika maeneo yafuatayo:-

(i) Zoezi la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura;

(ii) Zoezi la Uwekaji wazi wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura;

(iii) Kampeni za Wagombea zilivyoendeshwa;

(iv) Zoezi la Uchaguzi Mkuu ulivyoendeshwa; na

(v) Uhesabuji, Ujumlishaji, na Utoaji wa Matokeo ya Rais, Wabunge na Madiwani.

Njia hii ya majadiliano kwa makundi hayo ilifanyika katika kila Kata iliyofanyiwa Tathmini. Aidha, kila kundi lilihusisha Wapiga Kura 10 wakiwemo Wanawake 5 na Wanaume 5.



*Maafisa wa Tume wakifanya majadiliano na Vijana Kutathmini Uchaguzi Mkuu katika Kata ya Bwiru, Wilaya ya Ilemela Mkoani Mwanza.*

### 9.4 Vigezo Vilivyotumika Kuchagua Maeneo ya Kufanyia Tathmini.

Katika utekelezaji wa zoezi la Tathmini kuhusu Uchaguzi Mkuu, Tume iliainisha maeneo ya kufanyia Tathmini kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo:-

(i) Maeneo ambayo mwitikio wa Wapiga Kura ulikuwa kati ya asilimia 38 – 55, ikilinganishwa na idadi ya Wapiga Kura waliojiandikisha kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura;

(ii) Maeneo ambayo mwitikio wa Wapiga Kura ulikuwa kati ya asilimia 69 – 70, ikilinganishwa na idadi ya Wapiga Kura walioandikishwa kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura;

(iii) Maeneo ambayo mwitikio wa Wapiga Kura ulikuwa kati ya asilimia 78 – 83, ikilinganishwa na idadi ya Wapiga Kura walioandikishwa kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura;

(iv) Maeneo ambayo yaliyoonekana kuwa na ushindani mkubwa wa kisiasa;

(v) Maeneo yaliyoathiriwa na hali mbaya ya hewa wakati wa Uchaguzi; na

(vi) Ugumu wa baadhi ya maeneo kufikika kutokana na jiografia ya maeneo husika.

### 9.5 Matokeo ya Awali ya Tathmini

Kwa muhtasari matokeo ya awali ya tathmini yameonesha kuwa asilimia **76.4** ya waliohojiwa katika maeneo yaliyofanyiwa Tathmini wana uelewa mzuri kuhusu Elimu ya Mpiga Kura. Hata hivyo, Tathmini hiyo inaonesha kwamba, asilimia **23.6** ya waliohojiwa hawana uelewa mzuri kuhusu Elimu ya Mpiga Kura kama inavyooneshwa kwenye **Chati Na. 10.** Hali hii inaonesha kuwa, kuna haja ya kuweka mikakati madhubuti kwenye suala zima la Elimu ya Mpiga Kura.

**Chati Na. 10: Uelewa kuhusu Elimu ya Mpiga Kura**



Tathmini pia, imebaini kuwa katika maeneo yaliyofanyiwa tathmini asilimia **7.0** ya waliohojiwa, walionesha kuwa Wapiga Kura hutumia zaidi ya dakika 60 katika kufika Kituo cha Kupigia Kura. Asilimia **17.5** ya Wahojiwa hutumia dakika 30 hadi 60 kufika Kituo cha kupigia Kura na asilimia **75.6** ya Wahojiwa ndiyo waliokuwa wakitumia chini ya dakika 30 kufika katika Kituo cha Kupigia Kura kama inavyoonesha kwenye **Chati Na. 11**.

**Chati Na. 11: Wastani wa muda waliotumia Wapiga Kura kufika katika Kituo cha Kupigia Kura**




Katika maeneo yenye mazingira magumu hususan, maeneo ya wafugaji yalionesha kuwa na changamoto hiyo kutokana na mtawanyiko wa kaya moja hadi nyingine. Pia, ilibainika kuwa wafugaji huhama kutoka eneo moja hadi jingine hasa msimu wa kiangazi kwa ajili ya kutafuta malisho ya mifugo yao. Hii, husababisha wakati wa Uchaguzi kutoweza Kupiga Kura.

Katika majadiliano yaliyofanyika kwa makundi ya wazee na vijana, hoja mbalimbali zilitolewa. Baadhi ya hoja hizo zililenga maeneo yafuatayo:-

(i) Elimu ya Mpiga Kura iliwafikia Wapiga Kura wachache kwenye maeneo ya vijijini;

(ii) Baadhi ya Wapiga Kura kushindwa kupiga Kura kutokana na kuhamia maeneo mengine tofauti na walipojiandikishia; na

(iii) Katika baadhi ya maeneo Wapiga Kura kushindwa kufika katika vituo vya kupigia kura kutokana na kuharibika kwa miundombinu wakati wa mvua.

## SURA YA KUMI

## MAFANIKIO NA CHANGAMOTO

### 10.1 Mafanikio

Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilifanikiwa kuendesha Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, kwa Amani na Utulivu. Uchaguzi huo pia ulikuwa **Huru,** wa **Haki** na wa **Wazi**. Kwa ujumla, Taarifa za Watazamaji wa Uchaguzi zimethibitisha jambo hili. Aidha, mafanikio mengine ni;-

(i) Kuandikisha Wapiga Kura **23,161,440** kwa kipindi kifupi (miezi 6 tu) kuanzia tarehe 23 Februari hadi tarehe 4 Agosti, 2015 na kuwa na Daftari lililotumika katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika tarehe 25 Oktoba, 2015;

(ii) Kusafirisha vifaa vya uboreshaji na vile vya Uchaguzi kwa ufanisi mkubwa;

(iii) Wapiga Kura waliojitokeza mwaka 2015 ni **15,596,110** sawa na asilimia **67.34** walijitokeza Kupiga Kura. Idadi hii ni kubwa ikilinganishwa na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 ambapo waliojitokeza Kupiga Kura walikuwa **8,626,303** sawa na asilimia **42.84;**

(iv) Kutangaza Matokeo ya Kiti cha Rais ndani ya saa 72 kama Tume ilivyopanga;

(v) Kushirikiana na wadau wa uchaguzi hatua kwa hatua kupitia mikutano mbalimbali ili kuwajulisha mchakato ulivyokuwa unaendelea katika kuelekea Uchaguzi Mkuu na kupata maoni yao; na

(vi) Kwa mara ya kwanza Tume imefanikiwa kufanya zoezi la Tathmini Baada ya Uchaguzi *(Post Election Evaluation).*

### 10.2 Changamoto

Pamoja na mafanikio hayo, zilikuwepo changamoto kadhaa ambazo zimegawanyika katika maeneo makuu mawili:

(i) Wakati wa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, na

(ii) Wakati wa Uchaguzi Mkuu.

### 10.2.1 Changamoto Wakati wa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura

(i) Kuchelewa kwa fedha, kulisababisha Tume kushindwa kufanya Uboreshaji mara mbili baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 na kabla ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, kama Sheria inavyoelekeza. Badala yake Uboreshaji ulifanyika mara moja tu;

(ii) Baadhi ya watu kutoa taarifa za uongo ili kujiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura;

(iii) Tatizo la miundombinu lilichangia kufanya Uboreshaji kuwa mgumu kama vile usafirishaji wa BVR *Kits* na vifaa vya uboreshaji kutoka eneo moja hadi jingine;

(iv) Tume kutokuwa na fedha za kutosha kwa ajili ya kutolea Elimu ya Mpiga Kura na mafunzo kwa Waandikishaji waliotumia BVR *Kits* wakati wa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura;

(v) Matumizi ya teknolojia mpya ya BVR yalihitaji Watendaji wenye weledi zaidi kuliko walioweza kupatikana kwenye maeneo mengi;

(vi) Kufanyika kwa mabadiliko ya mipaka ya kiutawala baada ya zoezi la uandikishaji au ugawaji wa maeneo ya Uchaguzi kumalizika kuliathiri zoezi la uandaaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, Uteuzi wa Wagombea na Upigaji Kura;

(vii) Uchache wa BVR *Kits.* Tume ilihitaji jumla ya BVR *Kits* 15,000 ili kufanikisha zoezi la uandikishaji mapema. Hata hivyo, Tume ilipatiwa fedha kwa ajili ya kununulia BVR *Kits* 8,000 tu. Tume ilipata BVR *Kits* hizi kwa awamu. Hivyo, Tume ililazimika kuanza zoezi la Uandikishaji kwa kutumia BVR *Kits* 250 tu; na

(viii) Baadhi ya Viongozi wa Vyama vya Siasa kutoa taarifa za kupotosha kuhusu zoezi la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

### 10.2.2 Changamoto Wakati wa Uchaguzi Mkuu

Pamoja na kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Katiba na Sheria, Tume ilikabiliana na changamoto zifuatazo:-

(i) Fedha kutopatikana kwa wakati ambapo kulisababisha baadhi ya majukumu na maandalizi mengine muhimu ya uchaguzi kuchelewa kutekelezwa;

(ii) Ukiukwaji wa Maadili na Sheria za Uchaguzi kwa baadhi ya Vyama vya Siasa, Wagombea na Watazamaji;

(iii) Kuharibiwa kwa vifaa vya uchaguzi katika baadhi ya maeneo kulisababisha Uchaguzi kuchelewa kuanza na kuahirishwa katika baadhi ya maeneo;

(iv) Tume kutokuwa na fedha kwa ajili ya kuwezesha Asasi za Kiraia zinazopewa kibali kwa ajili ya kutoa Elimu ya Mpiga Kura;

(v) Tume kutokuwa na ofisi na watendaji hadi ngazi ya halmashauri na pia kutokuwa na ofisi upande wa Tanzania Zanzibar;

(vi) Watumishi wa Halmashauri walioteuliwa na Tume kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya uchaguzi kuhamishwa katikati ya Zoezi la Uchaguzi;

(vii) Kutokuwepo kwa Sheria ya Tume ambayo ingebainisha Muundo wa Tume na namna ya kutekeleza majukumu yake kikatiba kumeathiri utekelezaji wa majukumu hayo;

(viii) Baadhi ya wadau wa uchaguzi kutokuwa na imani na Tume kwa kuamini kuwa sio taasisi huru katika kutekeleza majukumu yake;

(ix) Baadhi ya Vyombo vya Habari kuripoti habari za uchaguzi kwa kupotosha kutokana na kuwa na mrengo wa Vyama vya Siasa;

(x) Kuwepo kwa Sheria zaidi ya moja zinazosimamia uchaguzi, kama Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Sheria ya Uchaguzi kwa Tanzania Zanzibar; na

(xi) Watazamaji wa Uchaguzi kutofuata Muongozo wa Watazamaji na kuingilia majukumu ya Tume.

## SURA YA KUMI NA MOJA

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 11.1 Hitimisho

Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, ulikuwa ni wa kipekee kwani ndiyo Uchaguzi wa kwanza nchini Tanzania ambao ulihusisha Uandikishaji wa Wapiga Kura kwa njia ya Kielekitroniki na uliokuwa na ushindani mkubwa wa kisiasa. Tume iliweza kufanikisha zoezi la Uandikishaji kwa kuandikisha Wapiga Kura **23,161,440** kwa muda mfupi (miezi sita) kwa kutumia BVR *Kits* **8,000** tu.

Zoezi la Uchaguzi Mkuu liliendeshwa kwa hali ya amani na utulivu kuanzia kipindi cha Kampeni hadi Siku ya Kupiga Kura. Hali hii, iliwezesha wananchi kuhudhuria mikutano ya kampeni za uchaguzi na Wapiga Kura kushiriki Kupiga Kura.

Kwa ujumla uchaguzi huo ulikuwa Huru, Wazi na wa Haki. Hili limethibitishwa na wadau mbalimbali wa Uchaguzi, wakiwemo Watazamaji wa Uchaguzi wa ndani na nje ya nchi. Vile vile, Tathmini Baada ya Uchaguzi Mkuu iliyofanywa na Tume kwa wadau mbalimbali wa uchaguzi ilibainisha hilo.

Mafanikio katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, kwa kiasi kikubwa yalitokana na utekelezaji mzuri wa Mpango Mkakati uliowekwa na Tume, ambao ulihusisha ushirikishwaji wa wadau mbalimbali wa uchaguzi kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa.

Pamoja na Uchaguzi Mkuu kufanyika kwa mafanikio makubwa, baadhi ya changamoto zilijitokeza kwenye zoezi la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kama vile Ugawaji wa Mipaka ya Kiutawala uliofanywa muda mfupi kabla ya Uchaguzi Mkuu kufanyika.

Kwa kawaida, Wagombea wasioridhika na matokeo ya uchaguzi wanapewa fursa ya kufungua malalamiko ya uchaguzi Mahakama Kuu kwa Uchaguzi wa Ubunge na Mahakama za Mahakimu Wakazi kwa Uchaguzi wa Madiwani. Katika ngazi ya Ubunge jumla ya malalamiko **52** yalifunguliwa. Aidha, kwa upande wa Udiwani malalamiko **194** yalifunguliwa.

### 11.2 Mapendekezo

Ili kuboresha shughuli za uendeshaji uchaguzi, Tume inapendekeza yafuatayo;-

**(i) Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi**

Kutungwa kwa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi ambayo itaiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake ya kikatiba kwa ufanisi zaidi kama ambavyo imefanyika katika nchi nyingine.

**(ii) Kurejesha Mfuko wa Uchaguzi**

Ili kuhakikisha kuwa Tume inaendesha shughuli zake kikamilifu ni vema kurejesha mfuko wa Kudumu wa Uchaguzi ambao utatengewa fedha kutoka bajeti ya Serikali ya kila mwaka. Hii, itawezesha Tume kutekeleza shughuli kama Uboreshaji wa Daftari na ununuzi wa Vifaa kwa wakati.

**(iii) Tume kuwa na Ofisi zake katika Ngazi ya Halmashauri**

Ili Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura uweze kufanikiwa na shughuli nyingine za uchaguzi kuendeshwa kwa ufanisi zaidi, inapendekezwa kuwa na ofisi zake katika ngazi ya halmashauri.

**(iv) Ofisi za Tume Tanzania Zanzibar**

Tume inapendekeza kuanzishwa kwa ofisi za kudumu kwa upande wa Tanzania Zanzibar ili kuendeleza shughuli zake.

**(v) Jengo la Kudumu la Ofisi ya Tume**

Tume kutokuwa na jengo la kudumu la ofisi inaathiri utendaji kwa kuwa watumishi wanalazimika kuwa na ofisi sehemu mbalimbali na hivyo kuathiri utendaji na kusababisha gharama za uendeshaji kuwa kubwa. Tume inahitaji kuwa na jengo la kudumu litakalokidhi mahitaji yake.

**(vi) Kugharamia Elimu ya Mpiga Kura**

Tume itengewe fedha za kutosha kwa ajili ya kutoa Elimu ya Mpiga Kura kila mwaka.

**(vii) Ugawaji wa Mipaka ya Kiutawala**

Tume inapendekeza ugawaji wa Halmashauri na Kata, ufanyike miezi sita ya Uchaguzi.

## VIAMBATISHO

### Kiambatisho Na. 1: Orodha ya Vyama vya Siasa vyenye Usajili wa Kudumu

| Na. | CHAMA CHA SIASA |
|---|---|
| 1. | Alliance for Change and Transparency- Wazalendo (ACT-Wazalendo) |
| 2. | African Democratic Alliance - Tanzania Democratic Alliance (ADA – TADEA) |
| 3. | Alliance for Democratic Change (ADC) |
| 4. | Alliance for Tanzanian Farmers Party (AFP) |
| 5. | African Progress Party of Tanzania - Maendeleo (APPT – Maendeleo) |
| 6. | Chama Cha Kijamii (CCK) |
| 7. | Chama Cha Mapinduzi (CCM) |
| 8. | Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) |
| 9. | Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA) |
| 10. | Chama cha Haki na Ustawi Tanzania (CHAUSTA) |
| 11. | Civic United Front (CUF) |
| 12. | DEMOKRASIA MAKINI |
| 13. | Democratic Party (DP) |
| 14. | JAHAZI ASILIA |
| 15. | National Convention for Construction and Reform – Mageuzi (NCCR-Mageuzi) |
| 16. | National League for Democracy (NLD) |
| 17. | National Reconstruction Alliance (NRA) |
| 18. | Sauti ya Umma (SAU) |
| 19. | Tanzania Labour Party (TLP) |
| 20. | United Democratic Party (UDP) |
| 21. | Union for Multiparty Democracy (UMD) |
| 22. | United People’s Democratic Party (UPDP) |

**Kiambatisho Na. 2: Orodha ya Majimbo ya Uchaguzi**

| Na. | MKOA | HALMASHAURI | Na | JIMBO |
|---|---|---|---|---|
| 1. | ARUSHA | MANISPAA YA ARUSHA | 1. | ARUSHA MJINI |
| | | WILAYA YA ARUSHA | 2. | ARUMERU MAGHARIBI |
| | | WILAYA YA KARATU | 3. | KARATU |
| | | WILAYA YA LONGIDO | 4. | LONGIDO |
| | | WILAYA YA MERU | 5. | ARUMERU MASHARIKI |
| | | WILAYA YA MONDULI | 6. | MONDULI |
| | | WILAYA YA NGORONGORO | 7. | NGORONGORO |
| 2. | DAR ES SALAAM | MANISPAA YA ILALA | 8. | SEGEREA |
| | | MANISPAA YA KINONDONI | 9. | KAWE |
| | | MANISPAA YA ILALA | 10. | ILALA |
| | | MANISPAA YA ILALA | 11. | UKONGA |
| | | MANISPAA YA KINONDONI | 12. | KIBAMBA |
| | | MANISPAA YA KINONDONI | 13. | KINONDONI |
| | | MANISPAA YA KINONDONI | 14. | UBUNGO |
| | | MANISPAA YA TEMEKE | 15. | KIGAMBONI |
| | | MANISPAA YA TEMEKE | 16. | MBAGALA |
| | | MANISPAA YA TEMEKE | 17. | TEMEKE |
| 3. | DODOMA | WILAYA YA KONDOA | 18. | KONDOA |
| | | MANISPAA YA DODOMA | 19. | DODOMA MJINI |
| | | MJI KONDOA | 20. | KONDOA MJINI |
| | | WILAYA YA BAHI | 21. | BAHI |
| | | WILAYA YA CHAMWINO | 22. | CHILONWA |
| | | WILAYA YA CHAMWINO | 23. | MTERA |
| | | WILAYA YA CHEMBA | 24. | CHEMBA |
| | | WILAYA YA KONGWA | 25. | KONGWA |
| | | WILAYA YA MPWAPWA | 26. | KIBAKWE |
| | | WILAYA YA MPWAPWA | 27. | MPWAPWA |
| 4. | GEITA | WILAYA YA GEITA | 28. | BUSANDA |
| | | MJI WA GEITA | 29. | GEITA MJINI |
| | | WILAYA YA NYANG'HWALE | 30. | NYANG'HWALE |
| | | WILAYA YA BUKOMBE | 31. | BUKOMBE |

| Na. | MKOA | HALMASHAURI | Na | JIMBO |
|---|---|---|---|---|
| | | WILAYA YA CHATO | 32. | CHATO |
| | | WILAYA YA GEITA | 33. | GEITA |
| | | WILAYA YA MBOGWE | 34. | MBOGWE |
| 5. | IRINGA | MANISPAA YA IRINGA | 35. | IRINGA MJINI |
| | | MJI WA MAFINGA | 36. | MAFINGA MJINI |
| | | WILAYA YA IRINGA | 37. | ISIMANI |
| | | WILAYA YA IRINGA | 38. | KALENGA |
| | | WILAYA YA KILOLO | 39. | KILOLO |
| | | WILAYA YA MUFINDI | 40. | MUFINDI KASKAZINI |
| | | WILAYA YA MUFINDI | 41. | MUFINDI KUSINI |
| 6. | KAGERA | WILAYA YA MULEBA | 42. | MULEBA KUSINI |
| | | MANISPAA YA BUKOBA | 43. | BUKOBA MJINI |
| | | WILAYA YA BIHARAMULO | 44. | BIHARAMULO MAGHARIBI |
| | | WILAYA YA BUKOBA | 45. | BUKOBA VIJIJINI |
| | | WILAYA YA KARAGWE | 46. | KARAGWE |
| | | WILAYA YA KYERWA | 47. | KYERWA |
| | | WILAYA YA MISSENYI | 48. | NKENGE |
| | | WILAYA YA MULEBA | 49. | MULEBA KASKAZINI |
| | | WILAYA YA NGARA | 50. | NGARA |
| 7. | KASKAZINI PEMBA | WILAYA YA MICHEWENI | 51. | WINGWI |
| | | WILAYA YA MICHEWENI | 52. | KONDE |
| | | WILAYA YA MICHEWENI | 53. | MICHEWENI |
| | | WILAYA YA MICHEWENI | 54. | TUMBE |
| | | WILAYA YA WETE | 55. | GANDO |
| | | WILAYA YA WETE | 56. | KOJANI |
| | | WILAYA YA WETE | 57. | MGOGONI |
| | | WILAYA YA WETE | 58. | MTAMBWE |
| | | WILAYA YA WETE | 59. | WETE |
| 8. | KASKAZINI UNGUJA | WILAYA YA KASKAZINI B | 60. | MAHONDA |
| | | WILAYA YA KASKAZINI A | 61. | CHAANI |
| | | WILAYA YA KASKAZINI A | 62. | KIJINI |
| | | WILAYA YA KASKAZINI A | 63. | MKWAJUNI |

| Na. | MKOA | HALMASHAURI | Na | JIMBO |
|---|---|---|---|---|
| | | WILAYA YA KASKAZINI A | 64. | NUNGWI |
| | | WILAYA YA KASKAZINI A | 65. | TUMBATU |
| | | WILAYA YA KASKAZINI B | 66. | BUMBWINI |
| | | WILAYA YA KASKAZINI B | 67. | DONGE |
| | | WILAYA YA KASKAZINI B | 68. | KIWENGWA |
| 9. | KATAVI | WILAYA YA MPIMBWE | 69. | KAVUU |
| | | MANISPAA YA MPANDA | 70. | MPANDA MJINI |
| | | WILAYA YA MLELE | 71. | KATAVI |
| | | WILAYA YA MPANDA | 72. | MPANDA VIJIJINI |
| | | WILAYA YA NSIMBO | 73. | NSIMBO |
| 10. | KIGOMA | WILAYA YA UVINZA | 74. | KIGOMA KUSINI |
| | | MANISPAA YA KIGOMA UJIJI | 75. | KIGOMA MJINI |
| | | MJI WA KASULU | 76. | KASULU MJINI |
| | | WILAYA YA BUHIGWE | 77. | BUHIGWE |
| | | WILAYA YA KAKONKO | 78. | BUYUNGU |
| | | WILAYA YA KASULU | 79. | KASULU VIJIJINI |
| | | WILAYA YA KIBONDO | 80. | MUHAMBWE |
| | | WILAYA YA KIGOMA | 81. | KIGOMA KASKAZINI |
| 11. | KILIMANJARO | WILAYA YA SAME | 82. | SAME MASHARIKI |
| | | MANISPAA YA MOSHI | 83. | MOSHI MJINI |
| | | WILAYA YA HAI | 84. | HAI |
| | | WILAYA YA MOSHI | 85. | MOSHI VIJIJINI |
| | | WILAYA YA MOSHI | 86. | VUNJO |
| | | WILAYA YA MWANGA | 87. | MWANGA |
| | | WILAYA YA ROMBO | 88. | ROMBO |
| | | WILAYA YA SAME | 89. | SAME MAGHARIBI |
| | | WILAYA YA SIHA | 90. | SIHA |
| 12. | KUSINI PEMBA | WILAYA YA CHAKECHAKE | 91. | CHAKECHAKE |
| | | WILAYA YA CHAKECHAKE | 92. | CHONGA |
| | | WILAYA YA CHAKECHAKE | 93. | OLE |
| | | WILAYA YA CHAKECHAKE | 94. | WAWI |
| | | WILAYA YA | 95. | ZIWANI |

| Na. | MKOA | HALMASHAURI | Na | JIMBO |
|---|---|---|---|---|
| | | CHAKECHAKE | | |
| | | WILAYA YA MKOANI | 96. | CHAMBANI |
| | | WILAYA YA MKOANI | 97. | KIWANI |
| | | WILAYA YA MKOANI | 98. | MKOANI |
| | | WILAYA YA MKOANI | 99. | MTAMBILE |
| 13. | KUSINI UNGUJA | WILAYA YA KATI | 100 | CHWAKA |
| | | WILAYA YA KATI | 101 | TUNGUU |
| | | WILAYA YA KATI | 102 | UZINI |
| | | WILAYA YA KUSINI | 103 | MAKUNDUCHI |
| | | WILAYA YA KUSINI | 104 | PAJE |
| 14. | LINDI | MANISPAA YA LINDI | 105 | LINDI MJINI |
| | | WILAYA YA KILWA | 106 | KILWA KASKAZINI |
| | | WILAYA YA KILWA | 107 | KILWA KUSINI |
| | | WILAYA YA LINDI | 108 | MCHINGA |
| | | WILAYA YA LINDI | 109 | MTAMA |
| | | WILAYA YA LIWALE | 110 | LIWALE |
| | | WILAYA YA NACHINGWEA | 111 | NACHINGWEA |
| | | WILAYA YA RUANGWA | 112 | RUANGWA |
| 15. | MANYARA | MJI WA BABATI | 113 | BABATI MJINI |
| | | WILAYA YA HANANG | 114 | HANANG |
| | | MJI WA MBULU | 115 | MBULU MJINI |
| | | WILAYA YA BABATI | 116 | BABATI VIJIJINI |
| | | WILAYA YA KITETO | 117 | KITETO |
| | | WILAYA YA MBULU | 118 | MBULU VIJIJINI |
| | | WILAYA YA SIMANJIRO | 119 | SIMANJIRO |
| 16. | MARA | MJI WA BUNDA | 120 | BUNDA MJINI |
| | | MJI WA TARIME | 121 | TARIME MJINI |
| | | MANISPAA YA MUSOMA | 122 | MUSOMA MJINI |
| | | WILAYA YA BUNDA | 123 | BUNDA |
| | | WILAYA YA BUNDA | 124 | MWIBARA |
| | | WILAYA YA BUTIAMA | 125 | BUTIAMA |
| | | WILAYA YA MUSOMA | 126 | MUSOMA VIJIJINI |
| | | WILAYA YA RORYA | 127 | RORYA |
| | | WILAYA YA SERENGETI | 128 | SERENGETI |
| | | WILAYA YA TARIME | 129 | TARIME |
| 17. | MBEYA | WILAYA YA ILEJE | 130 | ILEJE |
| | | JIJI LA MBEYA | 131 | MBEYA MJINI |
| | | MJI WA TUNDUMA | 132 | TUNDUMA |

| Na. | MKOA | HALMASHAURI | Na | JIMBO |
|---|---|---|---|---|
| | | WILAYA YA BUSOKELO | 133 | BUSOKELO |
| | | WILAYA YA CHUNYA | 134 | LUPA |
| | | WILAYA YA CHUNYA | 135 | SONGWE |
| | | WILAYA YA KYELA | 136 | KYELA |
| | | WILAYA YA MBARALI | 137 | MBARALI |
| | | WILAYA YA MBEYA | 138 | MBEYA VIJIJINI |
| | | WILAYA YA MBOZI | 139 | MBOZI |
| | | WILAYA YA MBOZI | 140 | VWAWA |
| | | WILAYA YA MOMBA | 141 | MOMBA |
| | | WILAYA YA RUNGWE | 142 | RUNGWE |
| | | WILAYA YA MAGHARIBI A | 143 | BUBUBU |
| | MJINI MAGHARIBI | WILAYA YA MAGHARIBI A | 144 | WELEZO |
| | | WILAYA YA MAGHARIBI A | 145 | MFENESINI |
| 18. | | WILAYA YA MAGHARIBI A | 146 | MWERA |
| | | WILAYA YA MAGHARIBI B | 147 | DIMANI |
| | | WILAYA YA MAGHARIBI B | 148 | FUONI |
| | | WILAYA YA MAGHARIBI B | 149 | KIEMBE SAMAKI |
| | | WILAYA YA MAGHARIBI B | 150 | MWANAKWEREKWE |
| | | WILAYA YA MJINI | 151 | KIJITOUPELE |
| | | WILAYA YA MJINI | 152 | AMANI |
| | | WILAYA YA MJINI | 153 | CHUMBUNI |
| | | WILAYA YA MJINI | 154 | JANG'OMBE |
| | | WILAYA YA MJINI | 155 | KIKWAJUNI |
| | | WILAYA YA MJINI | 156 | KWAHANI |
| | | WILAYA YA MJINI | 157 | MAGOMENI |
| | | WILAYA YA MJINI | 158 | MALINDI |
| | | WILAYA YA MJINI | 159 | MPENDAE |
| | | WILAYA YA MJINI | 160 | SHAURIMOYO |
| | | WILAYA YA KILOMBERO | 161 | MLIMBA |
| | | MANISPAA YA MOROGORO | 162 | MOROGORO MJINI |
| | MOROGORO | WILAYA YA GAIRO | 163 | GAIRO |
| 19. | | WILAYA YA KILOMBERO | 164 | KILOMBERO |

| Na. | MKOA | HALMASHAURI | Na | JIMBO |
|---|---|---|---|---|
| | | WILAYA YA KILOSA | 165 | KILOSA |
| | | WILAYA YA KILOSA | 166 | MIKUMI |
| | | WILAYA YA MOROGORO | 167 | MOROGORO KUSINI |
| | | WILAYA YA MOROGORO | 168 | MOROGORO KUSINI MASHARIKI |
| | | WILAYA YA MVOMERO | 169 | MVOMERO |
| | | WILAYA YA ULANGA | 170 | ULANGA |
| | | WILAYA YA MALINYI | 171 | MALINYI |
| 20. | MTWARA | WILAYA YA MTWARA | 172 | MTWARA VIJIJINI |
| | | MANISPAA YA MTWARA MIKINDANI | 173 | MTWARA MJINI |
| | | MJI WA MASASI | 174 | MASASI MJINI |
| | | MJI WA NANYAMBA | 175 | NANYAMBA |
| | | MJI WA NEWALA | 176 | NEWALA MJINI |
| | | WILAYA YA MASASI | 177 | LULINDI |
| | | WILAYA YA MASASI | 178 | NDANDA |
| | | WILAYA YA NANYUMBU | 179 | NANYUMBU |
| | | WILAYA YA NEWALA | 180 | NEWALA VIJIJINI |
| | | WILAYA YA TANDAHIMBA | 181 | TANDAHIMBA |
| 21. | MWANZA | MANISPAA YA ILEMELA | 182 | ILEMELA |
| | | JIJI LA MWANZA | 183 | NYAMAGANA |
| | | WILAYA YA BUCHOSA | 184 | BUCHOSA |
| | | WILAYA YA KWIMBA | 185 | KWIMBA |
| | | WILAYA YA KWIMBA | 186 | SUMVE |
| | | WILAYA YA MAGU | 187 | MAGU |
| | | WILAYA YA MISUNGWI | 188 | MISUNGWI |
| | | WILAYA YA SENGEREMA | 189 | SENGEREMA |
| | | WILAYA YA UKEREWE | 190 | UKEREWE |
| 22. | NJOMBE | MJI WA MAKAMBAKO | 191 | MAKAMBAKO |
| | | MJI WA NJOMBE | 192 | NJOMBE MJINI |
| | | WILAYA YA LUDEWA | 193 | LUDEWA |
| | | WILAYA YA MAKETE | 194 | MAKETE |
| | | WILAYA YA NJOMBE | 195 | LUPEMBE |
| | | WILAYA YA | 196 | WANGING'OMBE |

| Na. | MKOA | HALMASHAURI | Na | JIMBO |
|---|---|---|---|---|
| | | WANGING'OMBE | | |
| 23. | PWANI | MJI WA KIBAHA | 197 | KIBAHA MJINI |
| | | WILAYA YA BAGAMOYO | 198 | BAGAMOYO |
| | | WILAYA YA CHALINZE | 199 | CHALINZE |
| | | WILAYA YA KIBAHA | 200 | KIBAHA VIJIJINI |
| | | WILAYA YA KISARAWE | 201 | KISARAWE |
| | | WILAYA YA MAFIA | 202 | MAFIA |
| | | WILAYA YA MKURANGA | 203 | MKURANGA |
| | | WILAYA YA RUFIJI | 204 | KIBITI |
| | | WILAYA YA RUFIJI | 205 | RUFIJI |
| 24. | RUKWA | MANISPAA YA SUMBAWANGA | 206 | SUMBAWANGA MJINI |
| | | WILAYA YA KALAMBO | 207 | KALAMBO |
| | | WILAYA YA NKASI | 208 | NKASI KASKAZINI |
| | | WILAYA YA NKASI | 209 | NKASI KUSINI |
| | | WILAYA YA SUMBAWANGA | 210 | KWELA |
| 25. | RUVUMA | WILAYA YA NYASA | 211 | NYASA |
| | | WILAYA YA SONGEA | 212 | PERAMIHO |
| | | MANISPAA YA SONGEA | 213 | SONGEA MJINI |
| | | MJI WA MBINGA | 214 | MBINGA MJINI |
| | | WILAYA YA MADABA | 215 | MADABA |
| | | WILAYA YA MBINGA | 216 | MBINGA VIJIJINI |
